DSPACE

https://dspace.org/

# Changamoto zinazohusu usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama ya Kericho, Kenya.

**Machani, Jane**

**2017-06**
University of Kabianga
http://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/110

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

# CHANGAMOTO ZINAZOHUSU USAWA WA VIPENGELE VYA LUGHA KATIKA UKALIMANI WA DISKOSI ZA WAHUSIKA KATIKA UENDESHAJI WA KESI KATIKA MAHAKAMA YA KERICHO, KENYA.

**Na**

**Jane Machani**

**KPG/KIS/004/13**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KUTAHINIWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KABIANGA**

**IDARA YA ISIMU, FASIHI NA MAWASILIANO: KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA JAMII**

**CHUO KIKUU CHA KABIANGA**

**JUNI, 2017**

## UNGAMO NA IDHINI

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia ila sehemu ambazo nimezinukuu kwa ajili ya utafiti huu. Kazi hii haijawahi kutolewa kutahiniwa kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kingine chochote.

Jane Machani: PGC/KIS/004/13

Sahihi: ______________________Tarehe: _______________________

Tasnifu hii imewasilishwa na kutolewa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Kabianga.

<u>Wasimamizi</u>

Profesa Issa Mwamzandi

Idara ya Isimu, Fasihi na Mawasiliano: Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii,

Chuo Kikuu cha Kabianga.

Sahihi: _________________ Tarehe: ____________________________

Dkt. Simiyu Kisurulia

Idara ya Isimu, Fasihi na Mawasiliano: Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii,

Chuo Kikuu cha Kabianga.

Sahihi: ___________________Tarehe: _________________________

## HAKI ZA KUNAKILI

© Haki ya kunakili ni ya mtafiti, 2017

Haki zote zimehifadhiwa. Sehemu yoyote ya hii tasnifu hairuhusiwi kuigwa, kunakiliwa, kupigwa chapa au kutolewa kwa manufaa ya kibinafsi na yeyote kwa jinsi yoyote bila idhini ya mwandishi au ya Chuo Kikuu cha Kabianga ila kwa utafiti zaidi katika taaluma maalumu ili kuongeza maarifa zaidi.

## TABARUKU

Natabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu, Bw. Machani na Marehemu Bi. Kwamboka kwa kunilea kwa hali na mali, kunielimisha na kunihimiza kufanya lolote maishani kwa bidii na uvumilivu. Mlinifunza umuhimu wa elimu na kwamba elimu haina mwisho maishani.

# SHUKURANI

Ninaungama kuwa kazi hii haingekamilika bila ya usaidizi, maelekezo na mchango wa watu wengi. Ni vigumu kuwataja wote katika nafasi hii. Nitawataja baadhi yao tu.

Mosi, ninamshukuru kwa dhati Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema, maarifa na uwezo wa kuiandika tasnifu hii.

Shukrani zangu za dhati pia zinawaendea majaji, mawakili, makarani na maafisa wote katika mahakama ya Kericho kwa kunishughulikia kwa mioyo mikunjufu katika kila hatua ya ukusanyaji data katika mahakama kuu ya Kericho. Usaidizi wao uliniwezesha kuelewa hali ya ukalimani na namna ya kupata data yangu kutoka vyumba mbalimbali ambapo vikao vya kesi viliendeshwa.

Ninawatolea shukrani za dhati wasimamizi wangu, Profesa Issa Mwamzandi na Daktari Simiyu Kisurulia, kwa kunihimiza bila kuchoka muda wote nilipokuwa ninaandika kazi hii tangu mwanzo hadi mwisho. Walinitia shime katika kila hatua za uandishi wa kazi hii na kupitia kila sehemu kwa makini ili kuniwezesha kukamilisha utafiti wangu. Maelekezo yao ya kitaaluma yaliniwezesha kukazana kuiboresha na kuikamilisha kazi hii kwa wakati. Mwenyezi Mungu awabariki na kuwajalia busara na afya njema maishani.

Ninawashukuru pia kwa dhati na taadhima kuu wahadhiri wangu wote ambao walinifunza katika Idara ya Isimu, Fasihi na Mawasiliano katika Chuo Kikuu cha Kabianga. Walinifungua macho, wakanielekeza na kunihimiza katika bahari hii kuu ya usomi. Wahadhiri wangu watukufu, Profesa Issa Mwamzandi, DaktariSimiyu Kisurulia, Daktari Samuel Obuchi Moseti na Daktari Mark Kandagor, Mungu azidi kuwapa hekima ili muendeleze shughuli hii ya kuimarisha lugha ya Kiswahili.

Ninawashukuru wenzangu ambao tulikuwa tukiabiri pamoja meli hii katika maji makuu ya kutafuta shahada hii ya uzamili na kuhimizana mara kwa mara hadi mwisho wa safari hii. Wenzangu Bw. Gedion Kipsang, Bi. Korir Esther, Bi. Chemutai Emily na Bi. Kiberenge Clare; Mungu azidi kuwapa nguvu na imani katika shughuli zenu.

Sitasahau kumshukuru mume wangu, Bw. David Nyamweya kwa kunihimiza kuendeleza elimu yangu. Pia, wanangu Lewis, Brian na George ambao walinihimiza na kunipa muda wa kushughulikia kazi hii, kunipigia chapa na wakati mwingine kusahihisha makosa ambayo mimi mwenyewe nilikosa kuyagundua wakati wa kuidurusu kazi yangu. Nawaombea Rabana awamiminie hekima na hisani katika mambo yenu yote maishani mwenu!

Asanteni!

# IKISIRI

Utafiti huu umechunguza changamoto zinazohusu usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama ya Kericho, Kenya. Utafiti huu ulifanywa katika mahakama kuu ya Kericho, Kaunti ya Kericho, Kenya. Uchunguzi huu ulishughulikia changamoto kuhusu usawa wa vipengele vya ujumbe, mtindo, maumbo na toni katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi mbalimbali katika lugha husika wakati wa uendeshaji wa kesi katika mahakama hiyo. Madhumuni kuu ya utafiti huuyalikuwakubainisha changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika mahakama.Uchunguzi shirikishi ulitumiwa katika kukusanya data za utafiti huu. Diskosi za wahusika wa kesi katika vikao vya kesi sita ambazo zilichukua muda kati ya dakika kumi na tano hadi dakika arobaini na tano ziliteuliwa kutoka miongoni mwa diskosi za kesi kadhaa. Uteuzi wa diskosi hizi ulifanywa kwa kutumia sampuli nasibu horomo na sampuli makusudi. Data hizi zilikusanywa kati ya mwezi June hadi Agosti, 2016. Wahusika katika kesi sita husika ambao walihitaji usaidizi wa wakalimani walikuwa wa umri mbalimbali ambao hawakumaizi lugha ya Kiingereza vizuri, lugha rasmi ya mahakama ambayo hutumiwa na jaji, wakili na maafisa wengine wa mahakama. Wengi wa wahusika hao walikuwa vijana na walikuwa watu wa tabaka la chini katika jamii. Wakalimani waliohusika katika vikao vya kesi mbalimbali walikuwa wanane.Wakalimani, ambao pia ni makarani, hawakuwa na mafunzo maalum kuhusu ukalimani wala tafsiri kabla ya kuajiriwa kuwa makarani katika mahakama lakini baadhi yao wamepokea mafunzo ya muda mfupi kuhusu taaluma hii na wamepata tajriba ya kazi yao kutokana na muda waliofanya kazi hii. Nadharia ya usawa katika taaluma ya tafsiri ilitumiwa katika kuchanganua data zilizokusanywa. Nadharia ya usawa inadaiwa kuwa msingi imara watafsiri kwa sababu inamkumbusha mkalimani kuwa atakumbwa na changamoto tele za usawa wa vipengele vya lugha katika shughuli ya ukalimani. Pia, inaeleza kuwa hakuna lugha mbili ambazo zinaweza kutumia leksimu, virai, vishazi na sentensi sawa kuashiria kitu kimoja. Kwa hivyo, usawa katika ukalimani na tafsiri ni jambo la kukisia. Utafiti huu umechanganua majibu ya hojaji na diskosi zilizorekodiwa kwa kinasasauti na pia kunakiliwa katika daftari maalumu la mtafiti ili kubainisha changamoto za usawa wa vipengele vya ujumbe, maumbo, mitindo na toni katika ukalimani. Uchanganuziuliofanywa ulikuwa wa kistahilifu wala si wa kitakwimu. Iligunduliwa kuwa wakalimani walikumbwa na changamoto za usawa wa vipengele vyote vya lugha ingawa walijaribu kadiri ya uwezo wao kukalimani diskosi husika. Inapendekezwa kwamba ni muhimu kwa wanasheria kuibua msamiati mwafaka wa kutumiwa katika mahakama ili kurahisisha kazi ya wakalimani katika mahakama.

**ABSTRACT**

This study examinesthe challenges of equivalence in the interpretation of courtroom discourses of various actors in case proceedings in Kericho Law Courts, Kenya. The research was carried out in Kericho law courts to find out the challenges of equivalence in language issues in interpreting discourses of actors in various cases during the case proceedings. The purpose of this study was to find out the challenges of equivalence that interpretors encountered in the interpretation of discourses occurring during case proceedings. In essence, the study was intended to examine the challenges of interpretation of language issues such as messages, forms, styles and tone. The observation method was used to collect data.Disourses of six case proceedings were selected for analysis. The case proceedings took between fifteen to forty five minutes each. The data was collected for a period of eight weeks in the months of June and August 2016. Case proceedings were randomly and purposively sampled. The actors in these six cases selected needed the services of the interpretor because they did not understand English, the official language of the courtroom used by the judge and other officials. It was observed that most of those participants who could not understand English were young people and low-class folks in society. Eight interpretors were involved in various case proceedings. The theory of equivalence was used to analyse the data selected according to the objectives of the study. The theory of equivalence states that equivalence is the foundation of translation because it reminds the interpreter that he will encounter many challenges of language issues in his work of interpreting discourses from one language to another. It also states that there exists no two languages that are similar in forms such as word, clauses, phrases and sentences. The data analysed was from the questionnaire, the discourses recorded in writing and mainly that was recorded in the voice recorder during the court proceedings. Only the interpreted discourses were of interest in this study. The challenges of equivalence in language issues were centred on message, forms, styles and tone in the ST and its interpretation in the TT. The analysis used was that of the qualitative nature and not quantitative in nature. The interpreters, who were also court clerks, had no prior formal education in translation before their employment but some have received training on the same during short courses and more importantly they have learnt through experience in their job as everyday inerpretors whenever they are needed. It is worthy noting that although the interpretors did not have prior training, they did their best in the job of interpreting the message in the discourses. They went about it through explanations, borrowing and adaptation of the English vocaburary that was used in the ST. Even then the interpretors had challenges in getting the right vocaburary and therefore were forced to use the same words as used, or dropped some or added some words which they deemed necessary. In that case, the meaning intended in the ST changed drastically. It is hereby recommended that it isnecessary that legal officers come up with language equivalence in the vocaburaries used in case proceedings to ease the work of interpretors in court.

**YALIYOMO**


UNGAMO ..... i
HAKI ZA KUNAKILI ..... ii
TABARUKU ..... iii
SHUKURANI ..... iv
IKISIRI ..... vi
ABSTRACT ..... vii
YALIYOMO ..... viii
AKRONIMU ..... xiii
UFAFANUZI WA DHANA NA ISTILAHI MUHIMU ..... xiv
SURA YA KWANZA ..... 1
UTANGULIZI ..... 1
1.0 Kichocheo ..... 1
1.1 Usuli wa Utafiti ..... 1
1.2 Suala la Utafiti ..... 7
1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti ..... 8
1.3.2 Malengo Mahususi ya Utafiti ..... 8
1.4 Maswali ya Utafiti ..... 8
1.5 Ufaafu wa Utafiti ..... 9
1.6 Umuhimu wa Utafiti Huu ..... 11
1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti ..... 12
1.8 Machukulio ..... 13
SURA YA PILI ..... 14
MAPITIO YA MAANDISHI KUHUSU MADA ..... 14
2.0 Utangulizi ..... 14
2.1 Dhana ya Ukalimani ..... 14
2.1.1 Historia Fupi na Maendeleo ya Ukalimani ..... 15
2.1.2 Umuhimu wa Ukalimani ..... 19
2.1.3 Aina za Ukalimani ..... 20
2.1.3.1 Ukalimani Mfululizo ..... 20
2.1.3.2 Ukalimani Fuatizi ..... 22

2.1.3.3 Ukalimani Muono....23
2.1.3.4 Ukalimani Muhtasari....24
2.1.4 Stadi Muhimu Kuhusu Mkalimani na Mfasiri Bora....24
2.1.5 Dhana ya Tafsiri....26
2.1.5.1 Historia Fupi na Maendeleo ya Tafsiri....28
2.1.5.2 Enzi ya Kale....29
2.1.5.3 Enzi ya Giza....30
2.1.5.4 Enzi ya Ufufuko....30
2.1.5.5 Enzi ya Kati....31
2.1.5.6 Enzi ya Sasa....32
2.1.6 Uhusiano Baina ya Ukalimani na Tafsiri....33
2.1.6.1 Tofauti Baina ya Tafsiri na Ukalimani....33
2.1.6.2 Kufanana kwa Tafsiri na Ukalimani....35
2.2 Nadharia ya Usawa....36
2.2.1 Mawazo ya Catford (1965) Kuhusu Nadharia ya Usawa....37
2.2.2 Mawazo ya Nida (1969) Kuhusu Nadharia ya Usawa Unaobadilika....38
2.2.3 Mawazo ya Komissarov (1978) Kuhusu Usawa Elekezi na Uliotapanyika....39
2.2.4 Mawazo ya Koller (1979) Kuhusu Usawa....40
2.3 Dhana ya Utamaduni....46
2.3.1 Uhusiano Kati ya Lugha na Utamaduni....48
2.3.2 Utamaduni, Tafsiri na Ukalimani....50
2.3.3 Mambo Magumu Kutafsiri na Kukalimani kwa Kuzingatia Utamaduni....51
2.3.4 Mikakati Katika Kutafsiri na Kukalimani kwa Kuzingatia Utamaduni....53
2.4 Yaliyoandikwa Kuhusu Suala la Ukalimani Katika Mahakama....56
2.4.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Usawa wa Ujumbe Katika Ukalimani wa Diskosi Katika Mahakama....56
2.4.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Usawa wa Maumbo Katika Ukalimani wa Diskosi Katika Mahakama....59
2.4.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Usawa wa Mtindo Katika Ukalimani wa Diskosi Katika Mahakama....60
2.4.4 Yaliyosemwa Kuhusu Usawa wa Ukalimani wa Toni Katika Diskosi Katika Mahakama..62

2.5 Wazo la Utafiti ....................................................................................................63
2.6 Utambuzi wa Pengo la Utafiti ....................................................................................................63
2.7 Hitimisho....................................................................................................64
SURA YA TATU ....................................................................................................66
MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI ....................................................................................................66
3.0 Utangulizi....................................................................................................66
3.1 Muundo wa Utafiti....................................................................................................66
3.2.1 Mahali pa Kukusanya Data ....................................................................................................67
3.2.2 Jumuiya ya Utafiti....................................................................................................69
3.3.1 Usampulishaji ....................................................................................................69
3.3.2 Vibadala Katika Utafiti ....................................................................................................70
3.4 Vifaa vya Utafiti ....................................................................................................71
3.5 Utaratibu wa Kukusanya Data....................................................................................................71
3.6 Uchanganuzi wa Data ....................................................................................................72
3.7 Masuala ya Kimaadili ....................................................................................................75
3.8 Mahitimisho ....................................................................................................76
SURA YA NNE....................................................................................................77
UCHANGANUZI WA DATA ....................................................................................................77
4.0 Utangulizi....................................................................................................77
4.1.1 Matokeo ya Hojaji kwa Wakalimani ....................................................................................................77
4.1.2 Sababu za Kuteua Data za Kesi Hizo ....................................................................................................79
4.2 Matokeo ya Uchanganuzi wa Data za Kesi Hizo ....................................................................................................80
4.3 Changamoto za Usawa wa Ujumbe Katika Ukalimani wa Diskosi za Wahusika...............80
4.3.1 Dhana ya Ujumbe....................................................................................................81
4.3.2 Ujumbe Uliokalimaniwa Vilivyo Katika Diskosi za Wahusika wa Kesi.....................82
4.3.3 Ujumbe Uliokalimaniwa Visivyo Katika Diskosi za Wahusika wa Kesi ....................87
4.3.4. Ujumbe Uliochopekwa....................................................................................................98
4.3.5 Ujumbe Uliodondoshwa ....................................................................................................100
4.4 Changamoto Kuhusu Usawa wa Kipengele cha Maumbo....................................................................................................106
4.4.1 Dhana ya Maumbo ....................................................................................................107
4.4.2 Maumbo ya Leksimu Kimofolojia ....................................................................................................108

4.4.3 Maumbo ya Virai na Vishazi ........ 111
4.4.4 Maumbo ya Kisintaksia ........ 116
4.5 Changamoto za Usawa wa Kipengele cha Mtindo ........ 118
4.6 Changamoto Kuhusu Usawa wa Kipengele cha Toni Katika Ukalimani ........ 123
4.6.1 Dhana ya Toni ........ 123
4.6.2 Toni Iliyokalimaniwa Vilivyo ........ 124
4.6.3 Toni Iliyokosa Kukalimaniwa Vilivyo ........ 130
4.7 Majibu kwa Maswali ya Utafiti ........ 133
4.8 Hitimisho ........ 137
SURA YA TAN0 ........ 138
MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 138
5.0 Utangulizi ........ 138
5.1 Muhtasari ........ 138
5.2 Mahitimisho ........ 143
5.3 Mapendekezo ........ 145
MAREJELEO ........ 148
VIAMBATISHO ........ 152
(a)(i) Barua ya kujitambulisha ........ 152
(ii) Hojaji kwa Wakalimani ........ 153
(b) Barua Kutoka Chuo Kikuu cha Kabianga ........ 155
(c) Barua ya Kibali kwa Utafiti Kutoka NACOSTI ........ 156
(d) Cheti cha Utafiti Kutoka NACOSTI ........ 157
(e) Barua ya Mkurugenzi wa Elimu Kaunti ya Kericho ........ 158
(f) Barua ya Kamishna wa Polisi Kericho ........ 159
(g) Barua ya Mkurugenzi wa Mahakama ya Kericho ........ 160
Data Iliyoteuliwa ........ 161
Kesi A ........ 161
Kesi B ........ 163
Kesi C ........ 165
Kesi D ........ 169
Kesi E ........ 171

Kesi F ........................................................................................................................ 173

## AKRONIMU

**ICC**- International Criminal Court

**Km**- Kiongozi wa mashtaka

**LA**- Lugha Asilia

**LC**-Lugha Chanzi

**LL-**LughaLengwa

**LP-** LughaPokezi

**MC -** Matini Chanzi

**Mk**-Mkalimani

**ML** - Matini Lengwa

**MP**- Matini Pokezi

**Mst**- Mshtakiwa

## UFAFANUZI WA DHANA NA ISTILAHI MUHIMU

**Diskosi-** Ni jumla ya mambo ambayo yanaandamana na maongezi, maneno, mazungumzo au hotuba ili kufanikisha ujumbe wa mzungumzaji kwa wasikilizaji wake. Mambo hayo hujumuisha lugha, muktadha, utamaduni, semiotiki, sauti, toni za kihisia, kidatu na mwonoulimwengu wa msemaji na wasikilizaji.

**Kisawe/Usawa-** Ni neno, kirai, kishazi, sentensi au mafungu ya maneno katika lugha lengwa ambayo maana na matumizi yake yanalingana au kukaribiana kimaana na yale ya neno, kirai, kishazi, sentensi au mafungu ya maneno katika lugha chanzi.

**Matini-** Ni mawazo au mfululizo wa mawazo ambao unajitosheleza kimaana hata kama ni neno moja, kirai, kishazi, sentensi, aya, kifungu cha habari, sura au kitabu kizima.

**Mkalimani-** Mtu yeyote anayejishughulisha na kazi ya kutafsiri papo kwa papo na ana ujuzi wa kutafsiri. Pia, huitwa mfasiri au mtarijumani.

**Ujumbe** – Hili ni wazo kuu linalowasilishwa katika matini. Wazo lenyewe laweza kuwa la kisemantiki au la kipragmatiki. Mkalimani anafaa azingatie kile ambacho mhusika anataka kuwasilisha kutokana na muktadha.

**Umboaumuundo**– Huu ni muundo au sura ya kitu. Katika makala haya, maumbo yatajumuisha; mofimu, maneno, virai, vishazi na sentensi zitakazotumika katika diskosi husika na tafsiri zao.

**Mtindo** - Mtindo katika makala haya lina maana sawa na tamathali za lugha ambazo zitajitokeza katika diskosi za wahusika wa kesi mbalimbali. Huu ni ufundi au ujuzi wa kujieleza kwa kutumia lugha. Vipengele vya mtindo ni pamoja na; jazanda, tashbihi, tasfida, istiara, methali na

misemo. Hii mitindo itategemea namna wahusika watateua msamiati wa lugha watakayoitumia. Hii ni kwa sababu kila mhusika ana namna ya kipekee ya kujieleza.

**Toni** – Hizi ni hisia ambazo zinaandamana na ujumbe wa mhusika anapowasilisha ujumbe huo katika diskosi yake. Hisia hizi zinaweza kuathiri ujumbe au maana ya maneno yaliyosemwa na mhusika. Katika tafsiri na ukalimani, hiki ni kigezo muhimu ambacho kinafaa kuzingatiwa na mkalimani. Hisia zaweza kuwa za huzuni, masikitiko, furaha, mapuuza, majuto, kejeli, hasira, dharau au upendo kutegemea ujumbe wa mhusika. Hisia huweza kutambuliwa kutokana na uteuzi wa msamiati anaotumia mhusika, kidatu na kiimbo cha sauti ya mhusika.

**Tafsiri-** Hili ni jaribio la kuwasilisha ujumbe ule ule kupitia maandishi kutoka lugha moja hadi lugha nyingine.

**Ukalimani-** Ni uhawilishaji wa ujumbe kutoka LC hadi LL papo kwa papo kwa mazungumzo. Matini iliyozungumzwa uhawilishwa kutoka lugha moja hadi nyingine.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Kichocheo

Sehemu hii inajumuisha; usuli wa utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, ufaafu wa utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, mahali pa kufanyia utafiti huu na machukulio katika utafiti huu. Sehemu hii imeeleza namna mtafiti aligundua pengo la utafiti na umuhimu wa utafiti huu pamoja na ufaafu wake kwa wakalimani, wahusika wa kesi katika mahakama, jamaa za wahusika wa kesi, wanajamii kwa jumla na wataalamu wa lugha.

## 1.1 Usuli wa Utafiti

Suala la usawa katika tafsiri limekuwa na utata kwa muda mrefu na limejadiliwa katika vikao mbalimbali vya kitaalamu. Utata huo umetolewa maoni na wataalamu na wahusika mbalimbali wa kesi katika mahakama kuhusu ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi. Kwa mfano,

Wataalamu wa taaluma ya tafsiri, Hale na Gibson (1999) wameeleza kuwa tafsiri ni harakati iliyo na dosari nyingi katika ulimwengu wenye dosari. Hii ni kutokana na ukosefu wa visawe vinavyoashiria kiashiriwa kimoja katika LC na LP. Pia, diskosi ambazo zimetafsiriwa ni tofauti tofauti kwa sababu wahusika hutofautiana kutokana na muonoulimwengu wao tofauti. Mara nyingi, wanasheria wanataka wakalimani watafsiri vipengele vya LC kwa kutumia visawe vya vipengele hivyo katika LP katika diskosi za wahusika kama zinavyotokea katika LC. Wakalimani hawana muda wa kutafuta kisawe mwafaka katika kamusi. Tafsiri yao ni ya papo kwa papo diskosi hizo zinapotokea katika uendeshaji wa kesi katika mahakama. Hivyo basi,

wakalimani hao hukumbwa na changamoto tele za usawa wa vipengele vya lugha kwa sababu msamiati mwafaka huenda ukawakwepa katika harakati za tafsiri ya papo kwa papo.

Kwa mujibu wa Olsen na wengine (2009) ni kama ndoto kwa wanasheria kutarajia tafsiri ya ML kulandana na ile ya MC kwani shughuli ya tafsiri ina changamoto nyingi. Maoni haya yalizua wazo la kuchunguza changamoto za usawa wa vipengele vya lugha husika zilizowakumba wakalimani kwa kuzingatia vipengele vya ujumbe, maumbo, mtindo na toni katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi katika uendeshaji wa kesi katika mahakama.

Kulingana na Milton na Bandia (2009) mkalimani anafaa kuwa na ujuzi wa hali ya juu ili kuweza kutafsiri ujumbe kwa usawa kutoka LC hadi LL bila kupoteza usawa wa vipengele muhimu ambavyo vimejikita katika MC. Katika utafiti huu, uchunguzi umefanywa ili kutathmini iwapo wakalimani walikuwa na ujuzi wa kutafsiri kwa usawa vipengele vya ujumbe, maumbo, mtindo na toni katika diskosi za wahusika wa kesi mbalimbali katika mahakama. Utafiti huu umechunguza changamoto za usawa wa vipengele vya lugha zilizowakabili wakalimani katika shughuli nzima ya ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi mbalimbali katika mahakama.

Aiello (2013) ameeleza kuwa mkalimani anafaa kutumia mbinu nyingi bunifu ili kufikia usawa wa vipengele vyote vya lugha katika matini chanzi. Inabidi mkalimani aweke mikakati maalumu ili kufikia usawa wa matini akizingatia utamaduni, jamii-lugha, dini, imani na tamathali za lugha zilizotumiwa katika MC. Mbinu bunifu zinazotumika mara nyingi huwa ni maelezo, uchopekaji, udondoshaji, ukopaji na hata matumizi ya tamathali za LP ambazo zinakaribiana kimaana na kimatumizi na za LC. Wakati mwingine, mkalimani anaweza kutumia tamathali za usemi katika ML hata ingawa hazikutumika katika MC. Katika utafiti huu, mtafiti amechunguza changamoto ambazo mkalimani anakumbwa nazo anapotafuta usawa wa vipengele vya lugha. Pia, ametafiti

mbinu bunifu mwafaka ambazo wakalimani hutumia katika matini pokezi ili kufikia usawa wa vipengele vya ujumbe, maumbo, mtindo na toni ya MC.

Armstrong (2005) anadai kuwa tafsiri bora ya MC inastahili kulandana kabisa na ile ya ML kiujumbe, kimaumbo, kimtindo na kitoni. Mawazo haya ni sawa na ya Venuti (1995) anayedai kuwa maumbo (maneno, virai, vishazi, sentensi na viunganishi) hufaa kuwa sawa kama kioo ambacho hakistahili kugunduliwa kuwa kipo mpaka kiwe na uchafu wa aina fulani ambao haustahili kuwepo hasa katika taaluma ya kisheria. Lakini je, inawezekana tafsiri ifikie kiwango hicho? Hata hivyo, alieleza kuwa maana ya neno hutegemea maana ya maneno yanayoshirikiana nalo katika muktadha wa matumizi yake. Mawazo ya Armstrong na Venuti ni kinyume na ya Hale na Gibson (1999) waliodai kuwa usawa katika tafsiri ni kama ndoto hasa katika taaluma ya kisheria. Hii ndiyo sababu utafiti huu ulifanywa ili kuziba pengo la changamoto zinazohusu usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama kwani ni wazi kuwa zipo changamoto ambazo hufanya tafsiri mwafaka kuonekana kuwa ndoto kwa wataalamu hawa.

Kwa mujibu wa Namakula (2013), matumizi ya lugha nyingi za jamii mbalimbali katika mahakama, kwa ajili ya kutekeleza haki za wahusika wa kesi wasioelewa lugha ya Kiingereza, huathiri matokeo ya kesi na kuwanyima haki wahusika hao. Ameeleza kuwa ni vigumu kupata usawa baina ya lugha mbili zenye tamaduni tofauti. Amefafanua kuwa hata wakalimani walijipata matatani walipokalimani diskosi za wahusika kwa kutumia visawe mahususi vya lugha husika. Ametoa mfano wa mkalimani mmoja aliyekemewa na hakimu kuwa alikosa nidhamu katika mahakama kwa kutumia kisawe mahususiambacho kilikuwa lugha matusi kwa mujibu wa jaji wa mahakama hiyo. Mkalimani huyo alielekezwa na jaji atumie tasfida ili kuficha

lugha chafu ya shahidi. Kutokana na hali hii, ni wazi kuwa wakalimani wanakumbwa na changamoto za usawa wa vipengele vya lugha wanazozitumia katika mahakama kwa sababu wanahitajika kutumia tasfida badala ya kutafsiri msamiati uliotumiwa kisemantiki. Baadhi ya tasfida husika hukosa kufasiri ujumbe uliokusudiwa katika MC. Utafiti huu, umechunguza changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi zawahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama ya Kericho, Kenya. Namakula alitumia data kutoka mahakama kuu ya kimataifa, Uganda.

Owiti (2014) ameeleza kuwa ujumbe uliokusudiwa ulipotea pale wakalimani walipodondosha au kuchopeka baadhi ya maneno katika MP wakati wa kukalimani diskosi za wahusika katika mahakama ndogo ya Nyando, Kenya. Alidhihirisha kuwa wakalimani walikabiliwa na changamoto za usawa wa vipengele fulani vya lugha. Hii ndiyo sababu walidondosha au kuchopeka baadhi ya maneno katika MP. Hali hii iliishia kubadilisha au kupoteza ujumbe uliokusudiwa na msemaji. Kwa kufanya hivyo, huenda walimkosesha mhusika haki yake. Katika utafiti huu, mtafiti amezichunguza changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi katika mahakama. Amebainisha mambo yaliyosababisha kuwepo kwa changamoto za vipengele vya ujumbe, mtindo, maumbo na toni baina ya LC na LL.

Odhiambo (2013) aligundua kwamba wakalimani katika Mkoa wa Nyanza hawakuwa na mafunzo yoyote kuhusiana na ukalimani wa lugha zote mbili walizozitumia ingawa baadhi yao walikuwa na mafunzo kuhusiana na tafsiri ya ishara. Zaidi ya hayo, hawakuwa na mafunzo yoyote kuhusiana na namna wanavyokalimani lugha ya taaluma ya kisheria. Odhiambo alitafiti hali ya wakalimani katika shughuli ya ukalimani baina ya lugha ya Kiingereza na Dholuo. Utafiti

huu wa Odhiambo ulisaidia katika kuelekeza utafiti huu katika kuchunguza changamoto za usawa wa vipengele vya ujumbe, maumbo, mtindo na toni katika ukalimani baina ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Hii ni kwa sababu usawa unaotafutwa na mkalimani katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi katika mahakama ni ule wa ujumbe, umbo, mtindo na toni kama inavyojitokeza katika LC ili kufanikisha ukalimani lakini baadhi ya wakati malengo hayo ya ukalimani hayatimizwi. Changamoto za usawa wa vipengele vya lugha zinazowakabili wakalimani zimefafanuliwa katika utafiti huu.

Gazeti la Taifa Leo, Kenya, (22-09-13: 15-16) liliripoti habari kuhusu kesi katika mahakama ya kimataifa (ICC), huko Uholanzi, iliyowakabili mtangazaji wa kituo cha *KassRedio* Bwana Joshua Sang na Naibu wa Rais wa Kenya, Mheshimiwa William Samoei Ruto. Taarifa hiyo ilidai kuwa kesi hiyo ilikumbwa na changamoto kuhusu usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani si haba. Shughuli za ukalimani zilizua wasiwasi kwa mawakili na washukiwa. Huko Uholanzi, kulizuka upinzani iwapo msamiati *'kutembea*' na '*kusafiri'* ni tafsiri sawa kulingana na ukalimani uliotolewa. *'Je, mtu anaweza kutembea kwa baiskeli?'* Bwana Nderitu, wakili wa waathiriwa alikuwa na wasiwasi iwapo tafsiri ya msamiati huo iliambatana na maana ya matumizi ya msamiati huo nchini Kenya. Msamiati mwingine uliozua mtafaruku ni; '*Vinyasa'* (shorts) uliofasiriwa kuwa 'nyasi' (grass), 'kundi' (group) likawa 'adui' (enemy), na 'kusafiri' (travel) likawa 'kutembea' (have a leasurely walk). Wakili wa Bw. Joshua Sang, Bw. Katwa Kigen, alidai kuwa;'*katika siku zijazo mahakama ya ICC itahitaji kuwa na mkalimani ambaye anaelewa matumizi ya Kiswahili katika muktadha wa Kenya nchini Kenya ili kuipatia misamiati ufasiri unaofaa kulingana na matumizi.'*

Katika kesi hiyo hiyo ya ICC, Mheshimiwa Ruto (ambaye alikuwa mshukiwa wakati huo) alinukuliwa akilalamika kuwa tafsiri ya diskosi ya shahidi wa ishirini na tisa (29) haikufaa kwani wakalimani kutoka nchi ya Kongo walifanya makosa mengi katika tafsiri yao kwa sababu hawamaizi msamiati wa lugha ya Kiswahili unavyotumiwa nchini Kenya. (Gazeti la *DailyNation*, Kenya, (21-1-2015:8). Makala haya pia yalizua wazo la kuchunguza changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika kesi mbalimbali katika mahakama. Hii ni kwa sababu iwapo washtakiwa, mawakili wa walalamishi pamoja na mawakili wa washtakiwa, kule ICC, walilalamika kuwa ukalimani uliotolewa haukufaa muktadha wa matumizi nchini Kenya, inamaanisha kuwa kulikuwa na kasoro katika ukalimani katika diskosi za wahusika wa kesi. Kasoro hizo huenda zikasababisha ukosefu wa haki katika maamuzi ya hakimu.

Sura ya pili ya Katiba ya nchi ya Kenya (2010: 135-165) inadai kuwa wananchi wana haki ya kutumia lugha zao za kwanza, lugha ya taifa na rasmi (Kiswahili) au lugha rasmi katika mahakama (Kiingereza). Pia, wahusika wasioweza kutumia lugha ya Kiingereza wanapewa haki ya kuwa na mkalimani bila malipo ili kuwasaidia kukalimani ujumbe wao hadi Kiingereza na ule ujumbe uliotolewa katika Kiingereza kukalimaniwa hadi Kiswahili au lugha waliyoichagua. Iwapo Katiba inatambua kuwa kuna wananchi ambao ni wanalughamoja au hawaelewi Kiingereza, basi wakalimani nao wanafaa kuwasilisha ujumbe ule ule wa wahusika ndipo wapate haki wanayoitarajia. Pia, wakalimani wenyewe wanafaa wakalimani diskosi za wahusika wakizingatia usawa kamili wa vipengele vya lugha husika ili kufanikisha ujumbe uliokusudiwa. Utafiti huu umebaini kuwa wahusika wamepewa haki hii lakini bado kuna changamoto za ukalimani kutokana na ukosefu wa usawa wa vipengele vya lugha mbili husika.

Kutokana na misingi hii, imeonekana wazi kuwa kuna utata katika shughuli ya ukalimani na ni vigumu kufikia usawa wa vipengele vyote vya lugha katika ukalimani. Utafiti huu umechunguza changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi mbalimbali katika mahakama. Vipengele vya lugha ambavyo vimechunguzwa ni vya; ujumbe, maumbo, mtindo na toni katika MC na MP katika diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama.

### 1.2 Suala la Utafiti

Kulingana na KatibaMpya ya Kenya (2010), wahusika wa kesi katika mahakama wana haki ya kutumia lugha wanayoipendelea na kuielewa vyema. Pia, wana haki ya kupewa mkalimani ili kukalimani diskosi za wahusika wengine hadi lugha hiyo wanayoipendelea na wakati huo huo, kukalimani diskosi zao hadi lugha rasmi ya mahakama ambayo mara nyingi huwa ni Kiingereza. Ingawa katiba imeweka bayana haki hizi za kimsingi kuhusu shughuli za mahakama, changamoto zinazotokana na kukosekana kwa usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji kesi katika mahakama hazijazingatiwa. Changamoto hizi zinafaa kuzingatiwa kwa sababu wakalimani hutumika kama daraja la kuwashirikisha wahusika wote katika vikao vya uendeshaji kesi katika mahakama. Mkalimani ndiye daraja kuu la kuwashirikisha hakimu, mawakili, baraza maalumu la kumshauri hakimu, mlalamishi, mshtakiwa, mashahidi, makarani na mwendeshaji shughuli katika mahakama.Hivyo basi, iwapo mkalimani atakumbwa na changamoto zozote za usawa wa vipengele vya lugha husika, huenda ujumbe wa kisemantiki na kipragmatiki ukapotea. Ikiwa ujumbe utapotea, huenda mhusika akakosa haki au kupata hukumu ambayo si haki yake kuipata. Utafiti huu umechunguza changamoto za usawa wa vipengele vya lugha husika ambazo wakalimani hukumbana nazo wanapokalimani matini kutoka LC hadi LL. Suala kuu lilikuwa ni kuchunguza changamoto za

usawa wa vipengele vya lugha yaani ujumbe, maumbo, mtindo na toni katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi katika mahakama.

### 1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kutathmini changamoto za usawa wa vipengele vya lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi katika uendeshaji wa kesi katika mahakama.

### 1.3.2 Malengo Mahususi ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo maalumu yafuatayo:

(i) Kufafanuakipengele cha ujumbe wa kisemantiki na ujumbe wa kipragmatiki uliokusudiwa katika LC na kukalimaniwa hadi LL kutegemea wahusika na muktadha wa matini.

(ii) Kulinganisha kipengelecha miundo au maumbo ya lugha hizombili husika hasa kuhusu maumbo ya maneno, virai, vishazi na sentensi katika ukalimani wa kipengele cha maumbo ya kileksia na kisintaksia katika diskosi za wahusika katika mahakama katika LC na LL.

(iii) Kubainisha kipengele cha mtindo wa LC na LL husika, yaani jazanda, misemo, tashbihi na tasfida katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika mahakama kutoka LC hadi LL.

(iv) Kulinganisha kipengele cha toni katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi kutoka LC hadi LL.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Maswali ambayo yalitarajiwa kujibiwa kutokana na utafiti huu ni;

i) Wakalimani katika mahakama walikumbwa na changamoto zipi kuhusu usawa wa kipengele cha ujumbe kutoka MC hadi ML katika harakati ya kukalimani diskosi za wahusika wa kesi mbalimbali katika mahakama?

ii) Wakalimani katika mahakama walikumbwa na changamoto gani kuhusu usawa wa kipengele cha maumbokatika ukalimani wao wa diskosi za wahusika wa kesi mbalimbali katika mahakama kutoka LC hadi LL?

iii) Je, wakalimani waliweza kufikia usawa wa kipengele cha mtindo wa lugha mbili husika katika ukalimani wa diskosi za wahusika mbalimbali wa kesi katika mahakama kutoka LC hadi LL?

iv) Je, wakalimani katika uendeshaji kesi walifikia usawa wa kipengele cha toni katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi kutoka LC hadi LL?

**1.5 Ufaafu wa Utafiti**

Matokeo ya utafiti huu iwapo yatazingatiwa yatawafaa wahusika ambao watahitaji wakalimani ili kuwasilisha ujumbe wao katika uendeshaji wa kesi katika mahakama. Hawa ni wahusika wa kesi mbalimbali watakaowasilisha diskosi zao kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili naujumbe wa wahusika wengine kukalimaniwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.Watatarajia mkalimani kuwasilisha diskosi hizo kwa lugha inayopendelewa na mhusika huku mkalimani akizingatia usawa wa vipengele kadhaa vya lugha ili kupata usawa unaotarajiwa. Kulingana na Katiba Mpya ya Kenya (2010), wahusika wa kesi katika mahakama wana haki ya kutumia lugha wanayoipendelea na kuielewa vyema. Pia, wana haki ya kupewa wakalimani ili kukalimani diskosi za wahusika wengine hadi lugha hiyo wanayoipendelea na wakati huo huo, kukalimani diskosi zao hadi lugha rasmi ya mahakama ambayo ni Kiingereza.

Matokeo ya utafiti huu yamebainisha changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi katika shughuli za uendeshaji kesi katika mahakama.Changamoto hizo huenda zikaathiri ujumbe uliokusudiwa na kuwanyima haki wahusika hao kinyume na mapendekezo ya Katiba Mpya ya Kenya (2010). Kutokana na changamoto zinazohusu usawa wa vipengele vya lugha husika, wahusika wanaweza kudai kuwa wamenyimwa haki zao za kimsingi. Hivyo basi, ikiwa ujumbe uliokalimaniwa si sawa kwa sababu ya msuko wa maumbo au mtindo wa matini au kutokana na toni ya uwasilishaji katika diskosi zao zilizokalimaniwa, huenda ikapendekezwa wapewe nafasi zaidi ya kujitetea.Ikiwa hakimu atawapa nafasi nyingine basi watakuwa wamepata haki inavyostahili. Wahusika wa kesi watafaidika zaidi aidha kwa kufanyiwa uchunguzi zaidi au kwa kupewa nafasi ya kujieleza vyema tena ili kupata haki kulingana na Katiba Mpya ya Kenya(2010).

Pia, matokeo ya utafiti huu yatawafaa wakalimani. Hii ni kwa sababu, ikiwa wanakumbwa na changamoto za usawa wa vipengele vya lugha huenda ikalazimu serikali kuwapata mafunzo maalumu ya taaluma ya tafsiri na ukalimani katika taaluma ya kisheria ili kuwawezesha kukalimani diskosi hizo kwa ufasaha. Changamoto hizi zinazowakumba wakalimani zinatokana na hali kwamba wakalimani wanahitaji muda zaidi ili kutafuta kisawe katika LL au nafasi ya kuelewa ujumbe uliokusudiwa na mhusika. Kwa kupewa nafasi ya kusaili wahusika, wakalimani watatumika vyema kama vyombo vya kuhawilisha ujumbe uliokusudiwa baada ya kuelewa ujumbe wa diskosi za wahusika.

Mawakili na jamaa za wahusika wa kesi watafaidi kutokana na ukalimani bora ikiwa wakalimani watapata mafunzo na kutekeleza ukalimani usio na kasoro za usawa wa vipengele vya lugha husika. Wakalimani wakipokea mafunzo kuhusu taaluma ya ukalimani na tafsiri, watapata maarifa ya kubuni mbinu za kutumia katika kukalimani ujumbe ambao unakosa kisawe moja

kwa moja katika LL. Hivyo basi, ujumbe utaeleweka vyema na kila mhusika atapata haki yake kulingana na hali ya kesi husika.

**1.6 Umuhimu wa Utafiti Huu**

Matokeo ya utafiti huu ikiwa yatazingatiwa yatawafaa wahusika ambao watahitaji wakalimani ili kuwasilisha ujumbe wao mahakamani. Hawa ni wale wahusika watakaotoa ushahidi wao mahakamani kwa lugha ya Kiswahili au ujumbe wa wahusika wengine kukalimaniwa katika lugha ya Kiswahili na hivyo kutarajia mkalimani kuwasilisha diskosi hizo kwa lugha inayotarajiwa akizingatia usawa wa vipengele kadhaa vya lugha ili kupata usawa.

Utafiti huu unalenga kuimarisha haki za wahusika wa kesi mahakamani na hasa washtakiwa. Kulingana na Katiba Mpya ya Kenya (2010) wahusika wa kesi katika mahakama wana haki ya kutumia lugha wanayoipendelea na kuielewa vyema. Pia, wana haki ya kupewa mkalimani ili kukalimani diskosi za wahusika wengine hadi lugha hiyo yao waliyoipendelea na wakati uo huo, kukalimani diskosi zao hadi lugha rasmi ya mahakama ambayo ni Kiingereza. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi katika shughuli za uendeshaji kesi katika mahakama. Changamoto hizo huenda zikaathiri ujumbe na kuwanyima haki wahusika hao kinyume na mapendekezo ya Katiba Mpya ya Kenya (2010). Kutokana na changamoto za usawa wa vipengele vya lugha husika, wahusika wanaweza kudai kuwa haki haikutendeka. Hivyo basi, ikiwa ujumbe uliokalimaniwa si sawa kwa sababu ya maana ya muktadha wa matumizi, msuko wa maumbo au mtindo wa matini au kutokana na toni ya uwasilishaji katika diskosi zao zilizokalimaniwa, huenda ikapendekezwa wapewe nafasi zaidi ya kujitetea. Ikiwa hakimu atawapa wahusika hao nafasi nyingine basi watakuwa wamepokea haki inavyostahili. Wahusika wa kesi watafaidika aidha kwa kufanyiwa

uchunguzi zaidi au kwa kupewa nafasi ya kujieleza vyema ili kupata haki kulingana na Katiba Mpya ya Kenya (2010).

### 1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika mahakama ya Kericho pekee katika Mji wa Kericho wala si mahakama tamba za eneo la Kaunti ya Kericho. Mahakama hii ina aina tano za mahakama: Mahakama Kuu, Mahakama ya Hakimu Mkuu, Mahakama ya Kupambana na Ufisadi, Mahakama ya Watoto na Mahakama ya Ajira na Mahusiano ya Utendakazi. Hii ndiyo mahakama ya pekee katika Kaunti ya Kericho. Kaunti hii ina kaunti ndogo sita (Kipkelion Magharibi, Kipkelion Mashariki, Ainamoi, Soin-Sigowet, Belgut na Buret).

Muda wa miezi miwili ulitumika kukusanya data. Mtafiti alihudhuria vikao kadhaa vya uendeshaji kesi mbalimbali katika vyumba mbalimbali katika mahakama hii na kunakili na pia kunasa diskosi zilizotokea katika uendeshaji wa kesi mbalimbali katika mahakama. Uchunguzi wa diskosi za wahusika katika vikao vya kesi mbalimbali ulifanywa hasa kulikokuwa na matumizi ya wakalimani.

Mtafiti aliteua diskosi za kesi sita miongoni mwa kesi kadhaa alizozichunguza kwa kutumia sampuli nasibu horomo na sampuli makusudi. Uchunguzi wake ulijikita kwenye changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi mbalimbali katika mahakama. Mtafiti alitumia nadharia ya usawa kuchanganua data aliyokusanya. Eneo hili la Kericho lina wakazi kutoka jamii nyingi za Kenya ambao wanazungumza lugha mbalimbali ingawa wengi hutumia Kiswahili au Kiingereza kama Lingua-Franka. Hata hivyo, usawa wa vipengele vya lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili ndio ulichunguzwa wala si usawa wa vipengele vya lugha za mama.

### 1.8 Machukulio

Wahusika wa kesi katika mahakama ya Kericho walitarajiwa kuwasilisha diskosi zao katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Ilitarajiwa kuwa hata wenyeji (Wakipsigis) wangependelea kutumia ama Kiswahili au Kiingereza katika mawasilisho ya ujumbe wao katika kesi zilizowakabili. Lugha hizi mbili ndizo lugha za kitaifa na rasmi nchini Kenya. Mara nyingi, lugha hizi hutumiwa kama lingua-franka kwa ajili ya mawasiliano baina ya wanajamii wa jamii nyingi tofauti nchini.

Utafiti huu pia ulichukulia kuwa Wakenya wengi angalau wanaweza kuelewa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na kuweza kujieleza kwa lugha mojawapo kati yazo ingawa si kwa viwango sawa. Hata hivyo, ilitarajiwa kuwa wahusika wengi wangehitaji wakalimani ili kuwasilisha ujumbe wao kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kiingereza au diskosi za hakimu au mawakili kukalimaniwa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili.

Ilitarajiwa kuwa wakalimani wangekuwapo kwa ajili ya wahusika waliowahitaji bila malipoili kufanikisha haja ya wahusika hao kama ilivyobainishwa katika Katiba Mpya ya Kenya (2010). Ilitarajiwa pia kuwa ingawa wakalimani wangechukuliwa kama vyombo vya mawasiliano visivyoonekana wala kuwa na hisia, wangekalimani diskosi zilizotokea vile wangezielewa kulingana na muktadha wa matukio yaliyozingira ujumbe uliowasilishwa. Diskosi teulekuhusu matini chanzi na diskosi zilizokalimaniwa zilichanganuliwa ili kubaini changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika LC na LL.

## SURA YA PILI

## MAPITIO YAMAANDISHI KUHUSU MADA

### 2.0 Utangulizi

Sehemu hii ya utafiti huu imefafanua dhana ya ukalimani, historia fupi na aina za ukalimani pamoja na dhana,historia na maendeleo ya tafsiri. Imeweka wazi tofauti baina ya dhana ya tafsiri na ukalimani. Pia, imeeleza uhusiano uliopo baina ya ukalimani na tafsiri na utamaduni kwa vile utamaduni huathiri maumbo na mitindo ya lugha inayotumiwa na wanajamii kwa sababu lugha ni utamaduni. Jambo jingine ambalo limeelezwahapa ni nadharia iliyotumiwa katika uchanganuzi wa data zilizokusanywa ili kuonyesha vipengele vya lugha ambavyo vinasababisha utata katika kukalimani matini kutoka LC hadi LL. Isitoshe, maelezo kuhusu mapitio ya maandishi kuhusu changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika suala la ukalimani katika mahakamayametolewa ili kuonyesha tofauti baina ya uchunguzi uliofanywa awali kuhusiana na diskosi za mahakama na pengo la utafiti ambalo uchunguzi huu umejaribu kuziba.

### 2.1 Dhana ya Ukalimani

Ukalimani wa lugha hulenga kurahisisha mawasiliano ya lugha ya mdomo au lugha ya alama kati ya watumiaji wa lugha mbili tofauti.  Shughuli ya ukalimani, kwa vile inahusu lugha na lugha ni utamaduni, inasaidia kuunganisha na kujenga uhusiano mwema kati ya tamaduni mbili au zaidi kwa njia ya mazungumzo kutoka lugha moja hadi nyingine. Hii ndiyo sababu dhana ya utamaduni imefafanuliwa katika utafiti huu ili kuonyesha kuwa lugha inasheheni utamaduni.

Kutokana na fasili ya TUKI (2000) kukalimani ni kuhawilisha mawazo moja kwa moja (papo kwa papo) kutoka lugha moja ya mazungumzo kwenda lugha nyingine ya mazungumzo bila kupoteza, kupotosha au kubadili maana. Hii inamaanisha kwamba wakalimani wanafasiri

mazungumzo au maongezi kwa kubainisha na kupambanua dhana husika kwa mujibu wa muktadha uliopo bila kupoteza lengo la mzungumzaji wa LC. Hii humshurutisha mkalimani kuwa makini sana na tamaduni zinazohusiana na LC na LL husika kwa kubadili maneno ya LC na kuyaweka katika maana ya LL na kisha kubadili njia ya mazungumzo ili kuingiliana na muundo wa LL.

Encarta (2009) anaeleza kuwa ukalimani ni tafsiri ya mdomo ya kile kinachosemwa katika lugha moja kwenda lugha nyingine ili kusudi wazungumzaji wa lugha tofauti waweze kuwasiliana. Basi huu ni uhawilishaji wa ujumbe katika lugha ya alama, ishara au mazungumzo kutoka lugha moja hadi lugha nyingine. Encarta anatumia neno tafsiri katika kueleza dhana ya ukalimani. Hali hii hudhihirisha kuwa kuna tofauti finyu mno kati ya ukalimani na tafsiri.

Kwa jumla ukalimani ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo, ujumbe na maana katika lugha ya mazungumzo au lugha ya alama kutoka LC kwenda LL. Hivyo basi, kazi ya mkalimani ni kuhawilisha mawazo, maelezo na maana kutoka LC na kuyaweka mawazo, maelezo na maana yenye maana inayolingana katika LL katika wakati halisi. Kazi ya mkalimani ni kufikisha kila kipengele cha kisemantiki na kila lengo na hisia za ujumbe ambao mzungumzaji wa LC amekusudia kufikishka katika LL.

### 2.1.1 Historia Fupi na Maendeleo ya Ukalimani

Wasomi wengi wa taaluma ya tafsiri wanaamini kuwa ukalimani ni mkongwe kuliko lugha andishi. Kwa mujibu wa Steiner (1998),Ngano ya Mnara wa Babeli katika Biblia katika kitabu cha Mwanzo sura ya sita hadi tisa, kulikuwa na lugha moja pekee kwa binadamu wote ulimwenguni. Mungu alipoona ushirika wa binadamu katika ujenzi wa mnara huu ili kufikia Mungu mbinguni, hakupendezwa kuwa binadamu wangekuwa na uwezo na nguvu nyingi jinsi

hiyo kwa sababu ya kuwa na lugha moja ya mawasiliano. Ngano hii inaeleza kuwa Mungu alituma nguvu ya kuwafanya binadamu kuwa na lugha nyingi ili wajenzi wakose kuelewana na hivyo wakose kukamilisha mnara huo. Inaaminiwa kuwa hapo ndipo binadamu walianza kuwa na haja ya ukalimani ili kuweza kuwasiliana kwa sababu walikuwa na lugha nyingi.

Kwa mujibu wa Fawcett (2003) ukalimani umekuwapo tangu binadamu walipoanza kuwasiliana kwa kutumia maneno katika mazungumzo. Ukalimani umekuwa ukitumika kujenga mahusiano baina ya watu kutoka jamii mbalimbali tangu kuwepo binadamu ulimwenguni. Hata hivyo, hakuna rekodi au ushahidi wowote kuwa ukalimani ulikuwapo kwa sababu hauachi alama yoyote kwa sababu ukalimani haukuwa na maandishi. Maandishi ya kwanza kuhusu ukalimani yalitokea mwaka wa 3000KK wakati Wamisri wa Kale walikuwa na hieroglifu iliyoashiria 'mkalimani'. Pia, ukalimani ulifanywa Uyunani na Ugiriki enzi za ukoloni wao walipolazimisha watawalwa wao (watumwa, wafungwa na kundi la machotara) kujifunza lugha yao na lugha nyinginezo ili kutumiwa kukalimani. Wakati huu wote hadi karne ya 17, Kilatini kilitumiwa miongoni mwa jamiilugha mbalimbali kama lingua-franka na lugha ya kidiplomasia Uropa na mataifa yote ili kuendeleza mahusiano ya kimataifa.

Ukalimani ulienea karne ya 7BK na 8BK kwa sababu ya vipengele kadha ikiwemo dini iliyoenezwa na waumini waliosafiri kwenda mataifa mbalimbali ili kueneza na kushirikisha imani zao. Kwa mfano, karne ya 7BK na 8BK, Waarabu walienda Afrika Magharibi kueneza dini ya Kiislamu na kufanya biashara ambapo lugha ya Kiarabu (lugha ya Kurani) ilitumiwa. Pia, mwaka wa 1253, dini ya Kikristo ilienezwa na William wa Rubruck na wakalimani waliotumwa na Louis IX kule Asia. Enzi za utalii wa ugunduzi wa bara mpya karne ya 16, ni kipengele kingine kilichoeneza ukalimani. Wakati huu, Dona Marina (La Malinche) kutoka Mexico

alikuwa mkalimani wa Corte. Hata hivyo, mara nyingi wakalimani walikuwa wenyeji ambao wengine waliwaona kama wasaliti wao kwa wageni. Ingawa waliitwa wasaliti, kazi yao ya ukalimani ilizaa matunda wakati ilisababisha kuwepo kwa mikataba na maafikiano yaliyotumika katika ugawanyaji wa ulimwengu kuwa ulivyo leo.

Mwaka wa 1924, katika karne ya 20, katika Mkutano wa Kimataifa wa Wafanyakazi kule Geneva, Uswizi, ukalimani sawia ulitumiwa kwa mara ya kwanza. Aina hii ya ukalimani haikutumiwa wakati wa Vita vya Pili vya Dunia kwa sababu ilionekana kuwa ghali mno na yenye utata mwingi. Mbinu hii ilianza kutumika mno mwaka wa 1945 kule Nuremberg katika uendeshaji wa kesi za jinai kuhusu wahalifu katika hivyo Vita vya Pili vya Dunia. Tangu hapo, ikawa sasa ukalimani sawia unatumiwa katika makongamano, mikutano na uendeshaji wa kesi za kimataifa. Kesi za Nerumberg zilipokamilika 1947, Azimio la Muungano wa Kimataifa 152, likaweka misingi imara kudumisha matumizi ya ukalimani sawia katika makongamano ya Muungano wa Kimataifa.

Msamiati 'Ukalimani wa Kijamii' ulizuka mwaka wa 1970 kule Australia na kuenea haraka hadi Uropa na Marekani. Msamiati huu una maana ya kuwepo kwa ukalimani katika asasi zote za kijamii na kiserikali ili kuwakalimania wafanyakazi na watu binafsi matini kutoka LC hadi LL wanayoielewa. Hata hivyo ukalimani wa kijamii unaonekana kuwepo tangu mwanzo wa ukalimani, yaani tangu binadamu alipoanza kuwasilisha ujumbe kwa mazungumzo kwa wanajamii wa lugha tofauti na yake. Kule Sweden, maendeleo na ukuaji wa ukalimani wa kijamii ulisababishwa na uhamihaji wa waathiriwa wa Vita vya Pili vya Dunia (1939-1945). Kule Australia, Ukalimani wa Kijamii ulitumiwa hadi wahamiaji wengi walipoingia na kusababisha uwingilugha ili kuwaridhia Waustralia wa Kigeni. Ukalimani wa kijamii ulikuwa

unafanywa na watu wasio na ujuzi hadi mwaka wa 1773 wakati wakalimani wa mazungumzo ya simu walipohitajika ndipo kulihitajika shule na vyuo vya ufundishaji wa taaluma ya ukalimani.

Mwaka wa 1978 Mahakama ya Marekani ilipitisha sera ya ukalimani ambayo ilisaidia katika uwepo wa ukalimani wa kulipwa katika mahakama na wakalimani wakahitajika kusomea taaluma ya ukalimani katika vyuo vikuu na taasisi nyingine zinazotoa mafunzo ya taaluma hiyo. Tangu miaka ya 1970 kumekuwa na mahitaji ya wakalimani wa ukalimani wa kijamii hivi kwamba kumezuka uwepo kamili wa mtaala na vyeti vinavyofanana katika taaluma ya ukalimani. Mwaka wa 1995, Mkutano wa Kimataifa wa Wakalimani wa Kijamii ulifanyika *GenievaPark* karibu na mji wa Toronto. Mwaka wa 1997, NAATI (*NationalAccreditationAuthorityforTranslatorsandInterpretersLtd*) ilianzishwa kule Australia ili kutunga na kuhifadhi hadhi bora za kitaifa katika taaluma za tafsiri na ukalimani.

Kule Sweden, ukalimani wa kijamii katika mahakama ni haki ya wahamiaji kwa mujibu wa kanuni za kimahakama katika uendeshaji kesi. Kanuni hii imekuwapo Sweden tangu mwaka wa 1968 na lugha 103 zimekuwa zikitumika katika mafunzo ya wakalimani. Taifa la Sweden pia limeweka kanuni za wakalimani waliohitimu na kukubalika ambapo utahini unafanywa na shirika la NALF (*NationalAgencyforLandsandFunds*). Nchini Kenya, katiba ya Kenya ya mwaka 2010 inapendekeza kuwa kila Mkenya ana haki ya kupewa mkalimani, bila malipo, katika mahakama iwapo haelewi lugha rasmi ya mahakama ambayo ni Kiingereza. Ukalimani wa kijamii una uwezo wa kukua katika ulimwengu wa sasa ambapo mataifa, miji mikuu na miji midogo midogo inazidi kuwa na wakaazi wenye uwingilugha. Chanzo cha tafsiri nchini Kenya ni uwepo wa jamiilugha nyingi na ukosefu wa umilisi wa lugha ya kitaifa na rasmi (Kiswahili) na lugha rasmi ya mahakama na taaluma ya kisheria (Kiingereza).Nchini Kenya, kuna jamiilugha

zaidi ya arobaini. Kila mara, wanajamii wasioelewa lugha ya Kiingereza na Kiswahili huhitaji wakalimani ili kuwasilisha ujumbe wao kwa wengine.

### 2.1.2 Umuhimu wa Ukalimani

Kulingana na Mwansoko na wenzake (2006), ukalimani hutumiwa kurahisisha mawasiliano miongoni mwa jamii mbili au zaidi zenye lugha na tamaduni tofauti. Ukalimani ni daraja linalosaidia kuunganisha watu au jamii mbili zinazozungumza lugha mbili tofauti. Kwa mfano, ukalimani hurahisisha mawasiliano katika makongamano ya kimataifa kuhusu maendeleo ya jamii katika taaluma za siasa, uchumi na utamaduni.Hivyo basi, ukalimani husaidia kufanikisha vikao, makongamano na mikutano ya kitaifa na kimataifa.

Pia, ukalimani husaidia kudumisha amani ya kisiasa na kisheria duniani. Hii ni kwa sababu watu waliofarakana huweza kukaa pamoja na kuzungumza chini ya wasuluhishi wa kimataifa kama vile Muungano wa Mataifa ya Afrika (AU), Muungano wa Kimataifa (UN) na Muungano wa Mahakama ya Kimataifa (ICC).

Zaidi ya hayo, ukalimani hutumika kudumisha imani za kidini za wanajamii duniani. Kwa mfano, wahubiri wengi wa kimataifa hupeleka ujumbe kuhusu Mungu sehemu mbalimbali za ulimwengu zenye lugha tofauti kwa kutumia wakalimani.

Isitoshe, ukalimani ni nyenzo muhimu ya kujifunzia lugha ya pili. Kwa mfano, mtu anayejifunza lugha ya Kiswahili anaweza kufanya hivyo kwa kutumia mkalimani kupitia lugha ya Kiingereza au lugha yoyote ile anayoijua.

Juu ya hayo, ukalimani husaidia lugha kuwa hai kulingana na wakati katika kuakisi mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni yaliyojitokeza katika jamii husika.  Kwa mfano, watu

maskini siku hizi huitwa walalahoi na matajiri huitwa walalahai au walalaheri katika uwanja wa kisiasa na kiuchumi nchini Kenya.

Mwisho, ukalimani huwasaidia hadhira lengwa kujifunza mawasiliano ya ishara na alamakama mkalimani anatumia njia hizo katika mawasilisho yake. Hii ni kwa sababu, mkalimani hukalimani matini katika LL kwa kuzingatia maneno dhahiri na ishara zilizotumiwa na mzungumzaji wa LC.

Hata hivyo, kuna umuhimu zaidi wa ukalimani unaojitokeza mbali na uhawilishaji wa ujumbe husika katika matini mahususi inayohawilishwa kutoka LC hadi LL. Hayo ni pamoja na ukalimani kutumika kueneza utamaduni wa jamii ya MC kwa jamii ya ML, kutumika katika kampuni za simu kuwasiliana na wateja wake kwa kutumia lugha ambayo wateja hao wanaielewa na vilevile kusaidia katika masuala ya kidiplomasia na uhusiano wa kimataifa hasa katika kusuluhisha migogoro iliyopo au kuendeleza urafiki baina ya jamii za kimataifa.

### 2.1.3 Aina za Ukalimani

Kuna aina mbalimbali za ukalimani kutegemea vigezo mbalimbali vya jinsi ukalimani unavyotumiwa kuhawilisha diskosi kutoka LC hadi LL. Kwa mujibu wa *NajitPositionPaper* (2006) kuna aina nne za ukalimani (ukalimani mfululizo, fuatilizi, muono na muhtasari) lakini Crystal (1997) anatambua aina mbili kuu za ukalimani: ukalimani mfululizo na ukalimani fuatilizi. Yafuatayo ni maelezo kuhusu aina hizo mbili za ukalimani zilizotambuliwa na crystal na *Najit*nambili Zaidi zilizotambuliwa na Najit. Kwa jumla kuna aina nne za ukalimani zilizoelezwa kama ifuatavyo;

#### 2.1.3.1Ukalimani Mfululizo

Katika ukalimani huu, mzungumzaji wa LC na mkalimani wa LL huanza kuzungumza pamoja na kumaliza pamoja uwasilishaji wa ujumbe kwa wasikilizaji. Hata hivyo, mzungumzaji katika LC huenda akaanza sekunde chache kabla ya mkalimani na katika kumaliza huenda mkalimani akamaliza sekunde mbili hadi kumi baada ya mzungumzaji wa LC. Mara nyingi, vifaa maalumu hutumika. Mkalimani hukaa katika chumba chenye kudhibiti sauti akizungumza kupitia kipaza-sauti wakati huo huo akisikiliza na kumwona barabara mzungumzaji wa LC kupitia visikizi. Aina hii ya ukalimani ilitumiwa mno na wakalimani wa lugha ya alama na ishara. Siku za hivi karibuni, ukalimani mfululizo umekuwa ukitumika katika uhawilishaji wa ujumbe wa lugha ya kusemwa. Ukalimani huu pia huitwa ukalimani sawia, ukalimani sambamba au ukalimani andamizi. Kwa mujibu wa Najit (2006) na Crystal (1997) aina hii ya ukalimani ina manufaa na udhaifu wake.

Manufaa ya ukalimani mfululizo ni kuwa huchukua muda mfupi kuhawilisha ujumbe kwa wasikilizaji wote kwani mkalimani huzungumza sawia na mzungumzaji wa matini inayokalimaniwa kutoka LC hadi LL.

Hata hivyo ukalimanimfululizo una udhaifu wake. Udhaifu wake ni kuwa ni ghali mno kwa sababu wakalimani wengi huhitajika na vifaa vya kusikilizia vinagharimu kiasi kikubwa cha fedha. Pia, wakalimani huhitaji chumba maalumu ambamo wanafanyia ukalimani wao huku wakiangalia mzungumzaji kupitia kifaa maalumu. Isitoshe, wakalimani hawana muda wa kufikiria kuhusu msamiati bora katika muktadha kwa sababu wanasikiliza huku wakikalimani. Hata hivyo, wakalimani wanafaa kuwa na umilisi walugha mbili na sajili husika ili kukalimani matini husika bila kukumbwa na changamoto tele. Mara kwa mara, wakalimani hupitwa na baadhi ya ujumbe uliosemwa katika LC kwa sababu ya kukosa muda wa kukalimani. Baadhi ya

wakati mzungumzaji huenda akazungumza kwa kasi hivi kwamba mkalimani hawezi kufikia kasi hiyo. Zaidi ya hayo, mkalimani hukumbwa na tatizo la mpangilio wa maneno katika sintaksia ya LL hususani katika sentensi changamano au katika sentensi ambazo mzungumzaji katika LC anabadilisha muundo wake anapoendelea kuzungumza.

**2.1.3.2Ukalimani Fuatizi**

Crystal (1997) na Najit (2006) wanaeleza kuwa katika ukalimani huu, mkalimani huzungumza baada ya mzungumzaji wa LC kumaliza kuzungumza. Mkalimani na mzungumzaji wa matini asilia huzungumza kwa zamu. Mkalimani huwa ameketi au kusimama karibu na mzungumzaji wa LC akisikiliza au hata kuandika anayozungumza mzungumzaji wa LC ili kumsaidia kukumbuka wakati ataanza kukalimani. Wakati mzungumzaji wa LC anamaliza kuzungumza au anapopumzika, mkalimani anahawilisha kipande cha ujumbe au ujumbe mzima wa mzungumzaji katika LL.

Ukalimani huu unafanywa katika mikutano ya kimataifa, mahakamani katika mabaraza ya kutolea hukumu, kituo cha polisi hususani wakati wa kuchukua maelezo ya mlalamishi na mshtakiwa, ukumbi wa mikutano ya maapisho, kiungani katika shughuli za utalii, katika vyombo vya habari kama vile redioni au runingani, mawasiliano ya simu, katika video, maabadani au katika jeshi la kimataifa. Pia, huitwa ukalimani fuatishi, fuatilizi au ukalimani mtawalia.

KwamujibuwaCrystal (1997) aina hii ya ukalimani humpa mkalimani nafasi ya kufikiria ili kupata msamiati mwafaka katika LL. Mara nyingi mkalimani huwa na nafasi ya kuandika matini ya mzungumzaji na kuitafutia kisawe chake katika LL kabla ya kuzungumza. Pia, mkalimani ana nafasi ya kutumia mpangilio wa kisintaksia unaofaa katika LL kwa sababu anasikiliza kwanza na kupata ujumbe mzima ndipo anapokalimani ujumbe huo. Mbali na hayo, ukalimani huu

haugharimu kiasi kikubwa cha fedha kwa sababu vifaa na vyumba vya wakalimani havihitajiki kwani mkalimani hukaa karibu na mzungumzaji na kumwangalia na kumsikiliza anapozungumza.

Hata hivyo, ukalimani huu huchukua muda mrefu kwani mkalimani hungoja mpaka mzungumzaji wa LC akamilishe kipande cha ujumbe au ujumbe mzima ndipo aukalimani na wakati huo mzungumzaji naye anamngoja mkalimani kukamilisha kukalimani ndipo aendelee na maelezo ya matini yake. Mkalimani anafaa kuandika ujumbe huo katika LC na hata kuukalimani katika LL kabla ya kuanza kuuwasilisha ujumbe wenyewe. Mkalimani anafaa kusikiliza huku akiandika matini hiyo katika LC au LL. Kwa sababu ya urefu wa ujumbe, mkalimani huenda akasahau baadhi ya ujumbe uliosemwa kama hakupata nafasi ya kunakili kwanza ndipo aanze kukalimani. Ukalimani huu ni karibu sawa na ukalimani muhtasari.

**2.1.3.3 Ukalimani Muono**

Katika Najit (2006) ukalimani muono au kuona ni uhawilishaji wa ujumbe kutoka matini andishi ya LC hadi matini ya kuzungumza katika LL. Huu ni ukalimani sawa na mahususi wa matini andishi kwa njia ya mdomo katika LL ili kuwezesha wahusika kuelewa ujumbe uliopo katika matini andishi. Aina hii ya ukalimani hutumiwa mahakamani wakati wahusika wa kesi wanakabidhiwa fomu zilizoandikwa katika lugha ya Kiingereza au lugha ngeni kwao na wanahitaji kufahamishwa ujumbe uliomo. Pia, aina hii ya ukalimani hutumiwa katika mahakamakuhusiana na hati na barua za kibinafsi zilizoandikwa kwa lugha ya kigeni zinapotolewa kama kipande cha ushahidi katika kesi. Ukalimani huu huhitaji muda mrefu ili mkalimani kuisoma matini kabla ya kukalimani yaliyomo kwa mdomo au mazungumzo.

Mkalimani basi anastahili kupewa matini husika mapema ili kutumia vifaa vya tafsiri kama kamusi kabla ya kesi kuendeshwa mahakamani.

#### 2.1.3.4 Ukalimani Muhtasari

Huu ni ukalimani ambapo mkalimani hutoa ujumbe uliosemwa kwa muhtasari bila kuzingatia kila kipengele cha ujumbe huo. Aina hii ya ukalimani haifai kabisa katika mahakama kwa sababu kila kipengele cha ujumbe huwa muhimu katika uendeshaji wa kesi na huchangia katika maamuzi ya kesi husika. Katika taaluma ya kisheria hakuna ujumbe unaodunishwa hasa iwapo ni ushahidi katika kesi. Kila kipande cha ujumbe humsaidia hakimu kutoa maamuzi faafu kuhusu kesi husika.

Katika utafiti huu, ukalimani mwafaka uliotumiwa ni ukalimani fuatizi kwa sababu kiongozi wa mashtaka alitangulia kuzungumza kisha kumpa mkalimani nafasi ya kukalimani matini husika. Kiongozi wa mashtaka alizungumza polepole na kumpa mkalimani nafasi ya kukalimani kipande cha ujumbe wa matini husika kabla ya kuendelea. Mkalimani na kiongozi wa mahakama walizungumza kwa zamu.

### 2.1.4 Stadi Muhimu Kuhusu Mkalimani na Mfasiri Bora

Bassnett (2002) akimnukuu Levyanadai kuwa kuhulutisha maumbo ya matini au kudondosha maumbo mengine yanayotatiza katika tafsiri ni mwiko au kitendo kisichokubalika katika taaluma ya tafsiri. Mtafsiri ana jukumu la kutafuta suluhu kwa vipengele vinavyotatiza na sharti azingatie ujumbe, muundo, mtindo na toni ya LC katika LL. Hivyo basi, mkalimani au mtafsiri bora sharti;
(i) Aelewe ujumbe wa mwandishi wa MC ili kuutafsiri katika LL. Kwa hivyo, anafaa awe na stadi ya kudondoa na kuandika muhtasari wa ujumbe muhimu pekee kati ya mengi yanayozungumzwa na mzungumzaji.

(ii) Awe na umilisi wa LC na LL ili aweze kutafsiri ujumbe uliokusudiwa kwa ufasaha.Mkalimani anafaa kumudu stadi za lugha za mawasiliano (LC na LL) ili kuwasilisha ujumbe kwa njia mwafaka.

(iii) Awe anafahamu utamaduni wa LC na LL ili kuelewa namna ya kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa katika LC kwa namna inayofaa katika LL ili asiwaudhi wala kuwatusi au kuwaaibisha wanajamiilugha husika.

(iv) Azingatie muktadha na wahusika wa MC na ML. Hapa muktadha wa tukio na sajili ya mawasilisho ni muhimu ili kufanikisha ujumbe husika katika LL.

(v) Asitumie mtindo wa neno kwa neno katika tafsiri. Badala yake atumie mbinu sisisi inapofaa, mbinu ya kisemantiki na ya kipragmatiki ili kuuwasilisha ujumbe uliokusudiwa.

(vi) Ateue msamiati unaofaa na apange maneno yake vyema katika LL ili kuzua toni iliyokusudiwa katika LL.

(vii) Azingatie LL na LC inavyotumiwa katika mazungumzo na mawasiliano ya kila siku ya wahusika au wasikilizaji.

(viii) Mkalimani anafaa kuwa na stadi ya kusikiliza kwa makini ili kupata ujumbe na kukuza stadi ya kumbukumbu ili aweze kukalimani yaliyosemwa na mzungumzaji wa LC kwa ukamilifu katika LL.

(ix) Mkalimani anafaa awe na sanaa ya kuzungumza hadharani, kuandaa hotuba, kuanza kwa kishindo, kumaliza kwa kishindo, kutoa mifano dhahiri na kuepuka tabia mbaya mbele ya watu kama vile kuingisha kidole puani, kushika sehemu za siri mwilini.

(x) Mkalimani ahakikishe amevaa vizuri ili asije akazua hisia za matamanio na kufanya wahusika kukosa kusikiliza ayasemayo.

Bassnett (2002)akiwanukuu Sapir na Whorf anaeleza kuwa mkalimani na mtafsiri anastahili kuwa na sifa hizo kwa sababu hakuna lugha mbili zinazolandana kimaana, kimuundo, kimtindo wala kitoni na kuwa na muonoulimwengu sawa. Ulimwengu wa jamii mbalimbali ni tofauti kwa vile lugha si manenopekee kutokana na lugha za jamii hizo. Lugha huzaa jamii na jamii huzaa lugha na hakuna lugha ambayo inaweza kudumu bila utamaduni na utamaduni hauwezi kudumu bila lugha yenye muundo wa kimsingi.

**2.1.5 Dhana ya Tafsiri**

Mwansoko (1996) sawa na Mshindo (2010) wanaeleza kuwa tafsiri ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine. Mawazo kati ya LC na LL sharti yawiane ingawa haiwezekani mawazo ya matini hizo mbili kulandana kabisa katika vipengele vyote vya lugha husika. Inaonekana kuwa ni vigumu kwa mkalimani kulandanisha maumbo na vipengele vyote vya lugha kutoka MC na ML.

Kwa mujibu wa Betlem (2013) na Nida (1969, 1982) tafsiri hujumuisha na kuzalisha upya ujumbe wa LC kwa kutumia visawe vya LL vinavyokaribiana zaidi na LC kimaana na kimtindo. Hata hivyo, kauli hii ina utata mwingi ambao unafaa kujadiliwa. Ujumbe hapa ni kwamba visawe ambavyo vitapatikana havitatosheleza kila kipengele cha lugha lakini vinakaribiana kimaana, kimtindo na kimaumbo.

Larson (1984) sawa na As-Safi (2007) akimnukuu Dubois (1974) wanaeleza kuwa tafsiri ni uhawilishaji wa maana iliyoko katika maandishi katika LC kwenda katika LL. Larson hakueleza ni vipi ujumbe huo utahawilishwa kutoka LC hadi LL ili kufikia usawa ambao unahitajika. Uhawilishaji wa ujumbe unamhitaji mkalimani kuzingatia maumbo, mtindo, toni, muktadha wa matumizi na hata utamaduni wa LC na LL. Katika kuzingatia hayo, mkalimani hukumbana na

changamoto tele kwa sababu hakuna lugha mbili ambazo zina maumbo, mtindo, toni na utamaduni sawa.

Snell-Hornby (1988) anafafanua dhana ya tafsiri kuwa shughuli kati ya mwandishi, mtafsiri na msomaji wa matini husika. Anasema kuwa tafsiri ni shughuli yenye utata katika tendo la kuwasiliana ambapo mwandishi katika LC, mtafsiri kama mwandishi katika LL na msomaji wa matini katika LL hutangamana. Anaeleza kwamba mwandishi wa MC huandika matini yake kulingana na mazingira yake na namna anavyotumia lugha kutokana na mtazamo-ulimwengu wake. Kwa hivyo, mfumo wa mtafsiri-msomaji wa matini chanzi husika unafaa kutegemea ujuzi na umilisi wake wa matini hiyo na muktadha wa matini yenyewe.Ikiwa mkalimani hana ujuzi na umilisi wa lugha mbili husika, atakumbwa na changamoto zipi za vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi husika?

Zabalbeascoa (1996) anadai kuwa tafsiri ni tendo la mawasiliano au mfanyiko wa kibinadamu na jamii ambao si kamilifu. Kwa hivyo, tafsiri ni tendo lenye dosari. Ikiwa tafsiri ni mfanyiko wenye dosari, basi inamaanisha kuwa itakuwa ni jambo la kawaida kuwepo kwa dosari katika ukalimani wowote ule. Ikiwa makosa hutokea, inamaanisha kuwa ujumbe kamili hautatekelezwa na hivyo kusababisha ukosefu wa haki hasa katika mawasiliano ya uendeshaji kesi katika mahakama. Basi, baadhi ya wahusika huenda wakanyimwa haki zao. Je, ni changamoto zipi za vipengele vya lugha zinazosababisha dosari hizo?

Carbonell (2006) anaeleza kuwa tafsiri ni mfumo wa mawasiliano na nia ya kufanikisha mawasiliano hayo. Hata hivyo, katika tafsiri, mfanyiko wa mawasiliano uhawilishwa katika muktadha mwingine ambapo wahusika ni tofauti kwa ajili ya malengo tofauti na ya muktadha wa kwanza. Uhawilishaji wa matini ni tofauti baina ya watafsiri wawili, kwa hivyo, kufanya tendo la

mawasiliano kuchukua mikondo tofauti kwa sababu ya walengwa wa ujumbe husika. Hii inamaanisha kuwa katika uhawilishaji wa ujumbe, wahusika huenda kila mmoja akauelewa kivyake ujumbe ule ule mmoja tofauti na mwingine. Ikiwa ujumbe utaeleweka visivyo na mkalimani basi wahusika watakoseshwa haki zao. Wakalimani katika mahakama inabidi wawe na umilisi mkubwa katika lugha mbili ambazo wanazitumia katika shughuli zao.

Kwa jumla, tafsiri ni mchakato unaohusisha matini katika lugha chanzi na uhawilishwaji wa matini hiyo na mkalimani katika LL huku mkalimani akizingatia walengwa wa matini hiyo katika LL.

#### 2.1.5.1Historia Fupi na Maendeleo ya Tafsiri

Kulingana na Wanjala (2011) historia ni taarifa, maelezo na uchambuzi wa matukio, watu na nyakati teule zinazoathiri maisha ya wanajamii husika, sasa na hata siku za usoni. Matukio hayo huteuliwa sawia na waasisi au wataalamu wa asasi hizo. Ujuzi wa historia hutuwezesha kudhibiti na kuthamini misingi na maendeleo ya taaluma zetu. Ujuzi huo ukirejelewa, unaweza kusaidia kubashiri mienendo ya siku za usoni.

Kwa mujibu wa Ghanooni (2012) kuna nadharia nyingi na wahusika wengi wanaohusishwa na historia ya tafsiri. Ghanooni (2012) anadai kuwa waasisi wa taaluma ya tafsiri ni Horace na Cicero katika karne ya 1BC. Waasisi hawa walipendekeza kuwa tafsiri ifuate mbinu ya neno kwa neno na mbinu sisisi katika kuhawilisha ujumbe kutoka LC hadi LL.

Historia ya tafsiri imechunguzwa kwa kutegemea vipindi muhimu vya maendeleo na mabadiliko ya elimu na utamaduni wa binadamu. Vipindi vilivyo dhahiri kuhusiana na historia ya tafsiri na ukalimani ni enzi ya kale, enzi ya giza, enzi ya ufufuo, enzi ya kati na enzi ya sasa.

### 2.1.5.2 Enzi ya Kale

Kwa mujibu wa Mwansoko (1996) zama hii hujumuisha kipindi chote cha kihistoria kabla ya mwaka 300BK kuanzia mnamo mwaka wa 3000KK. Kulingana na historia chimbo, mwaka wa 300BK ndiyo tarehe ya tafsiri ya kwanza iliyovumbuliwa katika enzi ya kale ya Wamisri ikilinganisha hati za lugha mbili. Tukio hili lilionyesha kuwa chanzo cha tafsiri ni kuwepo kwa lugha nyingi.

Nida (1969, 1998) anakisia kuwa taaluma ya tafsiri ilianza 4BC St. JeromealipotafsiriBiblia ya Septugint (*Septuagate au Septuagint*) ambapo Agano la Kale lilitafsiriwa kutoka lugha ya Kibraenia au Kilatini hadi lugha ya Kigiriki. Munday (2001) anadai kuwa tafsiri hii ya Biblia ilitumia mbinu ya kipragmatiki kwa sababu ya tofauti ya kisintaksia kati ya lugha ya Kilatini na lugha ya Kigiriki. Inaaminiwa kuwa watafsiri sabini na wawili walifanikisha kazi hii na hivyo kuwa msingi wa taaluma hii ya tafsiri. Nida (1998) anabainisha kuwa tafsiri ni sayansi au nadharia ambayo ilipuziliwa mbali na kutoshughulikiwa katika karne ya pili baada ya Kristo.

Douglas (1997, 2002) anadai kuwa tafsiri ilianza zama za kale ikitumia mbinu ya neno kwa neno na mbinu ya tafsiri sisisi ambayo ilitumiwa kwa mara ya kwanza na Tullius Cicero (106-43 KK) katika makala yake ya *TheBestKindofOrator* (*DeOptimoGenereOratorum*), mwaka wa 46KK na kutafsiriwa na Hubell. Wakati huu, Cicero alibainisha kuwa mtafsiri asitafsiri makala akitumia mbinu ya neno kwa neno (verbum pro verbo) bali atumie mbinu sisisi. Wazo hili lilizua mjadala mrefu ambao umekita mizizi kwa karne nyingi. Newmark (1998b) katika karne ya ishirini alidai kuwa changamoto kubwa ya tafsiri ni ikiwa mtafsiri atumie mtindo wa neno kwa neno au mtindo sisisi katika kutafsiri matini kutoka LC hadi LL.

Kwa mujjibu wa Fawcett (2003), tafsiri ilikuja kuwa shughuli muhimu Barani Uropa Magharibi kuanzia mwaka wa 300BK. Wakati huo Warumi waliwatawala Wagiriki na kuiga utamaduni na elimu ya sayansi, falsafa na dini ya Kigiriki. Hapo ndipo tafsiri nyingi za elimu ya Kigiriki zilifanywa katika Kilatini. Kilatini kilikuwa lugha rasmi ya himaya ya Warumi katika shughuli zote za maisha. Kilatini kiliendelea kuwa lugha rasmi, lugha ya elimu, lugha ya biashara, lugha ya siasa na lugha ya diplomasia, hata baada ya kuporomoka kwa himaya ya Warumi. Lugha ya Kilatini ilitumiwa kuhifadhi utamaduni na elimu ya kimagharibi wakati wa zama za giza.

**2.1.5.3 Enzi ya Giza**

Hiki ni kipindi cha historia ya elimu ya kimagharibi kilichotokea karne ya 5 hadi 11 hivi. Kufuatia kuporomoka kwa himaya ya Warumi mwaka wa 500BK, shughuli za elimu huko Uropa zilikwama, misingi ya utamaduni kuzorota na uozo wa kijamii kukithiri. Kulitokea ukame wa maadili, maendeleo ya elimu na utamaduni kwa jumla.

Hata hivyo, katika karne ya 6, mwaka wa 570BK, Waarabu Waislamu walieneza himaya na utamaduni wa Kiislamu na maarifa na ujuzi wa sayansi walipokuja kuwatawala Wagiriki na mataifa mengine ya Mashariki ya Kati. Mnamo K7 na K8, maarifa haya yalitafsiriwa kwa lugha ya Kiarabu na kuenezwa kote kwenye himaya ya Waarabu. Utawala wa Waarabu ulipoporomoka, Wahispaniola walizindua chuo cha tafsiri cha Toledo huko Uhispaniola, ambako walitafsiri maarifa mengi ya elimu na utamaduni wa Kiarabu kwa Kihispaniola hadi K10 wakati wa enzi ya ufufuko wa elimu na utamaduni wa Kilatini.

**2.1.5.4Enzi yaUfufuko**

Enzi hii ilikita mizizi kati ya karne ya 10 na karne ya 12 ambapo kulikuwa na hamu na juhudi kuu za kufufua shughuli za elimu na utamaduni baada ya zama za giza barani Uropa Magharibi.

Ufufuo huu ulianzia Uropa Kusini hasa Italia na kusambaa kaskazini kupitia Ufaransa na Ujerumani.

Karne ya kumi na mbili imenasibishwa na 'Vita vya Msalaba' yaani vita vya kidini baina ya Wakristo (Wazungu) na Waislamu (Waarabu). Wazungu walipofika Uarabuni, walipata maendeleo makubwa ya kisayansi ambayo yalikuwa yamehifadhiwa kimaandishi katika Kiarabu. Wasomi hao wa Kizungu walipata shauku kuu ya elimu hii ya Kiarabu na hivyo walivipeleka kwao vitabu vingi vya Kiarabu kwa minajili ya kuvitafsiri kwa Kifaransa, Kijerumani na Kiingereza. Tafsiri hizo zilisababisha msisimko mkubwa wa shughuli za elimu, maarifa na utamaduni unaorejelewa kama ufufuo au ufufuko (*'renaissance'*).

**2.1.5.5 Enzi ya Kati**

Hiki ni kipindi cha kihistoria cha kati ya karne ya kumi na sita (K16) hadi kumi na tisa (K19) ambapo mwamko wa kidini ulisambaa kuanzia Ujerumani hadi kote Barani Uropa na mabara mengine. Mwamko huu ulipinga mwelekeo, falsafa na mafunzo ya Kanisa Katoliki ya wakati huo pamoja na matumizi ya lugha ya Kilatini ambayo ilikuwa lugha ya Biblia, maandishi rasmi ya kanisa na ibada kama vile misa, mawasiliano na mafunzo yote ya kidini.

Hali hii ilisababisha mgawanyiko wa dini ya Kikristo, ambapo upande mmoja ulibaki Katoliki na mwingine ukafarakana na kuendelea kufarakana zaidi na kuunda madhehebu mbalimbali. Watu mbalimbali walitafsiri maandiko matakatifu katika lugha mbalimbali ili kuwafaa wafuasi wao. Kwa mfano, mnamo mwaka wa 1522BK, Mjerumani, Martin Luther, alimaliza na kutangaza tafsiri ya Biblia kwa lugha ya Kijerumani, hivyo kuashiria mwanzo wa tafsiri za Biblia kutoka lugha ya Kilatini hadi lugha nyinginezo za Uropa. Biblia ilitafsiriwa na wamishenari kwa lugha

ya Kiingereza mwaka wa 1611BK na baadaye kwa lugha nyinginezo za ulimwengu wamishenari hao walipovamia mabara yote ulimwenguni ili kueneza injili.

Tafsiri za Biblia zilisisimua na kuchochea utekelezi wa tafsiri za fasihi Barani Uropa. Tafsiri za fasihi ya mitazamo ya urasimi na ulimbwende wa Kifaransa na taratibu za mawasiliano zilikuwa zimeimarika hata kabla ya kutokea mwandishi mashuhuri Shakespeare.

#### 2.1.5.6 Enzi ya Sasa

Kipindi hiki kilianza kujitokeza mnamo karne ya kumi na tisa (K19) kutokana na masafa marefu ya mawasiliano, maendeleo makubwa ya elimu na teknolojia na harakati makusudi za ujenzi wa jamii ya kimataifa. Wanaisimu wananasibisha kipindi hiki cha kisasa na zama za tafsiri na isimu kwani hadi karne hii ya 19, kazi ya tafsiri ilikuwa imetengewa wasomi na viongozi wa dini. Kufikia karne ya ishirini (K20), tafsiri ilipanuka kutokana na mahitaji ya mashirika ya kimataifa ili kutekeleza mawasiliano na maelewano ya jamii na mashirika ya kimataifa. Maazimio, kumbukumbu na mikakati ya mikutano ilitafsiriwa angalau kwa lugha rasmi za mataifa shirikishi.

Wakati huu ulishuhudia kuzuka kwa mataifa mapya au machanga yaliyoandamana na mikakati ya kuteua lugha rasmi, lugha za kitaifa na lugha za elimu. Uteuzi huu ulifuatwa na tafsiri za maandishi yanayofasili kongoombalimbali kama vile katiba ya nchi, sera ya elimu na sera nyingine zinazotumika katika ujenzi na maendeleo ya jamii katika asasi mbalimbali. Katika uwanja wa elimu, taaluma ya tafsiri inaendelea kwa sababu za kiisimu ambapo wataalamu wa lugha wametafsiri vitabu vya fasihi kwa minajili ya kukuza, kuendeleza na kujaliza fasihi na utamaduni wa lugha mbalimbali.

Kwa mujibu wa Mwansoko na wenzake (2013) maendeleo ya tafsiri yamesababishwa na mambo makuu matano: biashara, siasa, dini, utamaduni na elimu. Katika uwanja wa elimu, maendeleo ya kiteknolojia yanajitokeza hususan tafsiri mashine ambayo inatarajiwa kurahisisha kazi ya tafsiri katika matini elezi, fafanuzi au arifishi kutokana na wingi wa tafsiri.

Wasomi wa karne ya ishirini na ishirini na moja (K20 na K21), mbali na kuunda tafsiri mashine, wameendeleza nadharia ya tafsiri ambayo imezua taarifa na mjadala mrefu kuhusiana na uwiano wa tafsiri na misingi ya maana, mifumo ya mawazo na falsafa za maisha. Taarifa nyingi za kinatharia na kiutenda-kazi zimesambaa upesi katika mitandao ya mawasiliano.

### 2.1.6 Uhusiano Baina ya Ukalimani na Tafsiri

Ukalimani na tafsiri ni dhana zinazokaribiana kimaana. Kwa sababu hiyo, wataalamu mbalimbali wametumia vigezo vinane kubainisha ukuruba na tofauti zilizopo mintarafu ya dhana hizi. Vigezo hivi vinavyoonyesha tofauti na ukuruba wao ni pamoja na;

#### 2.1.6.1 Tofauti Baina ya Tafsiri na Ukalimani

(i) **Dhana au Maana au Fasili ya Dhana Hizi Mbili**

Kwa mujibu wa Mwansoko na wengine (2013) ukalimani ni uhawilishaji wa ujumbe au taarifa kutoka kwa msemaji wa LC hadi kwa msemewa katika LL kwa njia ya mdomo au mazungumzo. Wanaeleza kuwa ujumbe hupatikana katikaMC na ML katika mazungumzo. Hata hivyo, mkalimani hana muda wa kutosha kujiandaa kwa sababu anatakiwa kukalimani kile anachokisikia wakati ambapo mzungumzaji anaendelea kuzungumza mambo mengine. Mkalimani huzingatia kigezo cha muktadha wa matini, muundo au mfumo wa lugha (imesemwa au ni ishara). Kwa upande mwingine tafsiri ni jaribio la kuwasilisha ujumbe ule ule ulioandikwa katika lugha moja kwa lugha nyingine au ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo katika maandishi

kutoka lugha moja hadi lugha nyingine. Tafsiri hufanywa katika maandishi kwa kujumuisha upya ujumbe wa LC katika LL kwa kuzingatia isimu, muktadha na utamaduni wa matini husika.

(ii) **Mtindo au Stadi Maalumu za Lugha Husika**

Taaluma ya tafsiri huhusisha stadi kuu mbili muhimu ambazo ni kusoma na kuandika ili kufanikisha mchakato mzima wa tafsiri. Taaluma ya ukalimani huhusisha stadi kuu za kusikiliza kutoka kwa msemaji wa LC na kuzungumza kwa walengwa katika LL na kutunza kumbukumbu za matini husika akilini mwa mkalimani.

(iii) **Kigezo cha Utendaji Kuhusiana na Vifaa vya Kazi**

Taaluma ya tafsiri huweza kushirikisha vifaa kama vile kamusi, kalamu, daftari na hata mashine za kisasa kama vile tarakilishi lakini taaluma ya ukalimani hutumia akili ya mkalimani na uamilifu wake wa LC na LL.

(iv) **Kigezo cha Mfumo wa Lugha**

Taaluma ya tafsiri hutumia mfumo wa lugha ya maandishi. Taaluma ya ukalimani hutumia mfumo wa lugha ya mazungumzo na ishara kwani mkalimani hukalimani mfululizo au andamizi hivyo mkalimani hufanya kazi kwa kasi ili kuendana na kasi ya mzungumzaji wa MC huku akifuata mfumu wa lugha mbili husika.

(v) **Kigezo cha Uhawilishaji**

Katika taaluma ya tafsiri, mtafsiri ana nafasi ya kudurusu kazi aliyopewa kutafsiri na tafsiri yake ili kuondoa na kurekebisha makosa yaliyojitokeza katika matini ya tafsiri yake. Katika taaluma ya ukalimani, mkalimani hana nafasi ya kudurusu matini lengwa hata kama kuna kosa lililojitokeza. Hii ndiyo maana ukalimani una makosa mengi ya kimatamshi, kisarufi na kiuteuzi wa msamiati ambao unahitajika kuwa kisawe cha msamiati wa matini chanzi. Uhawilishaji wake huwa ni mara moja mazungumzo yanapoendelea.

(**vi**) **Kigezo cha Muda**

Taaluma ya tafsiri huchukua muda mrefu wa maandalizi ya maandishi, hela nyingi na wakati wa kutosha ili kuhawilisha ujumbe ulio bora kutoka LC hadi LL. Hadhira ya tafsiri huwa ni ya mbali au tuli. Taaluma ya ukalimani huchukua muda mfupi wa kuhawilisha ujumbe kutoka LC hadi LL kwani huhitajika papo hapo katika mawasiliano mikutanoni, kwenye makongamano, warsha au hata mahakamani ambapo mkalimani anakalimani mfululizo au andamizi kuendana na msemaji wa LC. Hadhira ya taaluma ya ukalimani huwa tendi au hai.

(vii) **Ukongwe, Umri au Historia**

Baina ya ukalimani na tafsiri ni ipi iliyotangulia? Taaluma ya tafsiri imeanza hivi karibuni baada ya majilio ya maandishi kwani baada ya maandishi kuwepo ndipo taaluma hii ya tafsiri ikaanza. Ukalimani ni taaluma kongwe zaidi kwani mazungumzo yalikuwepo kabla ya maandishi. Hivyo basi, ukalimani ulianza utangamano wa kijamii ulipogundua kuwa kulikuwa na haja ya kukalimani mawasiliano hususan katika shughuli za kibiashara, kidini na nyanja nyinginezo.

(viii) **Kigezo cha Utunzaji wa Kumbukumbu**

Kumbukumbu ya taaluma ya tafsiri inahifadhiwa katika maandishi na hivyo hudumu kwa muda mrefu. Kumbukumbu ya taaluma ya ukalimani huhifadhiwa akilini mwa mkalimani na katika mazungumzo kinatharia na kivitendo.

### 2.1.6.2 Kufanana kwa Tafsiri na Ukalimani

Tafsiri na ukalimani,kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo, ni taaluma mbili ambazo hukurubiana pakubwa;

(i) **Kigezo cha Kufasili**

Taaluma zote huafikiana katika mambo makuu manne; mtoa ujumbe, ujumbe wenyewe, mhawilishaji ujumbe na mpokeaji wa ujumbe uliohawilishwa kutoka MC hadi ML. Mchango wa

kila kipengele ni muhimu katika taaluma zote mbili ili kukamilisha mchakato mzima wa tafsiri na ukalimani.

(ii) **Njia, Kibebeo au Uendeshwaji**

Taaluma zote huendeshwa na binadamu wenye umilisi wa LC na LL ili kufanikisha ujumbe uliokusudiwa katika LL.

(iii) **Lengo au Dhima Zao**

Taaluma zote mbili hulenga kufanikisha mchakato wa mawasiliano kati ya watu au jamii mbili au zaidi zinazotumia lugha tofauti.

Licha ya kuwa na tofauti kati ya ukalimani na tafsiri katika vijenzi au vipengele vya muundo wa mawasiliano kutoka kwa mwasisi hadi kwa mlengwa, taaluma zote mbili hutumia mfumo wa lugha husika kama chombo cha kuhawilisha majibu ya ujumbe katika matini chanzi na matini lengwa. Licha ya kufanana na kutofautiana kwa dhana au taaluma hizi mbili, mtafsiri na mkalimani hawana budikuzingatia isimu ya sarufi ya lugha husika, utamaduni, muktadha husika na historia ya jamii husika katika mawasiliano ya matini husika.

## 2.2Nadharia ya Usawa

Katika utafiti huu, nadharia ya usawa imetumika ili kuchunguza na kubainisha changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji kesi katika mahakama. Kwa mujibu wa Fawcett (2003) hii ni nadharia mojawapo inayohusishwa na isimu ambayo iliasisiwa na Koller (1979). Nadharia hii inabainisha namna mtafsiri anavyoweza kufanikisha tafsiri ya matini kutoka LC hadi LL.Koller anadai kuwa tafsiri na ukalimani hutegemea pakubwa lugha na utamaduni wa watumizi wa lugha hiyo. Pia, kwa mujibu wa Snell-Hornby (1988)iwapo wakalimanii au watafsiri wawili wanaweza kutafsiri makala, si rahisi yalandane kwa kila jambo kwa sababu watafsiri hao wana mitazamo-ulimwengu tofauti. Isitoshe,

Bell na Catford (1965) wanadai kuwa nadharia yoyote ya tafsiri inafaa kukopa mno kutoka nadharia ya kiisimu au lugha.

Nadharia hii inasisitiza kuwa ni vigumu kupata tafsiri inayolandana kutoka LC hadi LL. Ingawa inaamimiwa kuwa nadharia ya usawa iliasisiwa na Koller (1979) wataalamu wengi wakiwemo Vinay na Darbelnet (1958), Jakobson (1959), Catford (1965), Kommissarov (1967) na Nida na Taber (1969) walikuwa wameishughulikia katika viwango mbalimbali. Wataalamu wengine wa taaluma ya tafsiri waliochangia kukomaa kwa nadharia hii ni pamoja na Newmark (1981), Baker (1992), House (1997) na miaka ya hivi karibuni, Pym (2010). Wataalamu hawa wa taaluma ya tafsiri walichangia katika kuelekeza usomi wa taaluma ya tafsiri katika uwanja wa elimu.

### 2.2.1 Mawazo ya Catford (1965) Kuhusu Nadharia ya Usawa

Catford (1965) anaeleza kuwa kuna aina mbili za kulandana kwa makala. Aina hizo mbili za usawa ni;

(i) Usawa wa matini katika mawasiliano rasmi ambapo mfumo mzima wa lugha ya jamii husika (langue) hutegemewa. Kwa mujibu wa Catford, mfumo wa lugha katika mawasiliano rasmi hukuza usawa wa matini.

(ii) Usawa wa matini ambapo lugha hutafsiriwa kama inavyotumika na mtumizi mmoja (parole) hutegemewa.

Katika nadharia hii ya usawa, Catford anaeleza kuwa msamiati wa lugha asilia unalandanishwa na msamiati wa lugha pokezi ili kuchukua nafasi yake katika matini pokezi. Anazidi kusema kuwa huenda ikawa vigumu kupata tafsiri inayolandana ikiwa matini inayotafsiriwa inahusu tamaduni tofauti na miundo ya lugha ni tofauti.

Catford amesisitiza kuwa tafsiri hutegemea jamii na mfumo mzima wa lugha husika na pia mtumizi wa lugha husika katika mawasiliano. Catford hakueleza kanuni za kufuata wala viwango vya lugha ambavyo vinafaa kuzingatiwa katika tafsiri au ukalimani ili kufikia usawa wa vipengele vya LC na LL.

### 2.2.2 Mawazo ya Nida (1969) Kuhusu Nadharia ya Usawa Unaobadilika

Nida na Taber (1969) wanaeleza kuwa kanuni za tafsiri zinafaa kubadilika kutoka kutegemea matini hadi kwenye maoni ya msomaji, msikilizaji au mpokezi wa matini. Hii inamaanisha kuwa kutakuwa na matokeo mengi tofauti tofauti kutegemea idadi ya wapokezi wa matini husika. Kanuni ya tafsiri na ukalimani inategemea msamiati katika matini chanzi wenye maana inayolandana au kukaribia kuwa sawa na wa lugha pokezi na pia mtindo unaofaa katika lugha hiyo pokezi. Hivyo basi, mtafsiri anafaa kutafuta kusawazisha wala si kulandanisha matini katika LC na LL. Nida anasema kuwa tafsiri haiwezi kulandana moja kwa moja na matini asilia kwa sababu kila lugha huwa na pengo fulani kimsamiati kwa sababu ya kutokuwa na kiashiria na kiashiriwa kilicho katika lugha na utamaduni mwingine.

Nida (1976) anasisitiza kuwa muktadha na muundo wa kiisimu wa lugha chanzi ya matini na lugha pokezi ya matini unastahili kufuatwa katika uandishi wa makala mapya. Hii ni kwa sababu lugha hubadilika kwa kasi kutoka muktadha mmoja hadi mwingine na kipindi kimoja cha wakati hadi kingine na mtafsiri anafaa kuhakikisha kuwa anafuatilia mababadiliko hayo ya muktadha na maumbo ya lugha asilia na lugha pokezi katika tafsiri yake.

Hapa Nida anasisitiza kuwa jambo muhimu katika tafsiri nimuktadha na muundo wa matini na usawa wa msamiati uliotumiwa katika LC na uteuzi wa kisawe chake katika LL. Pia, anafafanua kuwa mabadiliko ya maumbo ya LC na LL hutegemea muktadha na kipindi cha matumizi na maoni ya mtafsiri na msomaji wa matini husika.

Hata hivyo, Nida anaeleza kuwa kuna changamoto za usawa wa lugha katika tafsiri ya misemo na methali kwa sababu mitindo hii hufungamanishwa na utamaduni wa lugha husika na hakuna lugha mbili zinazokuwa na viashiria sawa katika kurejelea kitu kimoja. Hivyo basi anapendekeza kuwa semi zenye maana inayokaribiana kimaana katika LL zitumiwe katika ML ili kufidia nafasi ya semi zilizotumiwa katika MC ili kubainisha ujumbe uliokusudiwa katika muktadha asilia husika.

### 2.2.3 Mawazo ya Komissarov (1978) Kuhusu Usawa Elekezi na Uliotapanyika

Komissarov (1978) alizua wazo kuwa nadharia ya usawa inafaa kuwa na usawa elekezi na uliotapanyika. Aliendelea kueleza kuwa usawa utafikiwa ikiwa viwango vitano vya kanuni katika tafsiri au ukalimani vitafuatwa.

Kulingana na Komissarov (1978) nadharia hii ya usawa hutafuta maana zaidi ya neno lilivyo katika matumizi yake ya kawaida ambapo anataja viwango vitatu vya kuzingatiwa katika tafsiri ambavyo ni maumbo, maana au ujumbe na uhalisia wa muktadha. Viwango hivi ni sawa na viwango vya Van den Broeck(1981) ambavyo vinaanzia kiwango cha sentensi au sintaksia, ujumbe wa kisemantiki na kipragmatiki kutegemea maana na maoni ya msomaji. Komissarov anaendelea kueleza kuwa viwango vitano huhitajika katika mchakato mzima wa tafsiri na viwango hivyo hujengana kutoka kiwango cha kwanza hadi kingine kama ifuatavyo:

(i) Katika kiwango cha kwanza, sharti kuwe na usawa katika kiwango cha ujumbe kwa jumla bila kujali asili ya matini au muktadha wake katika lugha chanzi na lugha pokezi.

(ii) Katika kiwango cha pili, mtafsiri anafaa kusawazisha muktadha wa lugha ya matini asilia na ile ya matini pokezi.

(iii) Katika kiwango cha tatu, mtafsiri anafaa kusawazisha dhima ya mawasiliano katika muktadha wake wa matini pokezi na ule wa matini asilia.

(iv) Kiwango hiki cha nne humhitaji mtafsiri kuzingatia muundo na uhusiano wa kisintaksia na wa kisemantiki hivi kwamba muundo wa sentensi katika matini unafaa kusalia ulivyo ili maana iliyokusudiwa kujitokeza ilivyotarajiwa.

(v) Katika kiwango hiki cha mwisho mtafsiri anafaa kuonyesha uhusiano wa karibu sana uliopo baina ya matini asilia na matini pokezi kimofolojia, kisintaksia, kimtindo na kimaana.

Utaratibu au hatua hizi za Komissarov humsaidia mtafsiri kutoa tafsiri ambayo haijifungi kwenye tafsiri ya neno kwa neno. Mawazo haya huhimiza kuwa katika tafsiri, mtafsiri sharti azingatie ujumbe, muundo, muktadha na dhima ya matini chanzi na matini lengwa huku akionyesha uhusiano wa viwango hivyo katika MC na ML.

**2.2.4 Mawazo ya Koller (1979) Kuhusu Usawa**

Koller (1979) anaeleza kuwa usawa unaweza kufikiwa katika tafsiri ikiwa mambo yafuatayo yanaweza kuzingatiwa:

(a) Ikiwa kiashiriwa kilichomaanishwa kilizingatiwa. Mwandishi au mzungumzaji anapotumia neno fulani, huwa anakusudia nini? Hii inamaanisha kuwa kusudio la mwandishi au msemaji wa maneno fulani ni muhimu kuliko maana na matumizi ya neno hilo katika kamusi ya lugha husika.

(b) Kwa kuonyesha maana inayotokana na msamiati uliotumika kutegemea;

(i) Kiwango cha umilisi wa lugha husika. Umilisi wa lugha wa mwandishi au mzungumzaji waweza kuwa wa kiwango cha juu au chini, lugha ya kiushairi au kinatharia inayoeleweka au ya kikale, sheng au hata lugha matusi. (ii) Kiwango cha lugha ya mtumizi kinaweza kuwa cha kisajili, yaani lugha ya makundi mbalimbali kama vile jeshi, madaktari, wanasheria au wanasiasa. (iii) Kiwango cha lugha kinaweza kutegemea lahaja. Lahaja au kilugha cha eneo

fulani la Kijiografia. Hivyo basi, wanakundi pekee wanaweza kuelewa maana iliyokusudiwa na msemaji.(iv) Njia ya mawasiliano iliyotumiwa ni muhimu kwani kuna tofauti kubwa baina ya mawasiliano yaliyotolewa ana kwa ana, kwa simu na mawasiliano ya kuandikwa.(v) Jinsi, namna au mtindo wa lugha uliotumika. Je, MC ina matumizi ya tamathali za lugha auni lugha ya kawaida, mtindo uliotumika umepitwa na wakati au bado unaendelea kutumiwa? (vi) Kiasi cha matumizi: yaani msamiatihuo unatumika kila wakati au kwa nadra sana katika mawasiliano ya wanajamii husika. (vii) Muktadha, matilaba au taaluma husika; yaani muktadha ni wa kawaida, kisheria, kisayansi au kiteknolojia. (viii) Dhima au umuhimu; Dhima ya mawasiliano ina matokeo chanya au hasi na athari yake ni ipi kwa wahusika? (ix)Toni ya kihisia inayojitokeza katika mawasiliano husika; toni husika ni ya kati au isiyo na hisia zozote, kutojali au ni ya mapokezi.

(c) Kaida za matini husika; Mtafsiri au mkalimani anafaa kuzingatia ile lugha ambayo kawaida hutumika katika muktadha na mada husika. Ikiwa ni siasa, lugha iliyojaa porojo itatumika, ikiwa ni kortini lugha rasmi itatumika na ikiwa ni kanisani basi lugha ya kushawishi pamoja na ya kutisha wakati uohuo itatumika.

(d) Maana ya kipragmatiki kutokana na msikilizaji na msomaji ni muhimu. Yaani, msomaji au msikilizaji anatarajia nini kutokana na makala husika kulingana na mtazamo wake wa maisha? Mara nyingi msomaji au msikilizaji hutafsiri makala kulingana na mwonoulimwengu na hisia zake wakati wa kusoma au kusikiliza makala husika. Kwa hivyo, mtafsiri wa matini moja anaweza kuwa na maana nyingi kutegemea hisia zake wakati wa kusoma makala husika.

(e) Tamathali na fani za lugha ni muhimu katika mawasiliano: Mtafsiri au mkalimani anafaa azingatie tamathali za lugha katika matini husika. Fani hizo ni kama vile, vina na mahadhi katika

ushairi pamoja na tamathali kama vile jazanda, tashihisi, methali, misemo na tashibiha katika ushairi na makala ya kinatharia.

Reiss (1977) anaeleza kuwa usawa wa matini huhusishwa na tafsiri au ukalimani wa matini katika umbo asilia. Reiss anahusisha sifa za matini na mtindo wa tafsiri unaotumika kwa sababu kila matini huhitaji mitindo tofauti ya tafsiri. Kwa mfano, matini ya kufahamisha hutumia mbinu ya maelezo pekee na kiwango cha lugha kinachotumika huwa ni cha kimantiki. Pia, lugha hurejelea matini na mada na ujumbe ndio muhimu katika mawasiliano. Lakini ikiwa makala ni ya ufafanuzi, huhitaji ubunifu na mwandishi au mkalimani atatumia lugha yenye mvuto na ya kupendeza. Kwa hivyo, Reiss anasisitiza kuwa kila aina ya matini huwa na matumizi ya lugha tofauti na hivyo katika tafsiri, mtafsiri anafaa kuzingatia jambo hili.

Kwa mujibu wa Fawcett (2003) wataalamu hawa wa lugha wanakubaliana kuwa Nadharia ya Usawa ndiyo msingi imara wa tafsiri kwa sababu inamkumbusha mkalimani kuwa atakabiliwa na changamoto tele za usawa wa vipengele vya lugha katika shughuli ya ukalimani. Pia, wanakubaliana kuwa usawa unaweza kufikiwa katika ukalimani iwapo vipengele maalumu vya lugha mbili husika vitazingatiwa na mkalimani. Hata hivyo, hakuna lugha mbili ambazo zinaweza kutumia leksimu, virai, vishazi na sentensi sawa kuashiria kitu kimoja. Haya ni maumbo ambayo msemaji anayateua ili kuwasilishia ujumbe wake na mkalimani anajaribu kukalimani akizingatia kuwa usawa katika kila kipengele cha lugha ni jambo ambalo haliwezekani. Hivyo basi, usawa katika ukalimani ni jambo la kukisiwa tu.

Nadharia hii inabainisha kuwa kipengele muhimu ambacho kinafaa kuzingatiwa katika ukalimani ni ujumbe wa msemaji katika diskosi yake. Ujumbe unaweza kuwa wa kisemantiki na kipragmatiki kutokana na msamiati uliotumika kutegemea kiwango cha lugha ya msemaji.

Mkalimani basi anafaa kuelewa ujumbe katika LC na kuutafsiri kisemantiki na kipragmatiki katika LP.

Kwa mujibu waReiss (1977) usawa wa matini huhusishwa na tafsiri au ukalimani wa matini katika umbo asilia. Reiss anahusisha sifa za umbo la matini na mtindo wa tafsiri unaotumika kwa sababu kila matini huhitaji mitindo tofauti ya tafsiri. Kwa mfano, matini ya kufahamisha hutumia mbinu ya maelezo pekee na kiwango cha lugha kinachotumika huwa ni cha kimantiki. Pia, lugha hurejelea matini na mada na ujumbe ndio muhimu katika mawasiliano. Lakini ikiwa makala ni ya ufafanuzi, huhitaji ubunifu na mwandishi au mkalimani atatumia lugha yenye mvuto na ya kupendeza. Kwa hivyo, Reiss anasisitiza kuwa kila aina ya matini huwa na matumizi ya lugha tofauti. Kwa hivyo, katika tafsiri mtafsiri anafaa kuzingatia jambo hili.

Pia, kipengele cha mtindo wa lugha uliotumika ni muhimu na mara nyingi hutegemea muktadha wa diskosi. Mtindo wa lugha katika MC huwa muhimu katika kuwasilisha ujumbe na iwapo mkalimani hazingatii mtindo huo na kuutafsiri ipasavyo, huenda ujumbe wa mhusika ukaathirika. Hivyo basi, mtindo wa lugha katika MC hufaa kutafutiwa visawe mwafaka katika LP. Mitindo ya lugha inayozingatiwa hapa ni tamathali za lugha kama vile tashbiha, jazanda, methali, istiara, misemo na tasfida katika MC na visawe vyake au inavyotafsiriwa katika ML.

Isitoshe, kulingana na nadharia hii, kipengele cha maumbo ya MC huathiri ujumbe katika ML. Maumbo yanahusu mofimu au leksimu, virai, vishazi na muundo wa kisintaksia katika diskosi za wahusika. Usawa wa kimaumbo huzingatiwa katika ukalimani wa matini katika umbo chasila. Hivyo basi msamiati wa LC unalandanishwa ama kusawazishwa na msamiati wa LL ili kufaa katika ML. Hata hivyo, huenda ikawa vigumu kupata tafsiri inayolandana ikiwa matini inayotafsiriwa inahusu tamaduni mbili tofauti. Hii ni kwa sababu maumbo ya lugha hutofautiana

na hivyo kuna pengo la msamiati baina ya lugha mbili husika. Koller (1979) anazidi kueleza kuwa ikiwa wakalimani wawili watatafsiri matini, si rahisi tafsiri zao kulandana katika kila kipengele cha lugha kwa sababu wakalimani hao wana mitazamoulimwengu tofauti ingawa wanazungumza lugha moja mahususi. Usawa wa matini katika mawasiliano rasmi kama vile mahakama, hutegemea mfumo mzima wa lugha ya jamii husika (Langue) ambao hukuza usawa wa matini. Nadharia hii ya usawa hutafuta maana zaidi ya neno lilivyo katika matumizi yake ya kawaida. Huamini kuwa maana ya neno hutokana na mazingira au muktadha ambamo limetumika na maana ya maneno ambayo yanalizunguka neno husika.

Koller (1979) anaendelea kubainisha kuwa kipengele cha usawa wa toni ya kihisia ya msemaji ni muhimu na inafaa kuzingatiwa katika tafsiri ya matini ingawa haina maumbo maalum ambayo yatajitokeza wazi. Toni kuhusiana na uhalisia au mandhari ya matumizi hutegemea hali ya msemaji. Mkalimani anafaa kuwa mwangalifu ili kutambua hisia hizo katika uteuzi wa msamiati au kidatu na kiimbo cha msemaji anapowasilisha ujumbe wake.

Vipengele vingine muhimu katika ukalimani kulingana na Koller (1979) ni utamaduni unaohusu lugha husika na mandhari au mazingira ya matukio ambayo yanatafsiriwa. Pia, enzi za tukio hudhibiti uteuzi wa msamiati unaotumika katika LC na LL kwani msamiati hubadilika jinsi wakati unavyopita kwa sababu matukio mapya huzua msamiati mpya.

Katika utafiti huu, nadharia ya usawa imetumiwa kuchunguza changamoto za usawa wa vipengele vya;

i) Ujumbe katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama. Utafiti huu umechunguza iwapo mkalimani alifikia usawa katika kipengele cha ujumbe wa

kisemantiki na kipragmatiki kwa jumla katika LL kwa kuzingatia muktadha wa MC. Ikiwa hakufikia kiwango hicho cha usawa, changamoto ambazo alikabiliana nazo katika kutafsiri kipengele hiki zitakuwa zimebainika katika uchanganuzi wa data teule ya utafiti huu.

(ii) Maumbo katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika mahakama wakalimani walipotafsiri matini kutoka muktadha wa LC hadi LL. Maumbo hayo ni leksimu, virai, na sintaksia. Maumbo ya LC na LL yalifikiwa ama wakalimani walikumbwa na changamoto zozote za usawa baina ya lugha hizo husika?

(iii) Mtindo uliotumika katika ukalimani wa matini ya diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama kutoka LC na mtindo wa wakalimani katika LL. Mtindo unahusu tasfida, methali, jazanda, tashbiha, istiara na misemo katika matini husika. Mtafiti amechunguza iwapo wakalimani walisawazisha mtindo wa LC na LL katika ukalimani wa diskosi za wahusika.

(iv) Toni za kihisia katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama. Utafiti ulizingatia namna ujumbe ulivyowasilishwa katika LC na namna wakalimani walivyouwasilisha katika LL kitoni.

Mbinu za ukalimani ambazo zimetumiwa na wakalimani ni muhimu sana katika utafiti huu huku nadharia ya usawa ikiongoza katika hatua zote. Wakalimani walikuwa na hiari ya kutumia mbinu ya ukalimani wa neno kwa neno, ukalimani sisisi au ukalimani wa kipragmatiki au hata kuchanganya mbinu zote za ukalimani kila zilipofaa au kuhitajika katika shughuli yao. Pia, walikuwa na hiari ya kubuni mbinu za kukalimani matini ya mhusika kama vile; kudondosha msamiati, kueleza, kutumia visawe, kukopa au kuchopeka ujumbe ilivyofaa kutegemea makala husika.

Kipengele cha utamaduni kimetajwa kuwa muhimu katika tafsiri na ukalimani katika nadharia hii ya usawa na vile vile katika ufafanuzi wa dhana ya tafsiri na ukalimani. Kwa hivyo, ni muhimu kueleza dhana ya utamaduni na mwingiliano wake na lugha ambazozinahusishwa kakita tafsiri na ukalimani.Ili kuelewa uhusiano baina ya utamaduni, ukalimani na tafsiri, ni vyema ikiwa kwanza maelezo yatatolewakuhusu dhana ya utamaduni kisha kubainisha uhusiano kati ya ukalimani na utamaduni.

**2.3Dhana ya Utamaduni**

Dhana ya tafsiri, ukalimani na nadharia ya usawa zimehusishwa pakubwa na suala la utamaduni katika ufafanuzi wao. Itakuwa bora kutoa maelezo kuhusu maana ya utamaduni na uhusiano baina ya lugha na utamaduni. Pia, maelezo kuhusu utamaduni katika tafsiri na ukalimani pamoja na vipengele vigumu kutafsiri na kukalimani kwa kuzingatia utamaduni na mikakati ya kutafsiri na kukalimani kwa kuzingatia utamaduni. Hii ni kwa sababu utamaduni na lugha ni mambo ambayo hayawezi kutenganishwa. Kamusi ya TUKI (2000) inaeleza kwamba utamaduni ni mila, asili, jadi na desturi za kundi la jamii fulani. Hii inamaanisha kuwa matendo yote ya jamii moja pamoja na mwonoulimwengu wa wanajamii husika ni utamaduni wa jamii hiyo.

Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanasema kuwa utamaduni ni imani, mbeko, miiko na miundo ya familia au jamii. Miundo hii yote ndiyo inayotambulisha na kuitofautisha jamii moja na nyingine na hivyo ndio utamaduni wao. Miundo hiyo ni michakato mbalimbali ambayo hupatikana katika utamaduni mmoja kutokana na kaida na kanuni katika jamii husika. Miundo hii ni pamoja na dini, lugha na matumizi yake, chakula, miviga, mavazi ya nyakati mbalimbali na mahusiano baina ya wanajamii wake.

Wardhaugh (2006) anadai kuwa utamaduni ni chochote ambacho mtu hufaa kujua ili kuweza kuishi na kutangamana vyema na wanajamii wa jamii husika. Haya ni sawa na maoni ya

Goodenough akinukuliwa na Wardhaugh (2006) anapodai kuwa utamaduni ni chochote kinachofaa mtu kujua na kuamini ndipo atangamane vyema na wengine katika jamii husika kwa njia itakayokubalika na wanajamii husika na aweze kuchukua nafasi yoyote ya kijamii atakayopewa katika jamii hiyo. Mambo haya mtu huyajua kwa kujihusisha wala si kwa kufunzwa. Hivyo basi, nadhani kuwa mambo hayo ni pamoja na; lugha, miviga, miiko, mila, desturi, mahusiano baina ya wanajamii, imani au dini, chakula, mbeko na mavazi ya jamii husika ili aweze kukubalika katika jamii hiyo.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa utamaduni ni uzoevu wa kimaisha wa watu fulani. Kwa kawaida neno hili huleta michakato ya kijamii ambayo huwezesha jamii hiyo kujieleza na kujitambulisha na kufanya shughuli zao za kila siku pamoja. Kulingana na Wamitila, mambo yote yanayowafanya watu kujitambulisha na kufanya shughuli zao za kila siku kwa pamoja yanaweza kuitwa utamaduni.

Naye Yule (2006) anafasili utamaduni kuwa ni mambo yote tunayoyajua kuhusu jamii hiyo tunapokuwa wanajamii bila kufunzwa. Tunapojifunza lugha ya kwanza, inatuwezesha kuelewa utamaduni wa jamii husika na kutuwezesha kupanga na kutenga mambo katika mazingira yetu na ujuzi wetu katika jamii. Kwa mfano, katika utamaduni fulani kama kunakosa kiashiriwa fulani, basi hakutakuwa na kiasshiria, msamiati au neno la kurejelea kiashiriwa hicho.

Basi ni dhahiri kuwa kuna uhusiano kati ya lugha na utamaduni na kwamba lugha hubeba utamaduni wa jamii fulani na uhusiano huohauwezi kuwekewa mipaka: huwezi kutenga lugha na utamaduni. Hii ndio sababu mtafsiri anapotafsiri matini kutoka lugha-chanzi hadi lugha-pokezi, inamwia vigumu kutafsiri utamaduni wa lugha chanzi hadi ule wa lugha pokezi moja kwa moja. Kwa sababu hii anafaa kuwa na mikakati maalumu ya kumwezesha kutafsiri matini chanzi kwa njia ambayo itawaridhisha wasomaji wa matini katika lugha pokezi. Pia, ni wazi kwamba

mtafsiri anafaa kuelewa utamaduni wa lugha chanzi na wa lugha pokezi ili kufaulu kuandika tafsiri inayofaa. Vivyo hivyo, katika utafiti huu mkalimani anafaa kuelewa utamaduni wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza ili kutekeleza ukalimani utakaokubalika katika LL. Lugha hizi mbili zina utamaduni tofauti utakaoathiri ujumbe, maumbo, mtindo na toni katika LC na LL.

### 2.3.1 Uhusiano Kati ya Lugha na Utamaduni

Iribemwangi na Mukhwana (2011), Fishman (1972) na Wardhaugh (2006) wanakubaliana kuwa kuna mahusiano makubwa baina ya lugha na utamaduni. Kuna mahusianomanne yanayohusisha lugha na utamaduni. Mahusiano hayo ni kama yafuatayo:

(i)Wardhaugh (2006) anaeleza kuwa uhusiano wa kwanza ni kuwa muundo wa jamii unaweza kuathiri muundo wa lugha.Kwa mfano,katika kiwango cha umri,mtoto atazungumza kwa namna iliyo tofauti na watu wazima.Utafiti unaonyesha kuwa aina ya lugha ambayo mzungumzaji hutumia huonyesha masuala kama vile anakotoka mtu huyo, kabila lake,jinsia yake, hadhi yake katika jamii na imani yake.Pia, utafiti unaonyesha kuwa uteuzi wake wa maneno na kanuni za kuongoza mjadala hutegemea mahitaji fulani ya kijamii kati ya mzungumzaji na mzungumziwa na muktadha au mada inayozungumziwa.

(ii) Uhusiano mwingine, unaoelekea kupinga uhusiano wa kwanza, unadai kuwa muundo wa lugha au tabia yake yaweza kuathiri au kuamua muundo wa kijamii. Maoni haya ni sawa na yale ya Whorf (1956)anayesema kuwa binadamu hutambua au hufahamu kile ambacho lugha yake inacho, yaani lugha hutawala mwonoulimwengu wa watumizi wa lugha husika.Kwa hivyo, wazungumzaji wa lugha tofauti watakuwa na mwonoulimwengu tofauti.

(iii)Mgullu(1999) naye aneleza kuwa uhusiano mwingine ni ule ulio na mtazamo kuwa kuathiriana kwa lugha na utamaduni ni kwa njia mbili. Hii ni kusema kuwa lugha na utamaduni

huathiriana kwa maana lugha huathiri utamaduni na utamaduni huathiri lugha. Mawazo haya ni sawa na yale ya nadharia ya lugha ya Wardhaugh (2006) na Whorf (1956) yanayodai kuwa mahusiano kati ya lugha na utamaduni ni jambo ambalo haliwezi kueleweka na huwezi kuhakiki moja na kuacha jingine kwa vile kuna mtagusano mkubwa kati ya lugha na utamaduni hivi kwamba huwezi kuzungumzia moja bila ya jingine.

(iv) Katika uhusiano wa aina ya nne,wanaisimujamii Chomsky (1957) na Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanadai kuwa hakuna uhusiano wowote kati ya muundo wa lugha na muundo wa jamii au utamaduni.Huamini kuwa miundo hii ni huru na kila mmoja hujisimamia.

Kutokana na mitazamo hii yote kuhusu lugha na utamaduni, ni dhahiri kuwa lugha ni mali ya mwanadamu kwa kuwa ndiye mwenye kuimiliki na kuitumia katika mawasiliano.Pia, kwa vile lugha hubeba maana, haina budi kuoana na utamaduni wa jamiilugha husika.Kwa hivyo, lugha ni utamaduni na utamaduni ni lugha.Madai haya yanathibitishwa kwa kuzingatia maoni kuwa kila lugha ina uwezo wa kuyaeleza mambo yote yanayoendelea katika ulimwengu wa jamii husika kwani hakuna jambo linaloweza kuelezwa bila kutumia lugha aidha kwa kutumia msamiati moja kwa moja au kwa kutumia tasfida au hata kwa kutumia maelezo marefu.

Katika utafiti huu ieleweke kuwa lugha zilizohusishwa katika ukalimani zimefungamanishwa na utamaduni wa jamii-tumizi-lugha. Kwa hivyo, suala la utamaduni limeathiri matumizi ya lugha aidha katika MC au ML. Ikiwa suala la utamaduni litakuwa limeathiri lugha katika MC, basi lugha katika ML pia itaathirika au ikiwa mkalimani ameathiriwa na utamaduni katika kukalimani lugha ya MC hadi ML, basi vipengele muhimu vya lugha kama vile ujumbe, muundo, mtindo na hata toni vitaathiriwa.

### 2.3.2Utamaduni, Tafsiri na Ukalimani

Mtafsiri wa matini akizingatia utamaduni, anahitaji mno aina ya nadharia ya tafsiri ya Kiethnografia na Kiisimujamii ambapo atalenga kusisitiza uasilia wa utamaduni wa mwandishi na utamaduni wa wasomaji wa lugha lengwa. Nadharia mahususi basi ni nadharia ya usawa inayojumuisha ethnografia na isimujamii. Hivyo basi, mtafsiri atazingatia tofauti za kitamaduni baina ya wanajamii wa lugha chanzi na lugha pokezi.

Katika kutafsiri, mtafsiri hufaa kuzingatia;

(i) Ujumbe ambao umebebwa na matini husika. Je, ni ujumbe wa mapenzi, kisiasa, kijamii au kiuchumi?

(ii) Maumbo au miundo ya matini husika. Je ni shairi, barua, hotuba, tamthilia, riwaya au ni mchanganyiko wa maumbo au miundo hii yote?

(iii) Sarufi. Ni sahihi au imeborongwa? Kwa nini iko vile ilivyo?

(iv) Kipindi cha kutekeleza tafsiri hiyo au muktadha wa tafsiri. Tafsiri inafanyika katika kipindi kipi cha kihistoria ya jamii ya mtafsiri? Kuna vita, uongozi wa kiimla na hali ya kiuchumi ipi?

(v) Dhamira ya matini. Mwandishi alipoandika aliwaandikia kina nani na kwa nia gani?

(vi) Muktadha wa uandishi wa matini yenyewe katika lugha chanzi pia ni muhimu kwa sababu mazingira ya mwandishi mara nyingi ndiyo humsukuma mwandishi kuyatungia kazi ya fasihi.

(vii) Torop (2002) anabainisha kuwa hali ya kijamii na kisiasa ya wakati wa kutafsiri na pia utamaduni wa jamii-lugha pokezi ya matini husika ni kipengele muhimu. Kipengele cha utamaduni ni muhimu sana ili matini iweze kuwafaa wapokezi wake. Basi, mtafsiri anafaa kuzingatia imani au dini ya wapokezi wa matini, tabia zinazokubalika katika jamii hiyo, lugha na msamiati wao katika hali mbalimbali za maisha katika jamii, miviga yao, mahusiano ya wanajamii, hali ya uchumi wao, siasa zao, michezo yao, ruwaza za utawala, mavazi na chakula

chao na hata mazingira yao hivi kwamba anapotafsiri kutoka lugha chanzi hadi lugha pokezi anatumia msamiati mwafaka ambao unafaa utamaduni wa lugha pokezi.

Aiello (2013) anaeleza kuwa tafsiri na utamaduni huhusu jinsi watafsiri wanakabiliana na vipengele vya kitamaduni vya lugha chanzi kama vile maisha ya jamii, dini, misemo, methali, msamiati, sarufi, na mahusiano baina ya wanajamii na mazingira yao kwa jumla. Anaendelea kueleza kuwa tafsiri ambayo inahusu utamaduni inahitaji ubunifu mwingi mno ili kukubali makala chanzi kwenye lugha ya makala pokezi kwa kuzingatia matumizi ya lugha, arudhi au kanuni, tamathali za usemi na maumbo au miundo ya matini au masimulizi, ili iweze kusomwa na wanajamii wa lugha pokezi.

Tafsiri inayozingatia utamaduni ina misingi yake katika tafsiri zilizofanywa na wamishenari na watawala wa kikoloni kwa kuzingatia uaminifu kwa makala chanzi za kazi za kidini na kifasihi huku wakitumia othografia, sarufi na hata kamusi za Kirumi. Aiello, anaeleza kuwa tafsiri na utamaduni hustahili kuzingatia mabadiliko ya lugha kiwakati katika lugha chanzi na lugha pokezi ya matini husika. Anasema kuwa lugha ni nyenzo ambayo hubadilika kutoka kipindi kimoja hadi kipindi kingine.

### 2.3.3Mambo Magumu Kutafsiri na Kukalimani kwa Kuzingatia Utamaduni

Armstrong (2005) anadai kuwa kuna vipengele ambavyo ni vigumu mno kutafsiri kutoka utamaduni wa matini asilia hadi utamaduni wa matini pokezi. Mambo hayo ni pamoja na:

(i) Tamathali za usemi kama vile methali, nahau na mafumbo. Katika Kiingereza kwa mfano, ‘*Keepsomethingforarainyday*.’ katika Kiswahili, haitakuwa ‘Weka kitu kwa siku ya mvua.’Maana ya methali hiyo imepotea. Kisawe cha methali hii ya Kiingereza itakuwa na maumbo na leksimu ambazo ni tofauti kimaana lakini maana batini ya methali hiyo ni karibu sawa. Kisawe hicho ni ‘Akiba haiozi’.

(ii)Lafudhi na rejesta iliyotumiwa katika matini asilia kwa sababu inafaa kuhusishwa na lahaja za kijamii na kimaeneo au kijiografia na pengine tabaka la mhusika katika matini. Hii ni kwa sababu kila jamii ina namna inavyotumia lugha katika matabaka na maeneo mbalimbali ya kijiografia.

(iii) Vichekesho au ucheshi pia huwa ni vigumu kutafsiri kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine kwa sababu vichekesho hutofautiana kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine hivi kwamba kinachowachekesha watu wa utamaduni wa matini asili huenda kisiwachekeshe na hata kikawa ni matusi na maudhi kwa watu wa utamaduni wa matini pokezi.

(iv) Miviga na matambiko pia hayawezi kutafsirika kwa sababu huwa ni tofauti au hata huenda yasiwepo kabisa katika utamaduni pokezi. Kwa mfano, baadhi ya jamii hazina miviga ya tohara na jando.

(v) Mazingira au mandhari huwa magumu kutafsiri kwa sababu ya msamiati wa vilivyomo katika mazingira ya tamaduni tofauti kama vile mazingira ya pwani na ya bara au mazingira ya maeneo yanayotengana sana kijiografia.

(vi)Misimu na majira ya mwaka huenda yakawa magumu kutafsiri kwa sababu maeneo kama ya Afrika hayana majira ambayo yanashuhudiwa kule Ulaya.

(vii) Msamiati wa vyakula,mavazina rangi huwa tofauti kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine. Vyakula vya Kizungu ni tofauti na vya Kihindi, Kiafrika au Kifaransa. Kwa mfano, sima au ugali ni msamiati wa chakula ambao haupatikani katika utamaduni wa Wafaransa.

(viii) Mahusiano ya kijamii hasa kuhusiana na ndoa na jamaa katika familia. Kuna baadhi ya jamii ambazo hukubali ndoa kati ya binamu na binamu na hata shangazi na mpwawe kuolewa na mume mmoja lakini katika utamaduni mwingine huwa ni mwiko ndoa kama hizo kutokea. Kwa

mfano, katika jamii ya Abagusii ni mwiko kwa mtu kumuoa binamu yake au mtu kumuoa mwanamke na baadaye amuoe mpwa wa mwanamke huyo.

Tafsiri na ukalimani unaozingatia utamaduni unachukuliwa kama mawasiliano baina ya tamaduni mbili tofauti kwa hivyo mtafsiri na mkalimani anafaa kubadilisha vipengelevyote vinavyohusu utamaduni anapotafsiri matini husika ili kuwafaa wasomaji wa utamaduni wa lugha pokezi. Venuti (1995) na Echo (2003) wanakubaliana kuwa kuubadilisha utamaduni wa matini asilia ili kufaa utamaduni wa matini pokezi huwafanya wasomaji kutambua na kuyapenda makala na kujitambulisha nayo ilhali tafsiri ya kuzingatia ugeni, ikizingatia muundo wa makala chanzi na kuhifadhi vipengele muhimu kuhusu utamaduni wa kigeni,mambo ambayo ni mageni kwa wapokezi wa makala yaliyotafsiriwa, huchosha na hata kutengwa na wasomaji wa matini pokezi.

### 2.3.4 Mikakati Katika Kutafsiri na Kukalimani kwa Kuzingatia Utamaduni

Utamaduni unapoingiliana na lugha tumizi katika ukalimani, mikakati maalumu huwekwa ili kufanikisha shughuli ya ukalimani. Mikakati hiyo ni pamoja na:

(I) Ubadilishaji, udondoshaji na upachikaji. Kulingana na Maria (1984) mtafsiri anaweza kutumia mbinu ya ubadilishaji, udondoshaji na upachikaji ili kufanikisha tafsiri inayohusiana na utamaduni. Anaeleza kuwa mtafsiri anaweza kubadilisha matini kana kwamba anaandika upya matini husika huku akijikita katika mazingira ya utamaduni pokezi kuanzia majina ya wahusika na mahali. Hata anaweza kuunda upya matini kwa kuzipanga sentensi upya na kuacha kabisa kuzingatia marejeleo ya mazingira na majina ya matini asilia.

Pia, katika kipengele hiki mtafsiri anaweza kudondosha sentensi au mafungu ya sentensi ambazo anadhani hazifai na kuchopeka maelezo yake ambayo anabaini yatawasaidia wasomaji wa matini

pokezi kuelewa matini husika. Majina ya wahusika na mahali hubadilishwa kutegemea sifa za lugha ya matini pokezi.

Katika kipengele hiki cha kubadilisha matini ili kufaa utamaduni husika, mtafsiri pia huweza kuchopeka tamathali za usemi katika lugha pokezi ambazo hazikutumika katika matini asilia lakini zinafaa ili kuwasilisha ujumbe kwa sababu kawaida zinatumika katika lugha pokezi. Anaweza hata kubadili dhamira na majina ya wahusika na mandhari ya matini husika kama alivyofanya Kawegere katika tafsiri yake ya riwaya ya '*AnimalFarm'* ya G. Orwell ambayo aliiita 'Shamba la Wanyama' ili kuwafaa Watanzania baada ya kuwekwa Maazimio ya Arusha ya kutaifisha mali ya umma ambapo wachache walijitajirisha kwa kushiriki ufisadi.

Katika kubadilisha matini ili kufaa utamaduni wa lugha pokezi, baadhi ya watafsiri hubadilisha hata anwani ya matini asilia ili kuonyesha dhamira yao ya kuhamisha ujumbe katika lugha na utamaduni tofauti kama alivyofanya Ndulute (1973) alipotafsiri riwaya ya Chinua Achebe '*ThingsFallApart'* ambayo aliiita 'Shujaa Okonkwo'. Ndulute alidondosha shairi lililotumika kutanguliza matini asilia kwa sababu shairi hilo lilirejelea utamaduni wa Kiigbo kule Nigeria. Aliona kwamba shairi husika halikuwa muhimu katika matini lengwa.

(II) Wafula (2009) anaeleza kuwa ukopaji na utohozi ni vipengele maalumu katika tafsiri. Mtafsiri anaweza kukopa baadhi ya msamiati wa utamaduni wa matini asilia na kutoa maelezo kwa wasomaji wa matini pokezi kwa sababu ya utamaduni tofauti ili waweze kuelewa ujumbe. Anaweza kufanya hivyo kwa kuuswahilisha msamiati huo hasa ule wa mahali na wahusika kama alivyofanya mtafsiri wa 'Antigoni'.

(III) Uaminifu ni kipengele kingine muhimu katika tafsiri. Mtafsiri anaweza kuwa mwaminifu kwa matini asilia hivi kwamba anahifadhi ujumbe na dhamira ya matini asilia lakini atoe maelezo ya msamiati alioutumia kuhusiana na matini asilia ili wasomaji wake waweze kuona

hali ya ujumbe lengwa katika utamaduni wake asilia kama alivyofanya Tirumanywa katika 'Mzee wa Bahari' (1980) tafsiri ya '*TheOldManandTheSea'* kitabu cha Ernest Hemingway (1952). Baadhi ya watafsiri hutumia mtindo huu wa tafsiri sisisi bila kujali kueleza maana ya msamiati huo mgeni.

(IV) Mtafsiri anaweza kuchanganya urahisishaji (maelezo marefu), udondoshaji na ubadilishaji wa matini. Mtafsiri anaweza kutafsiri matini akizingatia utamaduni hivi kwamba anachanganya mbinu ya kuhifadhi utamaduni wa matini asilia na katika baadhi ya sehemu abadilishe utamaduni huo inapowezekana. Hapa mtafsiri atachanganya mbinu ya kurahisisha ujumbe, kudondosha ujumbe, kubadilisha ujumbe na azingatie utamaduni wa lugha pokezi kama alivyofanya Ndulute (1973) alipohifadhi majina ya mahali, wahusika, miungu na mizimu, sherehe za matambiko, viashiriwa, imani za jamii husika (Igboland), mitazamo ya wanajamii, nyimbo na ngano zao na hata mandhari ya matini asilia. Baadhi ya msamiati hata unaweza kusalia ulivyo katika matini asilia ili kuhifadhi utamaduni wa matini asilia lakini mtafsiri ataeleza maana ya msamiati aliouhifadhi ili wasomaji wa makala pokezi waweze kuelewa na kufurahia utamaduni husika. Mtafsiri kwa kufanya hivyo hatakuwa ameegemea upande wowote bali atakuwa kama mhamahamaji au mchungaji wa kutembeza mifugo na kuleta habari nyumbani kutoka alikosafiri na mifugo wake. Atakuwa ni mtu wa kati wa kuunganisha tamaduni hizo mbili.

(V) Mtafsiri anaweza kumwandama msimulizi au mhusika mkuu. Maria (1984) anaeleza kwamba matafsiri wa matini asilia kwenye utamaduni mpya anaweza kufuata utaratibu wa kumwandama msimulizi na mhusika mkuu ambao ndio wanawakilisha mtazamo wa kitamaduni. Katika kumjenga mhusika huyo mkuu mtafsiri atapata nafasi ya kuzingatia au kueleza mawazo na maoni yake mwenyewe kuhusu matini. Katika kipengele hiki mtafsiri anaweza kudondosha maelezo ya ziada, mtazamo wa wahusika wajenzi na wasimulizi katika ploti kuu.Badala yake

mtafsiri achopeke maelezo ya ziada ili kuwafahamisha kwa urahisi mambo anayoyaona kuwa muhimu katika matini husika na yanafaa kupitishwa kwa wasomaji wa matini pokezi.

### 2.4 Yaliyoandikwa Kuhusu Suala la Ukalimani Katika Mahakama

Katika sehemu hii, mtafiti amechunguza maandishi kuhusu ukalimani wa matini ya kisheria akizingatia maswali na malengo ya utafiti wake. Ameigawanya sehemu hii katika sehemu nne na kila sehemu itashughulikia lengo mojamoja. Sehemu hii ya kwanza inahusu yaliyoandikwa kuhusu usawa wa ujumbe katika ukalimani wa diskosi katika mahakama. Sehemu ya pili inahusu yaliyoandikwa kuhusu usawa wa maumbo, kisha yaliyoandikwa kuhusu usawa wa mtindo na mwisho kuhusu usawa wa toni katika ukalimani katika diskosi za wahusika wa kesi katika mahakama.

#### 2.4.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Usawa wa Ujumbe Katika Ukalimani wa Diskosi KatikaMahakama

Kwa mujibu wa Owiti (2014), ujumbe uliokusudiwa na mhusika hupotea mkalimani anapotafsiri papo kwa papo diskosi ya mhusika katika mahakama. Kupotea kwa ujumbe hutokana na mkalimani kudondosha au kuchopeka leksimu katika ML anapotafsiri diskosi za wahusika. Hiiinamaanisha kuwa mhusika huenda ikawa hakupata haki ilivyostahili. Hii ndiyo sababu utafiti huu ulifanywa ili kuchunguza changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa matini kutoka MC hadi ML mkalimani anapokalimani diskosi za wahusika katika vikao vya uendeshaji kesi katika mahakama. Mtafiti alifanya utafiti katika mahakama ya Kericho ili kuchunguza na kubaini changamoto za usawa wa vipengele vya lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji kesi.

Kulingana na Odhiambo na wengine (2013), uchunguzi kuwahusu wakalimani katika mahakama ndogo za Mkoa wa Nyanza, Kenya, ulibainisha kwamba wakalimani wa mahakama hizo

hawakuwa wamepokea mafunzo ya tafsiri ya diskosi za kisheria na wengi wao hawakuwa wamepokea mafunzo yoyote ya taaluma ya kisheria wala ukalimani. Kwa vile lugha rasmi ya kisheria na mahakama ni Kiingereza, wahusika wasioweza kuzungumza lugha ya Kiingereza hulazimika kuwatumia wakalimani hao wasio na ujuzi ili kukalimani ujumbe wao. Hii inamaanisha kuwa wakalimani hao huenda wasikalimani kwa usawa vipengele vya lugha ya taaluma ya kisheria katika ukalimani wao na kusababisha mtafaruku au kukosesha mhusika haki ya kuwasilisha ujumbe alivyotarajia. Hii inamaanisha kuwa kuna vipengele vya lugha ambavyo huwa vigumu kukalimani kutoka lugha moja hadi nyingine. Utafiti huu, tofauti na uchunguzi uliofanywa na Odhiambo, umechunguza changamoto zinazohusu usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji kesi katika mahakama.

Satia (2013) alipambanua changamoto zilizowakumba mashahidi walipochunguzwa au kuhojiwa kwa mara nyingine na washukiwa wasiokuwa na ujuzi wa lugha ya kisheria na mahakama. Utafiti huo ulizua maswali iwapo wakalimani waliwaelewa washtakiwa na kukalimani ujumbe wao ilivyofaa kwa mashahidi hao ili kutoa majibu mwafaka kwa maswali waliyoulizwa.Utafiti huu ulipania kuziba pengo kuhusu changamoto zinazohusu usawa wa ujumbe kwa kuzingatia maumbo, mtindo na toni katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika mahakama hasa iwapo wakalimani wenyewe hawana ujuzi au mafunzo maalumu kuhusu tafsiri na ukalimani.

Kwa mujibu wa Kiguru (2009), mkalimani ana mamlaka makubwa katika kufanikisha mawasiliano na maamuzi ya kesi katika mahakama. Hii ni kwa sababu hakimu na maafisa wengine katika mahakama pamoja na mshtakiwa humtegemea mkalimani kuhawilisha ujumbe walioukusudia katika diskosi zao kwa ufasaha. Mkalimani basi hana budi kuwa na umilisi wa lugha na utamaduni wa jamiilugha mbili zinazohusika. Mkalimani anafaa kuelewa msamiati,

rejista, utamaduni na mitindo ya LC na LL. Hakimu hutegemea maelezo anayoyarekodi katika daftari lake kufuatia anayoyasikia kutoka kwa mkalimani wa diskosi za wahusika wa kesi ili kufanya maamuzi yake kuhusu kesi husika. Kiguru alieleza mamlaka ya wakalimani katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika mahakama na athari yao katika maamuzi ya kesi husika ilhali katika uchunguzi huu suala kuu ni kuchunguza changamoto zinazohusu vipengele vya lugha ambavyo wakalimani wanafaa kuvizingatia ili kufikia usawa wa matini ya LC katika matini ya LL.

Newmark (1988) anaeleza kuwa tafsiri ni jaribio la kuhawilisha ujumbe ule ule ulioandikwa katika lugha moja kwa lugha nyingine. Anaeleza kuwa ni jaribio kwa sababu si mara zote mtafsiri anaweza kufanikiwa kulandanisha ujumbe wa LC na LL. Maelezo ya Newmark yana udhaifu kwani hakuzingatia vipengele muhimu katika tafsiri kama vile toni ya mawasilisho ya kazi husika, umbo la kazi yenyewe na mtindo wa kazi husika ili kufanikisha mawasilisho ya ujumbe. Utafiti huu umebainisha changamoto zinazowakumba wakalimani katika shughuli yao wakizingatia vipengele vya ujumbe, maumbo, mitindo na toni ya LC na LL.

Wataalamu wa taaluma ya isimu na tafsiri Olsen na wengine (2009) wakiwanukuu Hale na Gibson walidai kuwa tafsiri ni shughuli iliyojaa dosari katika ulimwengu wenye dosari. Walieleza kuwa dosari hizi zinatokana na ukosefu wa visawe vya vipengele katika lugha mbili husika na namna tofauti za uhawilishaji wa diskosi kutoka mhusika mmoja hadi mwingine. Hivyo basi, kwa kiasi kikubwa, wakalimani na watafsiri hukumbwa na changamoto za kutimiza usawa wa ujumbe, maumbo, mitindo na toni. Hivyo basi, ukalimani wao huathiri matokeo ya ujumbe wa diskosi za wahusika. Utafiti huu umechunguza changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika mahakama ili kubaini iwapo ni kweli

kuwa kuna ukosefu wa usawa wa vipengele hivyo na ni kipi kinachosababisha ukosefu huo wa usawa.

### 2.4.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Usawa wa Maumbo Katika Ukalimani wa Diskosi Katika Mahakama

Sierocka (2014) anafafanua jinsi utamaduni unavyoathiri tafsiri ya matini ya kisheria na jinsi watafsiri wanavyotumia mbinu mbalimbali ili kupata tafsiri iliyo na usawa wa vipengele vyote vya lugha. Alieleza kuwa watafsiri hutumia kamusi kupata kisawe cha maumbo mbalimbali na ambapo hakuna msamiati mwafaka, mbinu ya maelezo ya msamiati husika hutumika katika lugha pokezi ili kufikia usawa hasa katika matini ya kisheria iliyotafsiriwa kutoka lugha moja hadi nyingine. Sierocka alichunguza tafsiri ya matini andishi ya kisheria. Hii ni kwa sababu watafsiri wa matini andishi wana nafasi ya kurejelea kamusi ili kupata kisawe kinachofaa kiashiriwa katika LL tofauti na wakalimani wanaokalimani ujumbe papo kwa papo. Utafiti huu umeshughulikia ukalimani wa diskosi ambazo zinatokea papo kwa papo katika uendeshaji wa kesi katika mahakama. Utafiti huu umechunguza changamoto za usawa unaohusu vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi katika uendeshaji wa kesi mbalimbali katika mahakama. Katika hali hii, wakalimani walikuwa hawana nafasi ya kurejelea kamusi au kuuliza anachokusudia msemaji na mkalimani alitarajiwa kutumia ujuzi wake wa lugha mbili husika kuteua kisawe mwafaka.

Hatman na Munday (2004) wanaeleza kuwa dhana ya tafsiri inahusu vipengele vya lugha na maumbo ya matini husika. Tatizo linalotokea ni kuhusu ni vipengele vipi vya lugha vinavyostahili kuzingatiwa. Wanauliza iwapo mtafsiri azingatie leksimu, semantiki au umbo la matini husika. Wanamalizia kusema kuwa tafsiri inafaa kufanyika kwa kutegemea matendokauli ya matini husika kuhusiana na maneno, virai, vishazi na sentensi. Hii inamaanisha kuwa katika

ukalimani sharti mkalimani azingatie maumbo ya matini na maana ya leksimu, virai, vishazi na sentensi pamoja na muktadha wa matini husika.

Bucholtz (1995) na Stolze (2013) wanaeleza kuhusu tofauti za kimaumbo baina ya MC na ML. Walieleza kuwa karani wa mahakama anaandika ripoti kwa LL ambapo mabadiliko ya kiothografia, kisemantiki na kipragmatiki hutokea. Hali hii huweza kuathiri hukumu ya washauri wa hakimu na huenda wakamnyima mhusika haki anayostahili. Katika utafiti huu uchunguzi umefanywa kubaini changamoto za usawa wa vipengele vya lugha ya MC na ML katika ukalimani wa diskosi za wahusika zinavyotokea katika mahakama.

### 2.4.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Usawa wa Mtindo Katika Ukalimani wa Diskosi Katika Mahakama

Utafiti wa Namakula (2013) ulibainisha changamoto zinazohusu ukalimani wa diskosi za wahusika katika mahakama ya kimataifa, Uganda. Alieleza kuwa mkalimani alipokalimani diskosi ya mhusika akizingatia usawa wa leksimu katika LP, alikemewa na hakimu kwa kutumia lugha chafu na akashauriwa na hakimu atumie tasfida. Ikiwa mkalimani anafaa kutumia tasfida katika ukalimani wake, ujumbe huenda ukapotea na hivyo mhusika kukosa kupata haki aliyoitarajia kwa kukosa kueleweka. Hii ndiyo sababu utafiti huu umechunguza changamoto zinazohusu usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani. Vipengele ambavyo vimetafitiwa ni pamoja na ujumbe, maumbo, mtindo na toni ya MC na ukalimani wake katika ML.

Stolze (2013) katika uchunguzi wake aligundua kuwa tafsiri ya kisheria kutoka lugha ya Kilatini hadi lugha za Ulaya huwa na ugumu wa kupata tafsiri inayolandana. Alibainisha kuwa kila lugha huwa na miundo, mitindo, toni na semiotiki za kipekee kutokana na utamaduni wake na hivyo makala yote ya kisheria yaliyotafsiriwa hufaa kufuata vigezo hivi. Hii humaanisha kuwa mtafsiri

anastahili kuelewa vyema lugha na tamaduni za lugha ya MC na ML. Katika tafsiri, mtafsiri ana muda wa kufanya uchunguzi wa kutosha kwa sababu anatafsiri matini andishi wala si mazungumzo ya papo kwa papo. Stolze (2013) alichunguza tafsiri ya makala ya kisheria yaliyoandikwa. Kwa upande mwingine, utafiti huu umechunguza changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika mbalimbali katika uendeshaji wa kesi katika mahakama.

Zambrano-Paff (2011) na Janigova (2011) walieleza kuwa tafsiri ya matini ya kisheria inafaa kuzingatia kikamilifu usawa kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha nyinginezo kwa kuzingatia nadharia ya usawa unaobadilika pamaoja na nadharia ya matendo kauli. Katika uchunguzi wao walitumia data iliyotokana na matini ya uamuzi wa jaji kuhusu kesi za talaka. Walichunguza iwapo kulikuwa na athari yoyote ya ukalimani ya msamiati unaotumiwa na mhusika kati ya lugha mbili husika uliosababisha matokeo ya maamuzi ya jaji. Wao walishughulikia maamuzi ya jaji yanavyoathiriwa na uteuzi wa msamiati wa wahusika wa kesi na namna mkalimani alikalimani msamiati huo. Katika utafiti huu, mtafiti ameshughulikia changamoto za usawa wa vipengele vya lugha mbili husika (ujumbe, maumbo, mitindo na toni) katika ukalimani wa diskosi za wahusika kama zilivyotokea katika uendeshaji wa kesi katika mahakama.

Ayuk (2015)akihutubia washiriki wa kongamano katika Chuo cha Buea anaeleza kuwa usawa katika ukalimani kuhusu taaluma ya kisheria inadai kuwepo kwa mawasiliano kuhusu ujumbe wa matini asilia pamoja na mbinu zote za lugha husika kama vile uradidi, mianzo kimakosa na makosa yote katika mazungumzo. Zaidi ya hayo, anadai kuwepo kwa uaminifu katika mitindo, toni, na rejista hadi kiasi cha kuiga elementi hizi za matini chanzi katika LL. Katika utafiti huu, mtafiti anachunguza diskosi za wahusika ili kubainisha changamoto ambazo zinamkumba

mkalimani anapotafuta uaminifu huu katika matini ya LL katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika kesi zinazoendeshwa katika mahakama.

### 2.4.4 Yaliyosemwa Kuhusu Usawa wa Ukalimani wa Toni Katika Diskosi Katika Mahakama

Armstrong (2005) anaeleza kuwa ni vigumu kulandanisha MC na ML kwani LC na LL huwa na misamiati, maumbo na mitindo tofauti kutokana na utamaduni wao tofauti. Pia, ni vigumu kukalimani toni ya mhusika kwa sababu namna ya kuwasilisha hisia ni tofauti baina ya jamii-tumizi-lugha tofauti. Mkalimani basi atakumbwa na changamoto tele katika ukalimani wa matini yanayohusu lugha mbili zenye utamaduni tofauti kwani atahitajika kuzingatia mwonoulimwengu wa jamii-lugha husika. Maoni haya yalichangia katika kuelekeza utafiti huu kuwa mkalimani basi angekumbwa na changamoto za usawa wa vipengele vya lugha husika katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi alipokalimani diskosi hizo aidha kutoka Kiswahili hadi Kiingereza au Kiingereza hadi Kiswahili kwani hizi ni lugha mbili zenye tamaduni na toni tofauti.

Morris (1995)anafafanua kuwa kuna masuala na mashaka ya kiisimu yanayowakumba watafsiri wa taaluma ya kisheria katika tafsiri ya lugha ya kisheria. Hii ni kwa sababu wakalimani wanadhibitiwa na taaluma yao kutafsiri matini ya wahusika bila kuzingatia utamaduni wala si mwonoulimwengu wa wahusika. Hivyo basi, wakalimani wanatumika kama 'vyombo' vya kusafirisha ujumbe kutoka LC hadi LL. Mkalimani hana idhini ya kufasili kivyake matini ya wahusika kwani anachukuliwa kuwa mashine au 'chombo' kisicho na hisia za kibinadamu. Akifanya ukalimani akitumia maoni na uelewa wake binafsi, inasemekana kuwa anatia maneno kinywani mwa msemaji. Maoni haya ya Morris yalizingatiwa katika utafiti huu ili kuelekeza

katika kuchunguza changamoto zinazohusu usawa wa vipengele vya lugha hasa toni,katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji kesi katika mahakama ya Kericho.

### 2.5Wazo la Utafiti

Utafiti huu umechunguza changamoto zinazohusu usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika kesi mbalimbali. Mtafiti amekusanya data kutoka mahakama ya Kericho, Kenya. Ametumia mbinu ya kuhudhuria na kushiriki vikao vya uendeshaji wa kesi mbalimbali katika mahakamahiyo. Mtafiti ametathmini changamoto za usawa wa vipengele vya lugha ambavyo ni ujumbe, maumbo, mitindo na toni kama vilivyojitokeza katika LC na LL ili kubainisha changamoto zilizowakumba wakalimani katika ukalimani wa vipengele hivyo vya lugha. Diskosi husika ni zile ambazo zimekalimaniwa kutoka lugha ya Kiswahili hadi Kiingereza au kutoka Kiingereza hadi Kiswahili.

Diskosi zilizokalimaniwa zilichunguzwa katika viwango vya namna zilivyoweza kufikia usawa wa vipengele vya ujumbe, maumbo, mitindo na toni ya MC na LC hadi ML na LL. Wazo hili lilitokana na malalamishi ya Naibu wa Rais katika kesi ya ICC kwamba wakalimani wa kutoka Kongo hawakukalimani diskosi za wahusika kulingana na matumizi ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Pia, wazo hili lilitokana na mawazo ya wanaismu kuwa tafsiri na kwa hivyo ukalimani ni shughuli iliyo na utata na dosari nyingi mno kwa kuwa hakuna lugha mbili ambazo zina msamiati unaolandana moja kwa mwingine. Hii ni kwa sababu ya kuwepo kwa historia, utamaduni, mazingira na miundo tofauti ya lugha mbili husika katika tafsiri na ukalimani.

### 2.6 Utambuzi wa Pengo la Utafiti

Taaluma ya tafsiri imeanza kushughulikiwa siku za hivi karibuni ingawa ukalimani umekuwapo tangu binadamu kutoka jamiilugha tofautu walipoanza kutangamana katika shughuli zao za kila siku. Hivyo basi kuna mengi ambayo bado hayajatafitiwa ili kudhihirishwa katika taaluma hii.

Katika uwanja wa sheria lugha na msamiati unaotumiwa ni wa kipekee. Majaji na mawakili wanatumia msamiati wa kawaida kwa namna ambayo inaupa msamiati huo maana inayoeleweka kwa wanasheria wenyewe. Lugha hii ya kipekee huwa ni vigumu kwa wahusika wasio wasomi wa taaluma ya kisheria kuuelewa ujumbe uliokusudiwa.Itakuwa bora na nafuu kwa watafiti wa lugha na wanaisimujamii kuchunguza matumizi ya lugha na msamiati katika muktadha wa sheria ili kuutafsiri ili tafsiri hiyo kuwafaa wakalimani wa mahakama mbalimbali katika taifa hili na hata mataifa ambayo hutumia lugha ya Kiingereza na Kiswahili katika uendeshaji wa shughuli za kesi katika mahakama zao.

Kutokana na kazi za wataalamu wa taaluma ya tafsiriwaliotajwa katika sehemuhii imeonekana kwamba ukalimani wa diskosi katika mahakama bado ni suala lenye mapengo na changamoto tele ambazo zinafaa kushughulikiwa. Hakuna mtaalamu mmoja ambaye anaweza kumaliza kuziba mapengo na kuondoa utata uliopo katika taaluma hii ya kisheria. Utafiti huu umechunguza suala la changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji kesi katika mahakama. Uchunguzi huu umetathmini iwapo wahusika waliohitaji wakalimani walipata ukalimani wa diskosi zao ipasavyo inavyopendekezwa katika Katiba ya Kenya (2010).

## 2.7 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia maelezo kuhusu historia ya ukalimani na tafsiri ili kutofautisha dhana hizi mbili ambazo zina ukuruba wa karibu mno ili kuondoa utata uliopo. Nadharia ya usawa imeshughulikiwa kikamilifu ili kuonyesha mawazo na mihimili muhimu inayofaa kufuatwa katika uchambuzi wa suala la usawa wa MC na ML kwa kuzingatia vipengele vya lugha katika LC na LL. Zaidi ya hayo, sura hii imechunguza maoni ya wasomi wengine kuhusu mada ya usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa MC na ML. Pia, maelezo yametolewa

kuhusu utambuzi wa pengo hili la utafiti na mpangilio wa wazo la utafiti ili kufikia matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inahusu muundo wa utafiti, mbinu zilizotumiwa kukusanya data, mahali ambapo data ilikusanywa, jumuiya ya utafiti, usampulishaji wa data,vibadala katika utafiti, vifaa vilivyotumiwa kukusanyia data, masuala ya kimaadili yaliyozingatiwa, uhifadhi wa data na namna data husika ilivyochanganuliwa. Kwa jumla, sehemu hii imebainisha namna mtafiti alikusanya data na namna ya uchanganuzi wa data aliyoikusanya kwa kuzingatia, suala la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti.

## 3.1Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa kistahilifu. Mbinu ya uchunguzi shirikishi ilitumika katika kukusanya data ghafi husika. Mtafiti alihudhuria vikao kadhaa vya uendeshaji kesi kwa muda wa miezi miwili. Diskosi za wahusika wa kesi hizo, wakiwemo mawakili, makarani, washtakiwa, washtaki na mashahidi, zilikusanywa kwa kunasa diskosi hizo kwenye kinasasauti na kurejelea rekodi hizo kwa kusikiliza tena yaliyojiri katika mahakama. Lugha rasmi za Kiswahili na Kiingereza zilitumiwa katika mawasiliano ya uendeshaji kesi zilizoteuliwa. Ambapo muhusika aliongea Kiswahili, mawakili na jaji waliwasilisha diskosi zao kwa Kiswahili kwani walikalimani wenyewe diskosi zao kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili na mhusika huyo kuwasilisha diskosi yake kwa lugha ya Kiswahili. Sampuli nasibu horomo na sampuli makusudi zilitumiwa katika kuteua diskosi za kesi sita ambazo zilichanganuliwa ili kubaini changamoto zinazohusu usawa wa vipengele vya ujumbe, maumbo, mtindo na toni baina ya MC na ML.

Mbali na kunakili diskosi za wahusika wa kesi katika uendeshaji kesi katika mahakama, fomu za hojaji zilitumiwa kukusanya data kuhusu changamoto za usawa wa ukalimani wa vipengele vya

lugha. Wakalimani ambao pia ni makarani walijaza fomu hizo na data hizo zimechanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya mtafiti katika utafiti huu. Haja kuu ya kufanya hivyo ni kutaka kuchunguza hali ya wakalimani kimasomo, changamoto zao katika shughuli nzima ya ukalimani na mbinu ambazo wao huzitumia ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili ili kufikia usawa unaotarajiwa.

Mtafiti ametumia mbinu ya maelezo pekee katika uwasilishaji wa matokeo ya utafiti wake kwa sababu utafiti huu ni wa kistahilifu. Uchanganuzi wa data za diskosi na hojaji umefanywa kwa kutolewa maelezo ili kubainisha vipengele vya lugha vilivyokuwa vinachunguzwa.

### 3.2.1 Mahali pa Kukusanya Data

Utafiti huu umefanywa katika mahakama ya Hakimu Mkuu wa Kericho, Kaunti ya Kericho, Kenya. Kaunti ya Kericho ina eneo la kilomita elfu mbili mia moja na kumi na moja mraba (2454.5km2) au maili mia tisa arobaini na nane mraba (948ml mraba). Kulingana na sensa ya idadi ya watu nchini Kenya mwaka wa 2009, idadi ya wakazi wa Kaunti ya Kericho ni watu 752396. Nadhani kwamba idadi hii imeongezeka kwa kiasi cha angaa asilimia kumi na tano kipindi hiki cha miaka saba tangu watu wahesabiwe nchini.

Kaunti hii inapakana na Kaunti ya Nyamira (wanajamii ni Wakisii), Kaunti ya Bomet (wanajamii ni Wakalenjin), Kaunti ya Nakuru (wanajamii wengi ni Wakalenjin, Wakikuyu na Wakisii), Kaunti ya Kisumu (wanajamii wengi ni Waluo) na Kaunti ya Nandi (wanajamii wengi ni Wanandi, Waluhya na Waluo). Kaunti ya Kericho ina Kaunti ndogo sita ambazo ni Kipkelion Mashariki, Kipkelion Magharibi, Soin-Sigowet, Belgut, Ainamoi na Buret. Wenyeji wa kaunti hii ni Wakipsigis, Waluo katika eneo la Sondu na Forternan katika Kaunti Ndogo ya Soin-Sigowet, Wakikuyu katika eneo la Londian Kaunti Ndogo ya Kipkelion Magharibi na Wakisii katika eneo la Kipkelion Kaunti Ndogo ya Kipkelion Mashariki.

Shughuli za kiuchumi katika kaunti hii ni kilimo cha majani chai na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na nyama. Mauzo ya mazao kutoka shambani kama vile, mahindi, mboga na matunda pia hushuhudiwa katika kaunti hii. Pia, kuna maduka ya kuuza bidhaa mbalimbali zikiwemo mavazi na vyakula hasa katika maduka makuu ya kujihudumia ya Uchumi, Nakumatt, Stagematt, Tusky's na Ukwala. Baadhi ya bidhaa kama vile mboga na matunda huletwa kutoka Kisii, Nyamira na hata Ukambani.

Hata hivyo, kwa sababu ya kuwepo kwa mji mkuu wa Kericho katika kaunti hii, wakazi wa mjini hutoka jamii mbalimbali nchini na hata nje ya nchi ya Kenya.Wakipsigis ndio wanaochukuliwa kuwa wenyeji wa eneo hili la Bonde la Ufa nchini Kenya ila wanajamii wengine wamehamia huku ili kufanya kazi katika Kampuni za Kimataifakatika kaunti hii. Kampuni hizo za kimataifa ni pamoja na *UniliverTea*,*BrookeBond*,*FinlayTea* na *GeorgeWilliamsonTea*. Kutokana na hali hii Kaunti ya Kericho ina wanajamii wenye lugha na utamaduni tofauti tofauti. Barabara kuu ya kuunganisha Kenya na Uganda na pia Kenya na Tanzania hupita katikati ya Mji wa Kericho ambapo mahakama husika imejengwa.

Kaunti ya Kericho ina mahakama kuu moja pekee. Mahakama hii hushughulikia kila aina ya kesi ambayo huripotiwa huko na mkazi yeyote kutoka kaunti nzima. Mahakama ya Kericho ina vyumba vingi ambavyo huendesha shughuli zao wakati mmoja chini ya uongozi wa hakimu wakuu watatu. Mahakama ya Kericho inahudumia wakazi wa kaunti nzima.Pia, washukiwa ambao watakamatwa wakiwa safarini kuelekea au kutoka Uganda au Tanzania hushtakiwa katika mahakama hii sawa na wakazi wa kaunti hii. Vikao vya kesi ni vingi mno kwa sababu kaunti hii hufumbata eneo kubwa la kijiografia.

**3.2.2 Jumuiya ya Utafiti**

Mahakama ya Kericho inahudumia wahusika wa kesi kutoka jamii mbalimbali za Kenya kwa sababu Mji wa Kericho na vitongoji vyake husheheni wafanyakazi wa kampuni za kimataifa na asasi za kiserikali ambazo waajiriwa wake hutoka jamii zote zaidi ya arobaini na mbili (42) za Kenya. Lugha ya Kiingereza na Kiswahili basi hutumiwa kama linguafranka ingawa kuna repetwaa ya lugha nyinginezo za kimaeneo. Hivyo basi, mara nyingi lugha za Kiswahili na Kiingereza zilitumiwa katika kuwasilisha diskosi za wahusika mbalimbali katika uendeshaji wa kesi sita zilizoteuliwa.

**3.3.1 Usampulishaji**

Mahakama ya Kericho huendesha kesi kadhaakwa wakati mmoja katika vyumba vyake mbalimbali. Wahusika wa diskosi za kesi zilizoteuliwa ni watu wa umri na uana tofauti tofauti na hutoka matabaka na jamii mbalimbali za Kenya na hata nje ya Kenya. Lugha zilizotumiwa kuwasilisha ujumbe katika kesi zilizoteuliwa ni Kiingereza na Kiswahili. Sampuli nasibu horomo na sampuli makusudi zilitumiwa kuteua diskosi ambazo zilikalimaniwa na wakalimani-makarani na majaji kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Diskosi za kesi sita ziliteuliwa kati ya kesi nyingi zilizoshuhudiwa zikiendeshwa katika vikao mbalimbali katika mahakama. Ibainike kuwa mtafiti hakufuatilia vikao vya kesi moja maalumu hadi mwisho wake kwa sababu baadhi ya kesi huenda zikachukua siku nyingi au hata miaka mingi kukamilika. Data zilizoteuliwa zilinakiliwa upya tayari kwa uchanganuzi kuhusu changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa matini baina ya LC na LL.

### 3.3.2 Vibadala Katika Utafiti

Vibadala katika utafiti huu ni shughuli nzima ya uendeshaji wa kesi katika vikao vya kesi, lugha mbili ambazo zimetumiwa katika kuwasilisha diskosi za wahusika wa kesi na wahusika wa kesi mbalimbali.

Vibadiliki huru vilivyotumiwa katika utafiti huu vilihusu;

(i) Usawa wa kipengele cha ujumbe ambao ulijikita katika diskosi zilizotokea katika LC na kukalimaniwa katika LL.

ii) Usawa wa kipengele cha maumbo katika diskosi zilizotokea katika LC na kukalimaniwa katika LL.

iii) Usawa wa kipengele cha mtindo uliotumiwa katika diskosi za lugha chanzi na mtindo huo ulivyokalimaniwa katika diskosi za lugha lengwa.

iv) Usawa wa kipengele cha toni ilivyojitokeza katika diskosi katika lugha chanzi na toni hiyo ilivyokalimaniwa katika diskosi za lugha pokezi.

Kibadiliki kitegemezi kilikuwa ni shughuli nzima ya ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi mbalimbali. Wahusika wa diskosi hizo ni pamoja na hakimu, mawakili, walalamishi, washtakiwa, mashahidi na wakalimani. Wahusika hao walikuwa watu wa umri, jinsia, taaluma, jamii na matabaka tofauti tofauti katika jamii. Lugha zilizochunguzwa ni Kiingereza na Kiswahili.

## 3.4 Vifaa vya Utafiti

Vifaa ambavyo mtafiti alivitumia katika ukusanyaji wa data hiini shajara na kalamu, kinasasautina tarakilishi. Alidhamiria kutumia kamera ya videolakini ilipigwa marufuku katika maeneo ya mahakama. Katika mahakama hakukuwa na video ila tarakilishi ambazo zilitumiwa kuhifadhi ripoti za kesi na siku za kusikilizwa kesi hizo. Kwa hivyo, data za diskosi za kesi zote huhifadhiwa katika madaftari yaliyoandikwa kwa mkono na hakimu na makarani.

**Shajara na kalamu:** Vifaa hivi ndivyo vilivyotumiwa mno na mtafiti katika utafiti huu na vilikuwa tegemeo kubwa katika ukusanyaji wa data hii. Diskosi zote ambazo zilikalimaniwa kutoka MC zilirekodiwa katika shajara maalumu ili kurejelewa baadaye na mtafiti. Zile diskosi zilizoteuliwa kimakusudi zilinakiliwa katika shajara hii na baadaye sita kati yazo zikateuliwa kwa uchanganuzi kuhusiana na mada ya utafiti huu.

**Kinasasauti:** Mtafiti alitumia kinasasauti muda wote wa utafiti wake ila kidatu cha baadhi ya wahusika kilikuwa chini mno. Hali hii ilisababishwa na idadi ndogo ya hadhira katika mahudhurio. Pia, ilitokea kwamba hakimu na mawakili katika mahakama waliongea kwa sauti ya chini. Hata hivyo, diskosi hizo zinasikika zikisikilizwa kwa makini.

**Kipakatalishi:**Kifaa hiki kilitumiwa katika kuhifadhi data ambazo ziliteuliwa kwa uchanganuzi ili kuafiki malengo ya utafiti huu. Kifaa hiki pia kilitumiwa kupigia chapa kazi nzima kuhusu utafiti huu.

## 3.5 Utaratibu wa Kukusanya Data

Mtafiti aliandaa hojaji ambazo aliwaomba wakalimani katika vyumba mbalimbali vya uendeshaji kesi katika mahakama ya Kericho kujaza kwa makini na kumrejeshea baada ya juma moja. Mtafiti pamoja na msaidizi wake walihudhuria vikao vya uendeshaji kesi kadhaa na kunasa diskosi za wahusika wa kesi mbalimbali zilizokalimaniwa kutoka LC hadi LL. Haja ya utafiti

huu haikuwa kuandama uendeshaji wa kesi hadi kutamatishwa kwake balidiskosi zilizokalimaniwa na zilizosheheni vipengele vya lugha ambavyo vilikuwa vinachunguzwa katika utafiti ndizo zilizoteuliwa.Baada ya kupata data ya kutosha mtafiti aliteua diskosi za vikao vya kesi sita ambazo alitambua zingefaa katika uchunguzi wake na kuzinakili upya kwa ajili ya uchanganuzi kwa kuzingatia maswali na malengo ya utafiti huu.

### 3.6 Uchanganuzi wa Data

Mbinu stahilifu ya uchanganuzi ilitumiwa ili kufafanua data zilizokusanywa katika utafiti huu. Diskosi za wahusika katika vikao vya uendeshaji wa kesi sita ziliteuliwa na kurekodiwa upya na kupewa kodi A hadi F. Mada na maelezo kuhusu wahusika wa kesi yaliandikwa kwa muhtasari. Diskosi za wahusika katika vikao vya kesi sita zilizoteuliwa (data asilia au data ghafi) baina ya diskosi za vikao vya kesi nyingi zilizoshuhudiwa na zilizonakiliwa zilichanganuliwa.

Diskosi zote sita za wahusika zilizofanyiwa ukalimani zilinakiliwa kwa muhtasari kama zilivyotokea. Maelezo yalitolewa kuhusu diskosi zilizokalimaniwa na kuonyesha changamoto zinazohusu usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi zilizotokea katika uendeshaji wa kesi katika mahakama. Mwishowe, uchanganuzi na ufafanuzi pamoja na mahitimisho yametolewa kwa kurejelea diskosi hizo za wahusika katika vikao vya uendeshaji wa kesi zote zilizoteuliwa, kurekodiwa upya na kuchanganuliwa.

Kwa kuzingatia nadharia ya usawa, vipengele vya lugha vilivyojitokeza katika uchanganuzi kuhusu changamoto zinazohusu usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili au kutoka Kiswahili hadi Kiingereza vilidondolewa. Mtafiti ameshughulikia suala la utafiti na malengo ya utafiti katika uchanganuzi huu. Mtafiti amepanga sehemu ya uchanganuzi katika mada ndogo ndogo ifuatavyo: kipengele

cha ujumbe, maumbo, mtindo na toni na wakalimani walivyobuni mbinu za kukalimani vipengele husika kutoka MC hadi ML.

Mihimili muhimu katika nadharia ya usawa iliyotumiwa katika uchanganuzi wa data hizi ni ile inayohusu ujumbe, maumbo, mtindo na toni kutegemea utamaduni unaohusu lugha mbili husika.

Nadharia ya usawa inabainisha kuwa mhimili waujumbe ni kipengele muhimu ambacho kinafaa kuzingatiwa katika ukalimani wa diskosi ya msemaji. Ujumbe unaweza kuwa wa kisemantiki na kipragmatiki kutokana na msamiati uliotumika kutegemea kiwango cha lugha ya msemaji. Mkalimani basi anafaa kuelewa ujumbe huo na kuukalimani kisemantiki na kipragmatiki katika LP. Katika uchanganuzi wa data hizi, mtafiti amebainisha ujumbe uliokusudiwa kwa kuzingatia muktadha wa matumizi, utamaduni wa wahusika pamoja na umilisi wa lugha wa mkalimani husika.

Mhimili wa usawa wa kipengele cha maumbo, kulingana na nadharia ya usawa, huathiri ujumbe uliokusudiwa katika MC kutegemea jinsi maumbo yalivyokalimaniwa katika ML. Maumbo yanahusu mofimu au leksimu, virai, vishazi na muundo wa kisintaksia katika diskosi za wahusika. Usawa wa kimaumbo huzingatiwa katika ukalimani wa matini katika umbo chasila. Hivyo basi, msamiati wa LC unalandanishwa na msamiati wa LL ili kufaa katika ML. Hata hivyo, huenda ikawa vigumu kupata tafsiri inayolandana ikiwa matini inayotafsiriwa inahusu tamaduni mbili tofauti. Hii ni kwa sababu maumbo ya lugha hutofautiana na hivyo kuna pengo la kimaumbo baina ya lugha mbili husika. Koller (1979) anazidi kueleza kuwa iwapo wakalimani wawili watakalimani matini moja, si rahisi tafsiri zao zilandane katika kila kipengele cha lugha kwa sababu wakalimani hao wana mitazamoulimwengu tofauti ingawa wanazungumza lugha moja. Usawa wa matini katika mawasiliano rasmi kama vile mahakama, hutegemea mfumo

mzima wa lugha ya jamii husika (Langue) ambao hukuza usawa wa matini. Mhimili huu wa nadharia hii ya usawa hutafuta maana zaidi ya neno lilivyo katika matumizi yake ya kawaida. Huamini kuwa maana ya neno hutokana na mazingira ambamo limetumika na maana ya maneno ambayo yanalizunguka neno husika. Mtafiti amechunguza ukalimani wa maumbo katika diskosi husika ili kubainisha iwapo ujumbe uliokusudiwa uliwasilishwa kwa kuzingatia maumbo ya LC na LL.

Isitoshe, mhimili wa kipengele cha mtindo wa lugha uliotumika ni muhimu na mara nyingi hutegemea muktadha wa diskosi. Mtindo wa lugha katika MC huwa muhimu katika kuwasilisha ujumbe na iwapo mkalimani hazingatii mtindo huo na kuukalimani ipasavyo, huenda ujumbe wa mhusika ukaathirika. Hivyo basi, mtindo wa lugha katika MC hufaa kutafutiwa visawe mwafaka katika LP. Mitindo ya lugha inayozingatiwa hapa ni tashbiha, jazanda, methali, istiara, misemo na tasfida katika MC na visawe vyake au inavyofasiriwa katika ML. Mtafiti basi amechunguza na kubainisha namna ujumbe ulisawasishwa au kuwa tofauti katika ukalimani wa tamathali hizi za lugha ambazo zilitumiwa katika diskosi husika.

Mhimili wa kipengele cha toni pia ni muhimu katika utafiti huu. Fawcett (2003) akimnukuu Koller (1979) anabainisha kuwa kipengele cha toni ya kihisia ya msemaji ni muhimu na inafaa kuzingatiwa katika tafsiri ya matini ingawa haina maumbo maalum ambayo yatajitokeza wazi. Toni huhusiana na uhalisia au mandhari ya matumizi na hutegemea hali ya msemaji. Mkalimani anafaa kuwa mwangalifu ili kutambua hisia hizo katika uteuzi wa msamiati au kidatu na kiimbo cha msemaji anapowasilisha ujumbe wake. Hivyo basi, mtafiti amezingatia msamiati, kidatu na kiimbo cha msemaji ili kubainisha toni ya msemaji katika diskosi husika.

Mtafiti katika uchunguzi wake kuhusu usawa wa ujumbe na toni amezingatia vipengele vingine muhimu katika ukalimani kulingana na Koller (1979) ambavyo nipamoja na utamaduni unaohusu lugha husika na mandhari au mazingira ya matukio ambayo yanatafsiriwa.

### 3.7 Masuala ya Kimaadili

Mtafiti aliandika pendekezo lake la utafiti kama inavyostahili ili kupata shahada ya uzamili kutoka chuo kikuu chochote. Pendekezo lilipokubalika katika Idara ya Isimu, Fasihi na Mawasiliano na kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii katika Chuo Kikuu cha Kabianga, aliomba idhini ya kuanza kukusanya data. Mtafiti alipewa kibali kutoka Chuo Kikuu cha Kabianga ili kuanza utafiti wake baada ya kupita mitihani ya masomo yanayofundishwa kwa ajili ya kuhitimu shahada ya uzamili na kuandika pendekezo lake kwa njia mwafaka. Mtafiti pia alituma maombi ya kibali kutoka bodi ya elimu ya juu kutoka Chuo Kikuu cha Kabianga ili kuonyesha kuwa mada ya utafiti wake haikuwa imeshughulikiwa katika chuo chochote kingine. Alipokea kibali hicho kuonyesha kuwa hiyo ni mada yake binafsi na asilia. Mtafiti alituma maombi na kupata kibali cha utafiti kutoka bodi ya inayoshughulikia uwanja wa utafiti, NACOSTI (*NationalCommissionforScience*,*TechnologyandInnovation*).

Mtafiti aliandika barua ya maombi ya mahali pa kufanyia utafiti kwa msimamizi mkuu wa mahakama ya Kericho ili kupewa kibali cha kukusanya data katika mahakama hiyo. Walipotosheka kuwa mtafiti alikuwa na jambo muhimu la kuchunguza, walimkubalia kuanza utafiti wake.

Pia, mtafiti alipewa kibali cha kufanya utafiti kutoka kwa Kamishina wa Polisi Kaunti ya Kericho na Mkurugenzi wa Elimu katika Kaunti ya Kericho alivyoagizwa na bodi ya NACOSTI.

Mtafiti alitii sheria zote za mahakama na aliomba usaidizi kutoka kwa maafisa husika kila alipohitaji. Alikamilisha utafiti wake bila matatizo yoyote.

Diskosi za kesi zilizoteuliwa hazikunakili majina halisi ya wahusika wala kutaja kazi ambayo wahusika wanafanya. Mtafiti hakufuatilia kesi husika mpaka mwisho ili kuonyesha hukumu ambayo ingetolewa kwa sababu baadhi ya kesi huchukua muda mrefu mno. Kesi zilizoteuliwa zilipewa kodi A, B, C, D, E na F.Data na matokeo kutokana na data zilizokusanywa yamewasilishwa kwa maelezo kwa sababu huu ni utafiti stahilifu.

### 3.8Mahitimisho

Sura hii imedhihirisha kuwa muundo wa utafiti huu ni shirikishi na mtindo stahilifu umetumiwa katika kuchanganua data zilizokusanywa.Mahali pa kukusanya data ni mahakama kuu ya Kericho ambapo jumuiya yake inajumuisha watu kutoka maeneo na jamii nyingi nchini Kenya na hata nje ya nchi ya Kenya. Usampulishaji nasibu-horomo umetumiwa na mwishowe usampulishaji makusudi ulitumiwa kuteua data zilizochanganuliwa kwa kuzingatia vibadala vilivyohusu lugha mbili husika na wahusika wa diskosi katika uendeshaji wa kesi zilizoteuliwa. Hata hivyo, hakimu, viongozi wa mashtaka na wakalimani hawakukalimani diskosi za wahusika kutoka lugha ya Kiswahili hadi Kiingereza kwa sababu ilichukuliwa kuwa wahusika wote walielewa lugha ya Kiswahili. Vifaa vya utafiti vilivyotumiwa ni kinasasauti na shajara. Kinyume na matarajiao ya awali, kamera ya video haikuruhusiwa katika mahakama kama kifaa cha utafiti. Hivyo basi, hisia na viziada lugha vya wahusika ambavyo vingerejelewa na mtafiti katika kubainisha toni za wahusika wa diskosi hizo havikupatikana ila kwa kutegemea aliyoyaona mtafiti na yaliyojitokeza katika sauti za wahusika wa diskosi wakati wa mahudhurio ya vikao vya uendeshaji kesi zilizorekodiwa katika kinasasauti. Masuala ya kimaadili katika utaratibu wa kukusanya data na uchanganuzi wa data hizo ulifuatwa kikamilifu.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA DATA

## 4.0 Utangulizi

Sura hii imebainisha matokeo ya utafiti uliotokana na data zilizokusanywa kutoka mahakama ya Kericho. Sura hii imeshughulikia sehemu mbalimbali zikiwemo matokeo ya hojaji kwa wakalimani, sababu za kuteua data za kesi husika na matokeo ya uchanganuzi wa data hizo kutegemea vipengele vya lugha vilivyochunguzwa. Kipengele cha ujumbe kimegawanywa katika sehemu zifuatazo; ujumbe uliokalimaniwa vilivyo, ujumbe uliokalimaniwa visivyo, ujumbe uliokosa kukalimaniwa, ujumbe uliochopekwa na ujumbe uliodondoshwa. Kipengele cha maumbo kimegawanywa katika maumbo ya leksimu kimofolojia, maumbo ya virai na vishazi na maumbo ya kisintaksia. Kipengele cha mtindo nacho kimeshughulikia tamathali ya tasfida, misemo na tashhisi. Aghalabu, kipengele cha toni kimesheheni toni iliyokalimaniwa vilivyo na toni iliyokosa kukalimaniwa vilivyo. Mwishowe, sura hii imechanganua majibu kwa maswali yaliyoelekeza utafiti huu.

### 4.1.1 Matokeo ya Hojaji kwa Wakalimani

Mtafiti aliwakabidhi hojaji wakalimani sita na wote walijibu maswali na kurejesha hojaji hizo. Hojaji sita zilizokabidhiwa wakalimani katika utafiti huu zilikusanywa na kuchunguzwa ili kubaini viwango vya masomo vya wakalimani hao, changamoto zao katika ukalimani wa vipengele vya lugha husika na mbinu bunifu walizozitumia ili kuwasilisha ujumbe uliotokana na matini chanzi licha ya kukumbwa na changamoto hizo zinazohusu usawa wa vipengele vya lugha husika.

Matokeo ya hojaji hizo ni kuwa wakalimani wa diskosi katika uendeshaji wa kesi hizo walikuwa pia makarani katika mahakama ya Kericho. Wote walieleza kuwa hawakuwa na mafunzo yoyote

kuhusu ukalimani na tafsiri kabla ya kuajiriwa kazi ya ukarani katika mahakama. Makarani-wakalimani wamepata ujuzi wao wa ukalimani katika utenda-kazi wao. Uvumbuzi huu ni sawa na wa Odhiambo (2013) kuhusu hali ya wakalimani katika mahakama ndogo za eneo la Nyando.

Watatu kati ya hao wakalimani sita wamepokea mafunzo ya muda mfupi yaliyodhaminiwa na serikali baada ya kuajiriwa na wengine watatu hawakupata mafunzo yoyote kuhusu taaluma ya ukalimani na tafsiri kufikia wakati wa kufanya utafiti huu. Wawili kati ya wakalimani waliojaza hojaji walikuwa na elimu ya shahada ya digrii kutoka chuo kikuu na wanne walikuwa na stashahada kutoka vyuo anuwai vya mafunzo mbalimbali. Imebainika kwamba wakalimani katika diskosi za mahakama wamelazimika kufanya shughuli ya ukalimani kwa sababu wao ni makarani wa mahakama hiyo ingawa hawana elimu kuhusu taaluma ya ukalimani. Maoni yangu ni kwamba wakalimani hao walionekana kutofurahia na kuipenda kazi ya ukalimani. Walionekana kutojiamini kuimudu kazi hii. Wengine hata walisema wazi kuwa lugha ya Kiswahili ni ngumu kwao na hawaipendi. Hali hii inadhihirika katika shughuli yao ya ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi ambapo walitumia maneno yale yale ya Kiingereza na walikosa kukalimani mafungu mazima katika diskosi za mhusika.

Wakalimani hawa walieleza kuwa walikumbwa na changamoto za usawa wa vipengele vya lugha nawalitumia mbinu mbalimbali katika shughuli ya ukalimani ili kufikia usawa ambao ulikubalika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama husika. Walieleza kuwa walitumia mbinu ya ukalimani wa neno kwa neno, ukalimani sisisi, utohozi, na ukopaji. Wakati mwingine walitoa maelezo ya msamiati husika au kuutumia vile ulivyo katika Kiingereza.

Kutokana na hojaji hizi ilibainika kuwa mahakama ya Kericho huhifadhi rekodi za kesi mbalimbali zinazoendeshwa katika mahakama hii katika tarakilishi na madaftari maalum ya hakimu. Rekodi za kesi na majina ya walalamishi na washtakiwa wa kesi huhifadhiwa kwenye

faili mbalimbali zilizoandikwa kwa mkono.  Mahakama hii bado haijafanikiwa kutumia vifaa mamboleo kama vile video na kinasasauti ili kurekodi matukio hasa katika vyumba vya kuendeshea kesi. Hivyo basi, hakimu na mawakili hutegemea diskosi zinazowasilishwa kwa njia ya mdomo na rekodi za kimaandishi za hakimu, mawakili na makarani katika uendeshaji wa kesi. Diskosi hizi hurekodiwa kwa lugha rasmi ya mahakama ambayo ni Kiingereza. Wakalimani wa mahakama hii walidai kuwa walihitaji tarakilishi za kutosha katika uhifadhi wa diskosi za kesi na pia tepurekoda na kamera za video ambazo zinaweza kurejelewa kila inapohitajika. Katika mahakama hii, kesi huendeshwa kwa lugha rasmi ya mahakama ambayo ni Kiingereza, lugha ya Kiswahili (lugha ya taifa) na lugha za mama kulingana na inavyopendekezwa katika kitabu cha kisheria (1997, sura ya 75) na Katiba ya Kenya (2010).Katiba inadai kwamba mhusika yeyote asiyeelewa lugha ya Kiingereza apewe nafasi ya kuchagua lugha ambayo angependa kuitumia kujieleza na apewe haki hiyo pamoja na mkalimani bila malipo. Makarani wa mahakama (wasidizi wa hakimu) walitumiwa kama wakalimani iwapo walielewa lugha ya mama ya wahusika na pia kuwasilisha diskosi hizo zilizotolewa kwa lugha ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili kwa wahusika waliohitaji usaidizi wa mkalimani.

### 4.1.2 Sababu za Kuteua Data za Kesi Hizo

Diskosi za kesi sita zilizoteuliwa zilitokana na matukio ya uhalifu yaliyokuwa yametokea katika eneo la Kaunti ya Kericho na kuendeshwa katika mahakama kuu ya Kericho pekee. Lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili zilitumiwa kuendesha kesi hizo. Diskosi zilizoteuliwa zimesheheni vipengele vya lugha ambavyo vilikuwa msingi wa uchunguzi wa utafiti huu. Diskosi hizo za kesi zilizoteuliwa zimesheheni vipengele vyote vya lugha vinavyochunguzwa katika utafiti huu. Diskosi hizi zina vipengele vya ujumbe, maumbo, mtindo na toni; vipengele ambavyo vimelinganishwa ili kubainisha changamoto kuhusu usawa katika ukalimani wa diskosi

hasa katika uendeshaji wa kesi katika mahakama. Kesi hizo zilipewa kodi A hadi F na kuchanganuliwa kwa kuzingatia vipengele vya ujumbe, maumbo, mtindo na toni ilivyobainishwa katika sehemu ifuatayo.

**4.2 Matokeo ya Uchanganuzi wa Data za Kesi Hizo**

Data iliyokusanywa na kuteuliwa ilichunguzwa kwa kuzingatia masuala mahususi na maswali yaliyoongoza utafiti huu kuhusu changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili. Maswali yaliyozingatiwa yalikuwa:

i) Je, wakalimani katika mahakama waliweza kufikia usawa mahususi wa kipengele cha ujumbe kutoka MC hadi ML katika harakati ya kukalimani diskosi za wahusika wa kesi mbalimbali katika mahakama?

ii) Je, wakalimani walifikiausawa wa kipengele cha maumbo katika ukalimani wao wa diskosi za wahusika wa kesi mbalimbali kutoka LC hadi LL?

iii) Je, wakalimani walifikia usawa wa kipengele cha mtindo katika ukalimani wa diskosi za wahusika kutoka LC hadi LL?

iv) Je, wakalimani walikumbwa na changamoto za usawa wa kipengele cha toni katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi kutoka LC hadi LL?Je, walitumia mbinu zipi bunifu katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi katika mahakama ili kufikia usawa wa kipengele cha toni?

**4.3 Changamoto za Usawa wa Ujumbe Katika Ukalimani wa Diskosi za Wahusika**

Sehemu hii imegawanywa katika mada ndogo ndogo muhimu zikiwemo mada kuhusu dhana ya ujumbe, ujumbe uliokalimaniwa, ujumbe uliokalimaniwa visivyo, ujumbe uliochopekwa na

ujumbe uliodondoshwa katika ukalimani wa diskosi teule. Kipengee hiki cha ujumbe kimechanganuliwa na kubainishwa kwa kuzingatia mhimili muhimu wa nadharia ya usawa. Mhimili huu katika nadharia ya usawa unabainisha kuwa kipengele muhimu ambacho kinafaa kuzingatiwa katika ukalimani ni ujumbe wa msemaji katika diskosi yake. Ujumbe unaweza kuwa wa kisemantiki na kipragmatiki kutokana na msamiati uliotumika kutegemea kiwango cha lugha ya msemaji. Mkalimani basi anafaa kuelewa ujumbe katika LC na kuukalimani kisemantiki na kipragmatiki katika LP.

### 4.3.1 Dhana ya Ujumbe

Kwa mujibu wa TUKI (2000), ujumbe ni 'habari, taarifa au salamu katika matini mahususi.' 'Habari, taarifa au salamu'hizo zinaweza kuwa wazi au fiche kutegemea msuko wa msamiati na muktadha wa matumizi yake kutokana na aina ya matini husika. Ujumbe unaokusudiwa hapa ni ule unaojitokeza katika diskosi za wahusika katika LC na zilizokalimaniwa hadi LL katika uendeshaji wa kesi zilizoteuliwa ili kuchanganuliwa. Ujumbe huo unaweza kuwa wa kipragmatiki (fiche) au kisemantiki (wazi) kutegemea mwonoulimwengu wa mkalimani na umilisi wake wa lugha azitumiazo katika shughuli hiyo ya ukalimani.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa ujumbe ni dhana inayotumika kueleza taarifa ambazo msanii au mtunzi hutoa kwa wasomaji au hadhira yake kama njia ya kuhakikisha kuwa dhamira yake imetimia. Katika utafiti huu, ujumbe uliojitokeza katika LC ulikalimaniwa katika LL huku mkalimani akitarajiwa kuzingatia dhamira ya ujumbe huo katika uendeshaji wa kesi husika. Dhamira ya ujumbe ni muhimu katika kufanikisha ujumbe wenyewe ili wahusika wapate haki au hukumu inayowafaa. Dhamira ya ujumbe hujikita katika kiimbo cha sentensi na uteuzi wa msamiati.

TUKI (2000) inaeleza kuwa ujumbe ni habari, taarifa, agizo au risala. Kulingana na utafiti huu, neno ujumbe linamaanisha wazo kuu linalowasilishwa katika matini ambayo ni diskosi ya mhusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama. Wazo hilo linaweza kuwa la kisemantiki au la kipragmatiki kutegemea muktadha na utamaduni wa mkalimani.

Ujumbe wa kisemantiki ni ujumbe ulio wazi kutokana na maana ya msamiati uliotumiwa. Maana husika hutokana na kamusi ya lugha husika. Kinyume na ujumbe wa kisemantiki, ujumbe wa kipragmatiki hupita mipaka ya maana ya msamiati katika kamusi ya lugha husika. Maana ya msamiati hutegemea muktadha wa matumizi na mtumizi mwenyewe. Kwa vile ujumbe wa msamiati uliotumiwa katika diskosi teule ulikalimaniwa kutoka lugha chanzi hadi lugha pokezi kutegemea umilisi wa lugha ya mkalimani, huenda ujumbe huo ukakosa kulandana katika LC na LL.

**4.3.2 Ujumbe UliokalimaniwaVilivyo Katika Diskosi za Wahusika wa Kesi**

Katika ukalimani wa diskosi za wahusika, ujumbe wa kipragmatiki uliokusudiwa katika MC uliweza kukalimaniwa katika ML ingawa kulikuwa na changamoto tele za usawa wa vipengele vya lugha mbili husika. Ujumbe wa kipragmatiki uliweza kufikiwa kwa sababu wahusika wa kesi walielewa ujumbe uliokusudiwa kabla ya kesi kuanza. Baadhi ya ujumbe uliokalimaniwa ni kama ufuatao:

Katika kesi A, ujumbe ufuatao ulikalimaniwa vyema na kuleta maana iliyokusudiwa na mhusika wa diskosi katika LC:

*Km: without a licence, against the laws of Kenya.*

Mk: bila leseni, kinyume na sheria za Kenya.

*Km: at Nyagacho, Kericho town*

Mk: mkiwa Nyagacho mji wa Kericho

Katika LL ilieleweka kuwa washtakiwa walipatikana mjini Kericho katika mtaa wa Nyagacho wakifanya uhalifu huo kwa sababu hawakuwa na leseni ya kuendesha shughuli waliyokuwa wakiendesha (kucheza kamari).

Katika diskosi za kesi B, ujumbe huu ulikalimaniwa vyema na kuleta usawa wa ujumbe uliokusudiwa;

*Km: You are accused of raping (name). Against the laws of Kenya.*

Mk: Unashtakiwa kwa kumnajisi (jina). Kinyume na sheria za Kenya.

Inaeleweka kuwa mshtakiwa alishtakiwa kwa kumnajisi mtoto huyo wa kike jambo ambalo ni kinyume na sheria za nchi ya Kenya.

Katika diskosi za kesi C, ujumbe ufuatao umekalimaniwa vyema. Katika diskosi hii inaeleweka kuwa mvulana huyo wa umri wa miaka minane alitayarishwa na mamake kuenda shule na mamake kuenda kazini mwake lakini huyo mtoto aliende kusomba mchanga kwa siku kadhaa kutokana na ushawishi wa mshtakiwa. Mamake mlalamishi alipopata ujumbe kutoka shule kuwa mwanawe hakuwa anaenda shule ndipo alipoenda kumtafuta.

*Km: who is a minor of eight years. He was prepared by his mother to go to school*

Mk: ambaye ni mtoto wa miaka minane, aliweza kutayarishwa na mamake ili aende shule.

*Km: then she left for work.*

Mk: na mamake akaenda kazini.

*Km: He was ferrying sand to the roadside,*

Mk: Alikuwa anapeleka mchanga kando ya barabara,

*Km: The complainant was prepared by his mother to go to school,*

Mk: Huyo mlalamishi alitayarishwa na mamake aende shule

*Km: but the said person called him and told him to work for her.*

Mk: wewe ulimwita tena ukamwambia akufanyie kazi

*Mk: as his mother had received information from the school, that he had not been attending school.*

Mk: na mamake alikuwa amepata habari kutoka shuleni, kwamba hakuwa akienda shule.

*Km: that is when she decided to track him*

Mk: ndipo alikuja kumtafuta.

Katika diskosi za kesi D, ujumbe uliokalimaniwa na ulieleweka kuwa mshtakiwa alipatikana na bangi kisha askari wakamtia mbaroni na kumpeleka kwenye kituo cha polisi cha Fort Tenan. Siku hiyo alifikishwa mahakamani na hiyo bangi ilikuwa mbele ya korti kama ushahidi kuwa alipatikana nayo.

*Km: They arrested him and took possession of the recovered bhang,*

Mk: Walikushika na wakachukua hiyo bangi ambayo walikuwa wamekushika nayo,

*Km: and escorted him to Fort Tenan where he was charged with the present charges.*

Mk: Walikushindikisha mpaka kituo cha police cha Fort Tenan na kukushtaki na makosa ambayo yako mbele ya korti hii.

*Km: The cannabis sativa is before court and I wish to produce it as exhibit.*

Mk: Hiyo bangi ambayo ilipatikana iko mbele ya korti na kiongozi wa mashtaka angependa kuitoa kama thibitisho.

Katika diskosi za kesi E, ujumbeuliokalimaniwa vyema ni kuwa mlalamishi alikuwa kazini kwake kulemshtakiwa alipomvamia kwa madai kwamba mlalamishi alikuwa akimsengenya. Mshtakiwa alimkwaruza kisha akamuumiza sehemu ya kushoto ya pua yake.

*Km: The complainant was at her place of work,*

Mk: Mlalamishi alikuwa mahali pake pa kazi,

*KM: when you the accused*

MK: wakati wewe mshtakiwa,

*KM: where she attacked her by scratching her, and injured her on her left side of the nose.*

MK: uliweza kumshambulia kwa kumkwaruza, ulimjeruhi upande wake wa kushoto wa pua.

*Km: She was alleging that the complainant was backbiting her*

MK: Alikuwa analalamika kuwa mlalamishi alikuwa akimsengenya

Katika diskosi za kesi F, ujumbe uliokalimaniwa vyema ni kwamba mshtakiwa aliyekuwa raia wa Tanzania alipatikana nchini Kenya bila kibali cha kumwezesha kuwepo nchini na alikamatwa kwa sababu alikuwa nchini Kenya kinyume cha sheria.

*Km: who was suspected to be of foreign national,*

Mk: kwamba ulishukiwa kuwa wewe si mtu wa Kenya, ni wa nchi ingine,

*Km: the officers approached this person and on interrogation they actually established that he is a Tanzanian national.*

Mk: Maaskari walipokuja na kukuuliza maswali walijua kuwa ulikuwa mwananchi wa Tanzania.

*Km: The officers arrested him and charged him with the present charges.*

Mk: Maafisa walikushika na kukushtaki na mashtaka ambayo yako mbele ya korti.

Ujumbe uliokusudiwa ni kwamba mshtakiwa alipatikana nchini Kenya bila kibali na askari walipomdadisi na kubainika kuwa alikuwa mwananchi wa Tanzania na alikuwa hana kibali cha kuwa nchini Kenya, askari hao walimtia mbaroni.

Ujumbe ulioeleweka ulisaidia kuendesha kesi hizi na ungetegemewa katika kutoa hukumu ingawa sehemu nyinginezo za diskosi hizi zilikalimaniwa visivyo.Ujumbe muhimu ulieleweka ni hiki ndicho kiini cha uendeshaji wa kesi katika mahakama. Ujumbe huu mwafaka uliwasababisha washtakiwa wakubali au wakatae mashtaka hayo yaliyowakabili mbele ya mahakama.

**4.3.3 Ujumbe Uliokalimaniwa Visivyo Katika Diskosi za Wahusika wa Kesi**

Ujumbe ufuatao ulikalimaniwa visivyo na huenda uliathiri mawasiliano katika uelewaji wa mashtaka yaliyowakabili wahusika wa kesi hii.

Diskosi A

> *KM: You have been accused of cheating the publicthat you are playing cards and they will win money.*
>
> MK: Mmeshtakiwa kwa kosa lakucheza 'karate' kwa umma.
>
> Km:*Without a licence against the laws of Kenya.*
>
> Mk: Bila leseni kinyume na sheria za Kenya.

Katika matini hii mkalimani alikosa kukalimani ujumbe wa kuwatapeli watu pesa katika ukalimani wa sentensi ya kwanza. Anautaja mchezo wa 'karata' ambao ni mchezo wa kamarikuwa mchezo wa 'karate' ambao ni mchezo wa wahusika kurushiana makonde na mateke. Ujumbe uliokusudiwa umekanganya kwa kutajwa mchezo wa 'karate' na kadi hamsini na mbili. Zaidi ya hayo, suala la kuwatapeli watu pesa halikujitokeza katika ukalimani badala yake ujumbe ulieleweka ni kuwa washtakiwa walikuwa wakiwaburudisha watu alipokalimani kuwa 'walicheza karate kwa umma'. Basi kwa mtu ambaye si mkazi wa Kericho, ukalimani ulikuwa na maana kwamba 'watu walipigwa mateke na makonde na kunyang'anywa pesa au washtakiwa walikuwa wanawatumbuiza watu ili kupata kiinua mgongo' alipokalimani kuwa walikuwa wakicheza 'karate kwa umma kwa nia ya kupata pesa'. Mkalimani alipoteua msamiati ambao ulikuwa na maana tofauti na msamiati uliotarajiwa, ujumbe uliokusudiwa ulikosa usawa uliotarajiwa katika ukalimani.

Katika diskosi ya kesi hii, kiongozi wa mashtaka anarejelea ‘kadi’ za mchezo wa bahati nasibu unaojulikana kama mchezo wa ‘karata’. Mkalimani anapokalimani mchezo huo wa kadi, anatumia msamiati au leksimu ‘karate’ ambao hauna uhusiano kabisa na neno kadi. Mkalimani alifahamu neno hilo 'karate' kuwa sawa na 'karata' ambalo linakaribiana kimatamshi au ni kitate. Ujumbe wa diskosi hii ulieleweka kwa wahusika wa kesi kwa sababu neno 'karate' linatumika katika muktadha wa matumizi ya lugha ya kila siku ya wakazi wa mji wa Kericho. Kwa wakazi wengi wa Kericho, mchezo huu wa bahati nasibu kwa kutumia kadi unaitwa 'karate' wala si 'karata' inavyostahili. Basi, ujumbe wa kipragmatiki ulieleweka kwa wahusika wa kesi wakati huo ingawa baadaye msamiati huu huenda ukazua mtafaruku na kubadili au kuchangia pakubwa uamuzi wa hakimu. Kama washtakiwa wangekataa mashtaka hayo kwa sababu walicheza ‘karata’ wala si ‘karate’, huenda kesi ingeamuliwa visivyo.

Pia katika diskosi ya kesi A,

*Hakimu: What do you say in mitigation?*

Mk: Malilio yako mbele ya korti kabla ya hukumu?

Mkalimani katikadiskosi za kesi hii alikalimani msamiati wa Kiingereza ‘*mitigation’*(ambao una maana ya ‘jambo linaloweza kumfanya hakimu kufikiria kupunguza hukumu yake’) kuwa ‘malilio’. Ukalimani huu huenda ndio sababu baadhi ya washtakiwa walifanya kitendo cha kulia wazi badala ya kujitetea kutokana na matukio ya kesi husika ili jaji aweze kuwa na sababu ya kuwahurumia na kuwasamehe makosa yao au kuwatolea hukumu nyepesi. Ujumbe wa kipragmatiki kulingana na sajili ya mahakama pengine ulieleweka kwa jaji na kiongozi wa mashtaka lakini kwa wahusika walioshtakiwa katika kesi hizo, hali ilikuwa tofauti. Washtakiwa walielewa ujumbe wa kisemantiki pekee. Hii ndio sababu wengi wao walilia na kuomba

msamaha kwa makosa yao ili jaji awahurumie na kuwaachilia huru. Basi haki yao ya kujitetea ili kupata kueleweka vyema ilikosekana kwa sababu ya ukosefu wa usawa wa kipengele cha ujumbe. Hali hii huenda ilizua utata katika uamuzi wa haki.

Zaidi ya hayo, katika kesi A,

*Km: You were asking for money…*

Mk: Hapo mlikuwa mkitafuta pesa…

Mkalimani alikalimani '*askingformoney'* kuwa 'mkitafuta pesa' badala ya 'mliwadai pesa'. Hili linatokea kwa sababu ya ukosefu wa msamiati mwafaka kwani mkalimani husika hana umilisi wa lugha na msamiati maalumu anaostahili kuwa nao katika ukalimani wa diskosi za kesi katika mahakama. Mkalimani huyu hajapokea mafunzo kuhusu ukalimani na alikuwa akikalimani kutokana na ujuzi binafsi alio nao kuhusu lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Ujumbe wa kisemantiki uliojitokeza katika ukalimani huu ni kuwa washtakiwa hawa walikuwa wakisaka pesa kana kwamba walikuwa wamezipoteza au walikuwa wakifanya kazi ili kupata ujira uliowafaa kutokana na kazi waliyoifanya. Ujumbe wa kipragmatiki wa kuwalaghai raia haukujitokeza na hali hii huenda ikasababisha washtakiwa kutolewa hukumu nyepesi.

Isitoshe, katika kesi A, jaji anawaambia washtakiwa kuwa '*Iwillcallyoushortly*…' ambapo mkalimani anakalimani kuwa 'mtaitwa baadaye…' ambapo ujumbe kwamba 'wangeitwa baada ya muda mfupi …' umebadilika na kuwa 'wataitwa baada ya muda usiojulikana kwani neno 'baadaye' laweza kumaamisha baada ya muda mfupi, siku hiyo au hata baada ya siku kadhaa.

Ujumbe pia, unapotea wakati mkalimani anakalimani '*Youhavebeenconvictedonyourownplea'* kuwa 'mmehukumiwa kwa sababu mmeitikia makosa' kana kwamba kukiri makosa ndiko kumesababisha kuhukumiwa kwao wala si kwa sababu kuwa wamepatikana na hatia na

wamekubali kuwa walifanya makosa. Pengine hili ndilo jambo lililowafanya wengi wa washtakiwa kukana mashtaka yaliyowakabili. Inawezekana kwamba hii ndiyo iliyokuwa sababu ya washtakiwa wengine kunyamaza walipoulizwa iwapo walikiri makosa au la. Walifikiri kwamba kukubali mashtaka kulisababisha kushtakiwa kwao na iwapo wangekana au kunyamaza, hakimu angekosa kuwahukumu na pengine kuwaondolea mashtaka. Hawakuelewa kuwa hakimu alitoa hukumu kutokana na mashtaka yaliyowakabili na kwa vile walikubali makosa yao alikuwa radhi kutoa hukumu iliyowafaa.

Katika diskosi ya kesi B,

> *KM: 'In your full senses, against the law. Your penis penetrated the vagina of the said girl who is five years old.'*
>
> MK: 'Kupenda kwako na kinyume na sheria. Uliweza kusababisha sehemu yako ya uume kupenyeza sehemu ya siri ya msichana huyo ambaye ana miaka mitano.'

Mkalimani amekalimani '*inyourfullsenses'* kuwa 'kupenda kwako' badala ya 'ukiwa na akili timamu' kana kwamba amekalimani '*onyouronfreewill'* anapokalimani kuwa 'kwa kupenda kwako au ikiwa ni kupenda kwako kunajisi'. Ukalimani huu umekosa kuonyesha kuwa mshtakiwa alikuwa na 'akili zake timamu' wala hakuongozwa na tamaa zake tu bali na akili yake pia.Mkalimani alifaa kukalimani hiki kirai cha kiongozi wa mashtaka hivi kwamba suala la mshtakiwa kuwa na 'akili yake timamu' na kwa 'hiari yake' alitenda kitendo hicho cha unyama cha kumnajisi mtoto huyo wa umri wa miaka mitano. Katika hukumu za jaji suala la urazini wa akili ya mshtakiwa wa kosa lolote lile ni muhimu kwa sababu walio na akili punguani wanachukuliwa kuwa hawakuelewa uhalifu walioufanya.

Msamiati wa Kiingereza '*penis* or *malegenitals'* umekalimaniwa kuwa 'sehemu yako ya uume' huku '*vagina* or *femalegenitals'*imekalimaniwakuwa 'sehemu ya siri'. Msikilizaji ambaye haelewi kuwa utamaduni wa jamii nyingi za Kiafrika, huwalazimu kutumia tasfida kuficha lugha ya matusi au lugha chafu atachanganyikiwa. Atakosa kuelewa ujumbe uliokusudiwa kwa sababu sehemu za 'siri' hutofautiana kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine. Huenda akaeleweka visivyo kwani katika jamii nyingine za Kiafrika huenda 'sehemu ya uume' ikamaanisha mkono wa kulia. Katika taaluma ya kisheria hasa katika mahakama, msamiati unaotumiwa katika kesi ni muhimu katika uamuzi wa jaji.

Katika diskosi ya kesi B,

> Km: '*You are accused of a secondcountof indescently touching the girl'sgenital area on 4/7/2015 at Kiptere.'*
>
> Mk: Una shtaka mbadala kuwa uliweza kupapasa sehemu za siri za msichana huyo 4/7/2015 ukiwa Kiptere.

Mkalimani anakalimani 'second count of the similar case' kuwa 'kesi mbadala' ya kupapasa sehemu ya siri. Msamiati uliotumiwa unazua wazo kuwa kesi ya kwanza huenda ikatupiliwa mbali na ashtakiwe kwa kosa jipya la kupapasa kwa mkono sehemu ya siri ya msichana huyo. Kwa mshtakiwa asiyeelewa lugha ya mahakama, huenda akafikiria kuwa kesi hiyo ni nafuu na ina hukumu nyepesi kuliko kesi ya kwanza iliyomkabili. Aghalabu, kesi zote mbili zina uzito sawa kisheria kwa sababu zote zinahusu unyanyasaji wa kimapenzi kwa wanawa kike. Kwa hivyo, mkalimani angesema kuwa 'shtaka la pili kuhusu kesi hii ni kuwa ulimkosea heshima kwa kumgusagusa kwa mkono msichana husika sehemu yake ya siri.' Badala yake ukalimani wake ungeleta dhana kwamba mshtakiwa anatolewa mashtaka ya pili yanayohusiana na yale ya shtaka

la kwanza. Huenda akakubali shtaka la pili akifikiri kuwa yale ya kwanza yametupiliwa mbali na mashtaka mepesi kidogo yamechukua nafasi yake huku akifikiri kuwa shtaka lakunajisi limeondolewa na badala yake anashtakiwa kwa kosa la pili la kumpapasa msichana. Mkalimani amefanya hivyo kwa sababu ameshindwa kupata msamiati mwafaka wa kutumia ili kueleza ujumbe huo kwa lugha ya Kiswahili.

Katika kesi C,

> Km: '*AccordingtothecomplainantofthiscasewhoisVictor.'*
>
> *Mk:* 'Kesi hii ambayo ni ya Victor.'

Ujumbe asilia unabadilika kwa kuwa haieleweki kama Victor ni mlalamishi au mshtakiwa. Ukalimani mwafaka ungekuwa, 'Kulingana na Victor, ambaye ni mlalamishi katika kesi hii.' Ukalimani huu ungeonyesha wazi mlalamishi ni nani katika kesi hii.

Pia, katika kesi C,

> *KM: 'The said person (the accused) took the complainant to transport for her sand. Which he did. He was ferrying the sand to the roadside.'*
>
> MK: 'Wewe mshtakiwa ukamchukua akusafirishie mchanga. Ambayo alifanya. Alikuwa anapeleka mchanga kando ya barabara.'

Msamiati '*transport'* umekalimaniwa kuwa 'safirisha' badala ya 'kubeba au kusomba' kulingana na muktadha wa matukio. Msamiati 'kusafirisha' unaibua wazo la masafa marefu mno na pia kwa kutumia chombo cha kusafirisha kama vile gari. Hivyo basi, msamiati 'somba' ambao unaibua dhana ya kubeba kitu kwa masafa mafupi na kukichukua kitu kizito mgongoni, kichwani au begani huku mtu akitembea kwa miguu ungefaa katika muktadha huu.

Isitoshe, katika kesi C,

Km: '*as his mother had received information from school that he had not been attending school and she had been informed by the members of the public that he had been working for the accused person.'*

Mk: 'na mamake alikuwa amepata habari kutoka shuleni kwamba hakuwa akienda shule, alikuwa ameambiwa na watu kwamba walikuwa wamemuona akikufanyia wewe kazi.'

Maneno '*Membersofthepublic'*yanakusudia kuwa na maana ya kipragmatiki ya watu wa eneo hilo ambao walikuwa wakimfahamu mamake mlalamishi, mlalamishi na mshtakiwa husika. Katika diskosi hii maneno hayo yamekalimaniwa kuwa 'watu' badala ya 'umma au watu waliomjua na kumuona.' Msamiati 'watu' hauashirii ujumbe mwafaka kuhusu wananchiwaliomjua na waliomuona huyo mtoto akifanya kazi badala ya kwenda shuleni. Hapa msamiati 'watu' unaweza kumaanisha yeyote hata wale wasiomjua huyo mtoto.

Vile vile, katika kesi C,

*KM: 'On second July, when the complainant saw his mother when he was carrying sand, he ran away and his mother ran after him.'*

MK*:* 'Na hii tarehe mbili mwezi wa saba wakati mlalamishi alimwona mamake, akiwa amebeba mchanga, alitoroka lakini mamake alitoka kumfuata.'

Hapa, neno '*and'* limekalimaniwa kuwa 'lakini' neno ambalo linaibua wazo la kupinga au wazo la ukatifu ili kufafanua jambo fulani. Ujumbe uliokusudiwa katika matini asilia ni 'na hivyo'. Pia, katika ukalimani huu haieleweki kama ni mama au mtoto aliyekuwa akibeba mchanga.

Katika diskosi ya kesi C pia, mkalimani amekalimani maneno, ‘*ashismotherhadreceivedinformation*…’ kuwa ‘na maamake alikuwa amepata habari…’ ambapo neno ‘as’ limekalimaniwa kuwa ‘na’ badala ya ‘kwa sababu’. Dhana ya nyongeza imechukua mahali pa dhana ya ‘kwa sababu’ na hivyo kubadilisha maana ambayo ilikuwa imekusudiwa katika matini asilia.

Katika kesi D,

> KM: ‘*TheAPofficerswhowereontheirroutine duty at Fort Tenan area, at the shopping centre, found the accused person who appeared suspicious and on approaching him he started running away. They followed him.They caught him. On inquiring and doing a search, they discovered twenty four rolls of bhang from his trauser pocket. They arrested himand took possession of the recovered bhang.’*
>
> MK:’ Maofisa wa utawala ambao walikuwa wakifanya kazi yao ya kawaida *area*ya Fort Tenan, walikupata wewe mshtakiwa ukionekana mshuku*. Walipokukaribia, ulianza kukimbia. Walikufuata, wakakushika. Walikushikashika waliendelea kupata misokoto ya bangikutoka mfuko wako wa long’i

Katika matini hii, mkalimani anakalimani kifungu ‘*appearedsuspicious’* kuwa ‘ulionekana mshuku’. Neno ‘mshuku’ si leksimu katikalugha ya Kiswahili bali alikusudia kusema kuwa ‘alionekana kama mhalifu’. Mkalimani alikusudia kunyambua neno la Kiswahili ‘shuku’ liwe ‘mshukiwa’ ili kuwa nomino lakini hana ujuzi wa lugha ya Kiswahili kwa hivyo unyambuzi wake umezua mtafaruku kuhusu alichomaanisha anapotumia neno ‘mshuku’ ambalo si msamiati katika lugha ya Kisawhili. Hata hivyo, msamiati mwafaka katika muktadha huu ni ‘mhalifu’.

Pia, maneno '*doingasearch'* yamekalimaniwa kuwa 'kushikashika' badala ya 'kupekua, kusaka au kupeleleza' kwa maana ya kutafuta kitu fulani kwa kumgusa mtu sehemu mbalimbali za mwili wake au mavazi au anachokibeba. Msamiati 'kushikashika' unaibua wazo la kucheza au kufanya mzaha na sio wazo la kumpekua mshukiwa wa uhalifu ilivyokusudiwa katika LC.

Sehemu ya sentensi, '*Theyfoundrollsofbhang'* imekalimaniwa kuwa 'waliendelea kupata bangi.' Ni wazi kuwa mkalimani ametumia neno 'waliendelea' badala ya ujumbe uliokusudiwa kuwa 'walipompekuawalipata' misokoto ya bangi. Ujumbe umebadilika kuwa walikuwa wamepata bangi tayari na wakiendelea kupata nyingine walipompekua zaidi. Ujumbe uliokusudiwa katika matini asilia ni kuwa walipomkamata na kumpekua, walipata misokoto hiyo ya bangi.

Maneno '*heranaway'* yamekalimaniwa kuwa 'alikimbia' ambalo katika mawazo ya watu wengi huibua wazo la kufanya mazoezi au mchezo wa riadha. Badala ya kukimbia mkalimani angetumia neno 'kutoroka' ambalo linaibua wazo la kukimbia ili kuepuka kukamatwa au kukutana na mtu fulani na linaleta taswira ya mshukiwa huyo akikimbia huku askari wakimfukuzia nyuma ili wamkamate.

Katika matini hii, mkalimani alishindwa kukalimani msamiati '*shoppingcentre'* hadi lugha ya Kiswahili. Badala ya maneno hayo ya Kiingereza mkalimani alitumia neno lingine la Kiingereza '*area'* ambalo haliibui taswira ya eneo la maduka. Neno '*area'*linaibua dhana ya eneo fulani lolote ambalo si lazima liwe na maduka au eneo la kibiashara. Kwa hivyo, ujumbe kuhusu eneo lenye maduka ya kuuzia bidhaa mbalimbali haujitokezi alivyokusudia msemaji wa diskosi asilia katika lugha ya Kiingereza.

Katika kesi E,

*KM: The complainant was at her place of work, when you the accused, went and confronted her there where she attacked her by scratching her.*

MK: Mlalamishi alikuwa mahali pake pa kazi, wakati wewe mshtakiwa, wakati ulienda na kumsimamia mahali pake na kumshambulia kwa kumkwaruza.

Fungu la maneno,'*Went and confronted her there'*limekalimaniwa kuwa 'wakati ulienda na kumsimamia mahali pake (pa kazi)' ambapo dhana ya mshtakiwa 'kufanya kazi kwa niaba ya mlalamishi' imejitokeza. Ujumbe uliokusudiwa ni kuwa mshtakiwa alimkabili kwa nia ya kumpiga au kumgombeza mlalamishi akiwa kazini kwake.

Pia, katika diskosi hii kiongozi wa mashtaka anasema,

Km: '*Shehadbeenbeatenbyherhusband*'.

Mk: 'ulikuwa umepigwa na bwanako'

Mkalimani anatumia msamiati 'bwana' ulio na vikoa vya maana ambavyo vitaleta utata katika kuelewa maana iliyokusudiwa. Dhana 'bwana'katika matumizi ya lugha ya kila siku ina maana ya 'mwajiri wake', 'mumewe' au mwanamume yeyote yule anayestahili heshima zake. Ukalimani wa mkalimani unatokana na mazoea ya matumizi ya neno 'bwana' hata hivyo, msamiati huu wa Kiswahili ungeibua maana yoyote kati ya hizo zilizotajwa hapo juu kwa wasikilizaji kwa sababu katika muktadha huu kumetajwa 'kazi'. Ujumbe wa mkalimani unakanganya kwa vile haieleweki kama ni 'mwajiri' au 'mumewe' ambaye alikuwa anamchapa kulingana na wanawake ambao walikuwa wakimsengenya katika LP.

Ujumbe katika sentensi,

Km: '*Thecomplainantraisedanalarm…'*

Mk: ’Mlalamishi aliweza kupiga rabsha…’

Dhana ‘kupiga rabsha’imetumika kama msemo wa lugha ya Kiswahili ili kusawazisha msemo wa Kiingereza ‘*raiseanalarm’* lakini msemo wenyewe ni ‘zua rabsha’ ambao unazua ujumbe wa kisemantiki kuwa alisababisha fujo au kusababisha kuwepo kwa kelele nyingi zenye vurugu na machafuko. Ujumbe uliokusudiwa katika matini chanzi ni kuwa mlalamishi ‘alipiga kamsa’ au kelele ili kuita watu waende kumsaidia wakati alikuwa akiaziriwa kwa kushambuliwa na mshtakiwa.

Vilevile, katika diskosi za kesi F,

*KM: ‘On 4/8/2016, police officers who were at Kipsitet shopping centre were informed of the presence of the accused person in the shopping centre, who was suspected to be of foreign national. The officers approached this person and on interrogation, they actually established that he is a Tanzanian national. At that particular time, you did not have any entry permit or any authorization to allow you to be in Kenya.’*

MK: ‘Jana saa tano na nusu, maaskari ambao walikuwa katika soko ya Kipsitet … kwamba ulishukiwa kuwa wewe si mtu wa Kenya, ni wa nchi ingine. Maaskari walipokuja na kukuuliza maswali walijua kuwa wewe ni mwananchi wa Tanzania. Hukuwa na *permit* yoyote au kibali ya kuonyesha kuwa ulikuwa umekubaliwa kuingia Kenya.’

Hapa, mkalimani alikalimani ‘*shoppingcentre’* kuwa ‘soko’ ambapo ameibua dhana ya kuwa alikuwa amekamatwa akiwa katika eneo la wazi ambapo bidhaa huuzwa ilhali kiongozi wa mashtaka alikuwa anamaanisha eneo la maduka. Ujumbe uliojitokeza kutokana na ukalimani huo huenda ukampa mshtakiwa nafasi ya kukataa mashtaka kwa sababu hakukamatwa kwenye eneo

la soko bali kwenye eneo la maduka. Taswira ya nyumba nyingi za kuuzia bidhaa inafaa kujitokeza na si eneo tambarare au jumba moja kuu la kuuzia bidhaa.

Mkalimani alikalimani visivyo maneno '*anyentrypermitoranyauthorization to allow you to be in Kenya'* na badala yake alikalimani neno '*permit'* kuwa 'kibali' aliposema 'hukuwa na *permit* yoyote au kibali ya kuonyesha kuwa ulikuwa umekubaliwa kuingia Kenya'. Maneno '*permit* na '*anyauthorization'*yamechukuliwa kuwa yana maana sawa ndio sababu mkalimani anatumia msamiati 'kibali' ili kurejelea dhana zote mbili. Mkalimani angesema 'hukuwa na kibali wala stakabadhi zozote za kukukubalia kuingia Kenya.'

Mkalimani alikalimani maneno '*…ataround11.00am'*, kuwa 'saa tano na nusu' bila kutaja kwamba ni asubuhi. Ukalimani huu unaweza kuvuruga ujumbe kwa sababu karibu saa tano inaweza kuwa kati ya saa nne na nusu na saa tano na nusu. Pia, hali ya kutojulikana kama ni mchana au usiku inaweza kuleta utata katika kuelewa ujumbe uliokusudiwa. Mkalimani angesema 'takribani saa tano asubuhi' ndipo ujumbe uliokusudiwa ueleweke ilivyostahili.

Hali hii ya kukosa kukalimani ujumbe uliokusudiwa katika diskosi hizi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama unaashiria kuwa huenda wahusika wakakosa haki au kupata hukumu isiyowafaa. Hii ni kwa sababu hakimu anamtegemea mkalimani kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa katika matini chanzi ili kupata majibu sahihi kwa maswali wanayoulizwa. Majibu ya wahusika humsaidia hakimu kukata kesi husika inavyostahili.

### 4.3.4. Ujumbe Uliochopekwa

Kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili sanifu TUKI(2000),uchopekaji ni kuweka vitu baina ya vitu vingine. Katika muktadha huu wa ukalimani neno uchopekaji litakuwa na dhana kwamba ni mchakato wa kubadili umbo la nje la sentensi kwa kuliongezea maneno ambayo hayakutokea

katika MC lakini ambayo mkalimani anadhamiria kuyatumia ili kueleweka. Anapofanya hivyo, mkalimani anakiuka sharti la kuwa mkalimani bora kwa sababu ya kupitisha ujumbe na maoni yake binafsi ambayo hayakubaliki katika ukalimani.

Katika diskosi ya kesi C, mkalimani alikalimani '*Whenhewasworkingforyou*,' kuwa 'akiwa anakufanyia kazi kama kawaida,' ambapo ni wazi kuwa ameongeza maneno 'kama kawaida' kana kwamba lilikuwa ni jambo la kawaida kwa mtoto huyo kumfanyia mshtakiwa kazi hiyo. Mkalimani alichopeka maneno hayo kutokana na uelewa wake wa ujumbe wa kiongozi wa mashtaka bila kuzingatia maneno yaliyotumiwa moja kwa moja. Maneno yaliyochopekwa katika usemi huu yanaibua dhana kuwa lilikuwa ni jambo lililozoeleka na kuwa mlalamishi alikuwa akimfanyia mshtakiwa kazi wakati wote wala si siku hizo chache ambazo alifanya kazi bila mamake mlalamishi kujua.

Mkalimani vile vile katika diskosi za kesi C amekalimani sentensi '*Iwillenterforyouapleaofnotguiltybecauseyouhavedeniedthejudges*…' kuwa 'Umekataa maelezo, kwa hivyo korti itaandika kuwa umekataa mashtaka…' ambapo mkalimani alichopeka maneno umekataa 'maelezo' badala ya 'mashtaka' yaliyomkabili mshtakiwa. Katika sehemu hii, mkalimani aligundua kuwa alitumia msamiati ambao si sahihi na akarekebisha kwa kurudia ujumbe huo kwa kutumia msamiati 'mashtaka' ili kuweza kueleweka vilivyo.

Katika diskosi F, mkalimani anachopeka maneno ambayo hayakutokea katika diskosi asilia anapokalimani '*foreignnational'* kuwa 'si mtu wa Kenya, ni wa nchi ingine'. Maneno 'si mtu wa Kenya' yameongezwa na mkalimani ili kusisitiza kuwa mtu huyo ni mgeni na mtu kutoka nchi nyingine ambayo si Kenya.

**4.3.5 Ujumbe Uliodondoshwa**

Kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili sanifu TUKI (2000), udondoshaji ni mchakato wa kuacha nje viambajengo vya sentensi wakati wa kuikalimani na hivyo sentensi husika huchukua muundo wa nje tofauti kabisa katika ML na ule wa MC. Hali hii hutokea mkalimani anapoamua kuwa ujumbe fulani haufai kukalimaniwa kwa sababu hauna uzito wa kubadilisha ujumbe muhimu wa diskosi husika. Baadhi ya wakati, mkalimani husahau sehemu ya ujumbe mzima uliosemwa katika MC kwa sababu ya kuwa na kumbukumbu mbaya au kwa sababu hakusikia sentensi yote kwa sababu anasikiliza anayoyasema msemaji wa LC huku akikalimani katika LL. Katika utafiti huu, mkalimani amedondosha ujumbe uliokusudiwa katika MC kama ifuatavyo;

Katika diskosi ya kesi A sentensi ‘*Together, youwerefoundbytheofficersplayingcards’* imekalimaniwa kuwa ‘mlikuwa pamoja, mlipatikana mkicheza mchezo wa karate’. Hapa mkalimani alikosa kuwataja ‘maafisa wa polisi’ ambao waliwakuta wahalifu hao wakiwa pamoja wakicheza mchezo huo ndipo wakawakamata. Mkalimani alifaa kukalimani kuwa maafisa wa polisi waliowakamata waliwavumania wakiwa pamoja wakicheza mchezo huo haramu wa kamari.

Katika diskosi ya kesi A, mkalimani amedondosha baadhi ya maneno katika ukalimani anapohawilisha ujumbe wa LC hadi LL. Ametumia maneno machache ili kuwasilisha ujumbe ambao alichukulia kuwa muhimu kwa mshtakiwa ambapo hakukalimani maneno ‘*andtheywillwinmoney’*. Ujumbe kuhusu kutapeliwa kwa umma kwa njia ya udanganyifu haukujitokeza katika LL.

> *Km: You have been accused of cheating the public that you are playing cards and they will win money.*
>
> Mk: Mmeshtakiwa kwa kosa la kucheza karate kwa umma.

Katika diskosi ya kesi A, mkalimani alikosa kukalimani diskosi yote ya kiongozi wa mashtaka baada ya washtakiwa kuitikia mashtaka. Alidondosha sehemu kubwa ya MC na kukalimani sentensi ya mwisho pekee ya ujumbe wa kiongozi wa mashtaka. Sehemu hii ni matini ambayo haikukalimaniwa;

> *KM:'I wish you to know that the accused have agreed that they were found in the said place and there were cards found in their possession which they used to play and fifty shillings which the officers found with them where they were playing the cards. I have them and I want to produce them as exhibit for this case;the cards are here and the fifty shilling coins.'*
>
> Mk: 'Na kadi ambazo mlishikwa nazo na kiongozi wa mashtaka anataka kuzitoa na pia pesa shilingi hamsinikama kielelezo.'

Ujumbe wote wa sentensi ya kwanza katika sehemu hii haujitokezi kwa vyovyote kwa sababu mkalimani hakukalimani sentensi hii nzima. Hii inaonyesha kuwa ni vigumu kuwa na usawa katika ukalimani wa ujumbe kutoka matini chanzi hadi matini lengwa. Hakuna sababu maalumu kuhusu hali hii ila kuwa mkalimani pengine aliamua kuwa ujumbe katika sentensi hii si muhimu na hivyo kuacha kuukalimani. Udondoshaji wa ujumbe kama huu unaweza kumkosesha mshtakiwa nafasi ya kuelewa mashtaka dhidi yake na kumfanya hakimu kutoa uamuzi usiofaa katika kesi husika.

Vivyo hivyo, katika diskosi ya kesi B,

> *Jaji: So, a plea of not guilty has been entered for you.*
>
> *Mk: ...*

*Jaji: And the alternative*

*Mk:* ...

*Jaji: You will be given another date of hearing.*

Mk: Utapewa tarehe ya kusikilizwa tena.

Mkalimani alikosa kukalimani sentensi mbili za jaji na hivyo ujumbe ambao jaji alikusudia kumwarifu mshtakiwa haukuweza kumfikia mshtakiwa huyo. Hivyo basi, itachukuliwa kuwa mshtakiwa hakujua kuwa hakuwa amekiri makosa yake yote mawili aliyosomewa mahakamani mbele ya jaji na hivyo alihitajika kusomewa mashtaka yake upya katika tarehe mpya ya kesi kusikilizwa tena mahakamani. Ujumbe huo ulipotea kwa sababu mkalimani aliamua kudondosha sentensi hizo katika ukalimani wake kwani alifikiri kuwa si muhimu kwa mshtakiwa.

Pia, katika diskosi za kesi C, mkalimani alikosa kukalimani sentensi,

*Km: 'According to the complainant of this case who is Victor. However, he was not paid because he did not finish and the rain started raining before lunch time.'*

Mk: 'Kesi hii ambayo ni ya Victor. Hakumaliza. Mvua ilianza kunyesha kabla ya saa ya maakuli.'

Mkalimani alidondosha ujumbe '*However, hewasnotpaid because he did not finish'* yaani 'mlalamishi hakupata malipo ya siku hiyo kwa sababu hakumaliza kazi'. Ujumbe huu ni muhimu katika diskosi hii kwani kutolipwa kwa mlalamishi pengine ndiko kulikomfanya mamake mshtakiwa kuenda kumtafuta mwanawe na kumshtaki mshtakiwa kwa kumfanyiza mwanawe kazi wakati alistahili kuwa shuleni. Pia, mkalimani anadondosha maneno '*accordingtothecomplainant'* na '*However, hewasnotpaidbecausehedidnotfinish'* anapokalimani

matini katika LP kwani pengine alifanya uamuzi kuwa ujumbe huo si muhimu katika kesi hii. Hata hivyo, ukosefu wa ujumbe huo katika MP huenda ukaathiri maamuzi ya jaji.

Isitoshe, mkalimani amekalimani maneno ya jaji, '*Theaccused, isthattrue*?' kuwa 'Hayo maelezo ni ya ukweli?' Mkalimani amedondosha maneno '*Theaccused'*. Katika ML haieleweki anayeulizwa swali hili kama ni mshtakiwa au ni kiongozi wa mashtaka au mtu mwingine katika ukumbi wa mahakama. Hali hii huenda ikamfanya mshtakiwa kutojibu swali hili kwa sababu hajui kama mlengwa wa swali hili ni yeye mshtakiwa.

Katika diskosi D, mkalimani mbali na kukosa kukalimani ujumbe huu;

Km '*On inquiring and doing a search they discovered'*

Mk: 'Walikushikashika waliendelea kupata'.

Maneno *'On inquiring'* yamedondoshwa katika sentensi ya mkalimani anapokalimani kipande hiki cha ujumbe wa kiongozi wa mashtaka.Hali ya kumpekua mshtakiwa ili kuchunguza kama alikuwa na bangi hiyo haijitokezi katika sehemu ya ukalimani katika LL. Badala yake, inaonyesha kuwa walikuwa wanampapasapapasa kana kwamba walikuwa wanacheza au kumchokoza bila kutafuta chochote na hawakupeleleza kwanza kabla ya kuanza kumpekua mshukiwa.

Vivyohivyo, katikakesi *E*,

*KM: You injured her on her left side of the nose, and the upper right arm.*

MK: Ulimjeruhi upande wake wa kushoto wa pua na upande wa kulia.

Mkalimani alikosa kukalimani ujumbe uliokusudiwa katika LC mara kadhaa aliposhindwa kupata msamiati mwafaka katika LL. Mkalimani alilazimika kudondosha baadhi ya ujumbe au

kuteua msamiati ambao alionelea ulikaribiana kimaana na msamiati ambao ulifaa kutumiwa. Kwa kufanya hivyo, alipoteza ujumbe ambao ulikusudiwa katika MC. Kwa mfano;

*'You injuredher on…upperrightarm*' ulikalimaniwa kuwa 'ulimjeruhi …upande wa kulia' ambapo mkalimani amedondosha maneno '*upperarm'*. Hali hii inasababisha kutoeleweka mahali ambapo aliumizwa. Inaweza kueleweka kuwa alimjeruhi sehemu ya kulia na kushoto kwenye pua lake au sehemu ya kushoto ya pua na sehemu yoyote ya kulia kwenye mwili wa mlalamishi. Kutokana na ukalimani huu mlalamishi aliumizwa sehemu ya kulia fulani au sehemu zote za kulia za mwili wa mlalamishi.

Katika diskosi ya kesi E,

> *Km: She boarded a motorcycle and went to the police station where she reported her complaint.*
>
> Mk: aliweza kuenda kituo cha polisi na kuweza kuripoti.

Sehemu ya sentensi ya kiongozi wa mashtaka katika matini hii, 'She b*oardedamotorcycle and'*haikukalimaniwa. Maneno haya yote yalidondoshwa na kusababisha kupotea kwa ujumbe ambao ulikusudiwa kuonyesha kuwa mlalamishi alitumia pesa kiasi fulani katika usafiri kwa pikipiki, pesaambazo huenda akadai kufidiwa na mshtakiwa wa kesi hii. Jaji pia alifaa kuelewa hivyo na kuzingatia jambo hilo wakati wa kukata kesi na mshtakiwa naye alifaa kuelewa hivyo kutokana na ukalimani wa ujumbe husika ili asije akaduwaa akiambiwa amlipe mlalamishi kiasi fulani cha fedha kama fidia.

Isitoshe, katika diskosi za kesi E,

*KM:'She reported at Nyagacho Police Station. The complainant was treated at Kericho District Hospital and issued with a p3 form. The statements were recorded.*

MK: 'Aliripoti Nyagacho Police Staion. Na mlalamishi aliendа Kericho District Hospital na aliweza kujaziwa p3 form. Na mlalamishi aliweza kuandika *statement*.'

Maneno *'was treated…'* yalidondoshwa pia kusababisha kupotea kwa ujumbe kuwa alitumia pesa ili kupata matibabu katika hospitali na alikuwa ameumia sana na hivyo mlalamishi huenda akadai fidia kutoka kwa mshtakiwa. Mshtakiwa hakupokea ujumbe huo na huenda akashindwa ni kwa nini jaji amwagize katika hukumu yake kuwa amfidie mlalamishi katika kesi hii.

Maneno '*policestation'*, '*statement* na *districthospital'* yanasalia hivyo katika MP kwa sababu mkalimani hakupata kisawe chake katika lugha ya Kiswahili.

Katika kesi F, mkalimani amedondosha sehemu nzima ambayo inarejelea tarehe '*On4$^{th}$ /8/2016, that is yesterday, at around 11.00am'* kutoka sentensi ya kiongozi wa mashtaka na badala yake mkalimani alikalimani, 'jana saa tano na nusu'. Tarehe iliyotajwa ilikuwa ni ya siku ambayo ilikuwa imetangulia lakini mashtaka hayo yakirejelewa baadaye katika LL, msomaji atatatanishwa na siku mahususi iliyokusudiwa kwa sababu mkalimani amedondosha tarehe iliyotajwa katika MC.

Katika ukalimani wa diskosi ya kesi F,

*Km: Police officers who were at Kipsitet shopping centre*

Mk: Maaskari ambao walikuwa 'soko' ya Kipsitet

*Km: were informed of the presence of the accused person in the shopping centre*

Mk: ………….

*Km: who was suspected to be of foreign national,*

Mk: kwamba ulishukiwa kuwa wewe si mtu wa Kenya, ni wa nchi ingine

Kulitokea ukosefu wa usawa wa ujumbe uliokusudiwa ambapo mkalimani alidondosha maneno '*policewereinformed of the presence of the accused person'* katika LL. Ukosefu were ujumbe huu katika LL utaleta mtafaruku kuhusu walivyojua kuwa mshtakiwa alikuwa mgeni nchini Kenya.

Isitoshe, mkalimani alikosa kukalimani sentensi,*'At that particular time you did not have any entry permit…'*kwa hivyo ujumbe huo haukupitishwa kwa mshtakiwa. Pengine, kudondoshwa kwa sehemu hii ndiko kulikomfanya mshtakiwa kukana mashtaka na hata kuchanganyikiwa akubali au asikubali mashtaka.Hata mshtakiwa aliwambia kuwa huo ulikuwa 'ukweliwao' na akakataa na wakati huo huo kukubali mashtaka mpaka akamchanganya hakimu. Mwishowe, hakimualiamuru afikirie alikusudia nini ndipo asomewe mashtaka yake tena baadaye ndipo pengine ayaelewe ndipo amjibu hakimu.

Pia, katika diskosi F, mkalimani alidondosha ujumbe '*atthatparticulartime'* anapokalimani ujumbe wa kiongozi wa mashtaka*'at that time you did not have any entry permit or any authorization to allow you to be in Kenya.'* Mkalimani anakalimani kuwa 'hukuwa na permit au kibali ya kuonyesha kuwa ulikuwa umekubaliwa kuingia Kenya.' Ni wazi kuwa ujumbe huu ulidondoshwa kwani mkalimani alifikiria kuwa haungebadilisha ujumbe uliokusudiwa katika MC.

**4.4 Changamoto KuhusuUsawa wa Kipengele cha Maumbo**

Kipengele hiki kimeelezwa kutokana na data iliyokusanywa kwa kuzingatia mhimili mmojawapo muhimu wa nadharia ya usawa katika ukalimani. Kulingana na Nida (1976), mhimili huu wa

maumbo unaeleza kuwa maumbo katika MC yanafaa kujitokeza katika ML katika ukalimani wa diskosi za wahusika kutoka muktadha wa LC hadi LL. Maumbo hayo ni pamoja na mofimu, leksimu, virai, na sintaksia.

### 4.4.1 Dhana ya Maumbo

Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili sanifu TUKI (2000), umbo ni mkao wa kitu kilivyoundwa au kilivyoumbwa. Umbo ni sura, jinsi, utaratibu, muundo au desturi ya neno, fungu la maneno ausentensi. Katika utafiti huu, maumbo yanayochunguzwa ni mofimu, leksimu, virai, vishazi na sentensi zilizotokea katika MC na zilivyokalimaniwa katika ML.

Kulingana na Wamitila (2003)maumbo ni mshikamano dhahania wa vipashio vya sentensi ambao ndio msingi wa tafsiri ya maana kamili ya sentensi hiyo. Kulingana na utafiti huu, neno maumbo lina maana sawa na muundo au sura ya matini ya diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama. Maumbo hayo nipamoja na mofimu, leksimu, virai, vishazi na sintaksia katika diskosi husika katika LC na LP.

Pia, Catford (1965)anaposhughulikia nadharia ya usawa, anasema kuwa tunapofanya kazi ya kutafsiri ni muhimu kuzingatia ulinganifu wa kimuundo kati ya MC na ML. Hii ina maana kwamba, muundo wa MC unafaa ujitokeze katika ML. Hata hivyo, kulingana na Catford (1965)ukalimani na tafsiri ni mchakato wenye dosari nyingi kiasi kwamba ni vigumu kulandanisha maumbo ya MC na ML kwa sababu lugha zinazohusika huwa na maumbo tofauti.Kila lugha ina maumbo yake kutegemea muundo wa kijamii. Katika utafiti huu, ilitarajiwa na imebainishwa kuwa maumbo ya lugha ya Kiswahili ni tofauti na maumbo ya lugha ya Kiingereza. Mifano ifuatayo imedhihirisha kuwa si rahisi kulandanisha maumbo ya lugha mbili zenye masharti tofauti ya upatanisho wa kisarufi.

### 4.4.2 Maumbo ya Leksimu Kimofolojia

Kamusi ya Kiswahili sanifu TUKI(2000) inaeleza kuwa mofolojia ni tawi la isimu linalojishughulisha na uchambuzi wa kanuni na mifumo inayohusu upangaji wa mofu mbalimbali ili kuunda maneno yenye maana katika lugha. Leksimu ni kipashio kidogo zaidi cha msamiati ambacho kina uwezo wa kusimama peke yake kama kidahizo au neno lenye maana katika lugha husika. Katika sehemu ifuatayo nimechanganua mifano ya maumbo iliyojitokeza katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi katika uendeshaji wa kesi mbalimbali katika mahakama.

Katika diskosi A, neno moja ambalo lina mofimu tegemezi limetumiwa katika lugha ya Kiswahili kusimamia maneno manne katika lugha ya Kiingereza katika sentensi ya kwanza.

> *Km: 'You have been accused of cheating the public that you are playing cards and they will win money'*
>
> Mk: 'Mmeshtakiwa kwa kosa la kucheza karate kwa umma'

Katika ukalimani wa maneno, '*Youhavebeenaccused'*mkalimaniameyahurutisha katika neno haya ya Kiingereza kama viambishi katika neon moja 'mmeshtakiwa'. Viambishi hivi vya Kiswahili vinamaanisha maneno kamili ya Kiingereza kama ifuatavyo;

> M -*you (*nafsiyapiliumoja*)*
>
> -me-*havebeen (*halitimilifu*)*
>
> Shtakiwa – *accusedof*(kitenzi na kihusishi)

Lugha ya Kiswahili ina uwezo wa kutumia mofimu ambazo zina maumbo yanayoweza kutengwa katika neno na kuwa na maana kisarufi ingawa hayawezi kujitegemea kinyume na lugha ya

Kiingereza ambayo ina mofimu changamano na maneno mazima yaliyo na maana moja kisarufi au hata maneno mawili yaliyo na maana moja. Hii ni kwa sababu lugha ya Kiswahili ni lugha ambishi ambapo mofimu huunganishwa kuunda maneno au hata sentensi za neno moja.

Pia, katika diskosi za wahusika wa kesi B, katika Kiingereza msamiati wa Kiingereza '*penis'* haukukalimaniwa kwa kupewa kisawe chake mahususi na badala yake mkalimani alitoa maelezo marefu kurejelea sehemu hiyo ya mwili ambayo ni mwiko kuitaja hadharani katika utamaduni wa jamii nyingi za Afrika. Mkalimani alikalimani neno hilo kuwa 'sehemu ya uume' badala ya kutumia neno moja hivyo kuathiri muundo wa MC.

Neno 'June' katika MC ya diskosi ya kesi C, limekalimaniwa kwa maneno 'mwezi wa sita' na '*July'* kuwa 'mwezi wa saba'. Mkalimani anatumia mbinu ya maelezo badala ya kutumia neno moja kwa kutohoza maneno 'Juni' na 'Julai'. Hii inaonyesha kuwa muundo wa diskosi ya matini chanzi hauwezi kuwa sawa na ule wa matini lengwa katika ukalimani kwa sababu mkalimani hutumia msamiati unaomjia akilini katika harakati za ukalimani. Nia kuu ya mkalimani huwa ni kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa na si maumbo ya maneno katika matini husika.

Pia, hali hii imeshuhudiwa katika diskosi za kesi C,

Km: *Theaccusedpersonwasarrested*.'

Mk: 'Wewe ulishikwa, mshtakiwa.'

Mkalimani alipokalimani matini katika LP, alitumia mbinu ya neno kwa neno. Maneno '*arrestedtheaccused'* yakawa 'wewe ulishikwa mshtakiwa' badala ya kufuata muundo wa utungaji wa sentensi katika lugha ya Kiswahili. Katika sehemu hii mkalimani angesema 'wewe mshtakiwa, ulishikwa'. Hali hii inaonyesha kuwa muundo wa sentensi za Kiingereza si sawa na muundo wa sentensi za lugha ya Kiswahili na mkalimani alipotumia mtindo wa neno kwa

nen0anapofuata muundo wa lugha ya Kiingereza katika kukalimani ujumbe katika sentensi, upatanisho wa kisarufi hufurugika katika lugha ya Kiswahili.

Katika diskosi ya kesi D,

> Km: '*The AP officers who were on their normal routine duty at Fort Tenan area at the shopping centre, found the accused person who appeared suspicious.'*
>
> MK: 'Maafisa wa utawala ambao walikuwa wakifanya kazi yao ya kawaida,area ya Fortenan. Walikupata mshtakiwa ukionekana mshuku.'

Mkalimani alikalimani maneno '*helookedsuspicious'* kuwa 'ulionekana mshuku' badala ya 'walikushuku' kwa sababu alitatizwa na hali ya unyambuaji wa neno husika ili kuunda nomino iliyokusudiwa katika MC kwa sababu alikalimani neno kwa neno akifuata mpangilio wa maneno katika lugha ya Kiingereza. Umbo sahihi la neno hilo halikufikiwa katika ML katika ukalimani na hivyo kutatiza hali ya ujumbe uliokusudiwa. Hali hii inaonyesha kuwa unyambuzi wa maneno katika lugha ya Kiingereza ili kuwasilisha maana mbalimbali kutokana na mzizi wa neno ni tofauti na namna unyambuzi huo unavyofanywa katika lugha ya Kiswahili. Katika Kiingereza unyambuzi hufanywa mwishoni mwa mzizi wa neno lakini katika Kiswahili unyambuzi hutokea mwanzoni na mwishoni mwa neno. Viambishi hivyo awali na tamati katika unyambuzi wa maneno katika lugha ya Kiswahili hulipa neno husika maana mbalimbali.

Katika diskosi ya kesi D, maneno ya kiongozi wa mashtaka:

> Km: '*Oninquiringanddoingasearchtheydiscovered twenty two rolls of bhang.'*
>
> Mk: 'walikushikashika waliendelea kupata…'

Katika sehemu hii maneno ya kwanza manane katika matini chanzi yalikalimaniwa kwa maneno matatu pekee na umbo la sentensi limebadilika kwa sababu maneno ya Kiswahili yalihulutisha mofimu nyingi ili kuunda neno moja tofauti na maneno ya lugha ya Kiingereza ambapo kila neno huwa na maana maalum isipokuwa ambapo kitenzi hujumuisha wakati uliopo na uliopita.

Katika ukalimani wa diskosi za kesi E, maumbo ya matini ni tofauti kati ya LC na LL ambapo katika Kiingereza kuna matumizi ya maneno mawili '*herhusband'*lakini katika Kiswahili dhana hizo mbili zimewekwa kwenye neno moja kwa **kuhulutisha** dhana hizo mbili. Kwa mfano, 'bwanako' badala ya 'bwana yako' kuonyesha kuwa si rahisi mkalimani kufikia usawa wa maumbo ya LC anapokalimani katika LL. Hii ni kwa sababu maumbo ya maneno na mpangilio wa maneno katika sentensi katika lugha hizi mbili ni taofauti.

Pia, katika diskosi F, maneno '*Tanzaniannational'*yamekalimaniwa kuwa 'mwananchi wa Tanzania' ambapo umbo la maneno haya limebadilika kwani nomino Tanzania imenyambuliwa mwishoni katika lugha ya Kiingereza lakini katika Kiswahili nomino hiyo haiwezi kuchukua viambishi tamati. Neno lililokuwa mwisho katika lugha ya Kiingereza limekuwa la kwanza katika lugha ya Kiswahili. Hali hii inatokana na kanuni tofauti za mpangilio wa maneno kufuatia upatanisho wa kisarufi katika lugha mbili husika. Pia, katika matini pokezi, maneno matatu yametumiwa badala ya mawili ili kusawazisha maumbo katika ukalimani katika MC kwa sababu katika Kiswahili hali ya umilikaji haihulutishwi na nomino kama ilivyo katika kiingereza. Hali hii inapelekea kutofautiana kwa maumbo ya matini katika LC na LL.

### 4.4.3 Maumbo ya Virai na Vishazi

Kwa mujibu wa TUKI (2000), kirai ni kipashio cha kimuundo chenye neno moja au zaidi lakini hakina uhusiano wa kiima-kiarifu (nomino na kitenzi). Matei (2008) anaeleza kuwa kirai ni fungu la maneno ambalo hufanya kazi kama neno moja au huwa na uamilifu sawa kimaana;

yaani kirai hudokeza maana lakini maana hiyo si kamilifu kwa sababu kirai hakina kitenzi kinachokamilisha wazo husika. Umbo la kirai sharti liwe neno moja au fungu la maneno ambalo linarejelea maana mahususi lakini maana hiyo si wazo kamili kwa sababu kirai si sentensi.

TUKI (2000)inaeleza kuwa kishazi ni fungu la maneno lenye muundo wa kiima-kiarifu ambalo limo ndani ya sentensi.Matei (2008) anafafanua kishazi kama fungu la maneno ambalo lina kiima kimoja na kiarifu kimoja na kila sentensi angalau ina kishazi kimoja.Hivyo basi, kishazi ni sehemu ya sentensi iliyo na kiima na kiarifu ambacho kinaweza kujisimamia na kuleta habari kamili kuhusu kiima (kishazi huru) au kukosa kujisimamia na kuleta habari kamili kuhusu kiima (kishazi tegemezi).

Katika diskosi A, mpangilio wa maneno katika kirai nomino ‘Kericho town’ umechukua mkondo tofauti ‘Mji wa Kericho’ badala ya ‘Kericho Mji’ kwa sababu mpangilio wa maneno katika sentensi ya Kiswahili ni tofauti na ule wa Kiingereza.

Pia, katika lugha ya Kiingereza kishazi, ‘*Youhavebeenaccusedof…*’ yamekalimaniwa kwa maneno mawili pekee, ‘Mmeshtakiwa kwa…’ kwani neno ‘mmeshtakiwa’ limesheheni mofimu tegemezi ambazo zimefumbata maana iliyokusudiwa katika maneno yale ya Kiingereza. Maumbo hayo ni tofauti kama inavyoonyeshwa hapa:

*You* – M-

*Havebeen* – me-

*Accused*- shtakiwa

*Of* - kwa

Pia, katika diskosi A, mkalimani alikalimani,

Km: ‘*Youhavebeenconvictedonyourownplea’*

Mk: ‘Korti inakutolea hukumu, mmekubali mashtaka.’

Mkalimani amevunja sentensi ya LC kuwa vishazi viwili katika LL. Ile ya Kiingereza ilikuwa na kishazi kimoja ilhali anapokalimani kwa kuzingatia mpangilio wa maneno katika sentensi ya Kiingereza, mkalimani anaishia kutumia vishazi viwili.

Katika diskosi B, amekalimani kwa neno moja manenoya Kiingereza *‘You are accused of ...’*kuwa ‘unashtakiwa…’ Mofimu zimechukua nafasi ya maneno mazima;

Kiambishi cha nafsi ya tatu u-*you*,kiambishi cha wakati uliopo -na-*are* na -shtakiwa-*accused*.

Pia, amekalimani katika vishazi viwili ‘*Nootherpriorrecords’* kuwa ‘Hakuna rekodi, hajawahi kufanya makosa mbeleni’ badala ya ‘Hakuna rekodi za awali kuwa amefanya makosa mengine.’ Katika LC kishazi kimoja kimetumiwa lakini katika LL vishazi viwili vinatumika kwa sababu mkalimani alijaribu kueleza msamiati ‘prior records’ kama unavyotumiwa katika mahakama. Hii ni kwa sababu mkalimani alikosa msamiati wa neno moja mwafakana hivyo akalazimika kutoa maelezo marefu na akajirudiarudia.

Baadhi ya maumbo ya sentensi za Kiingereza huwa na maneno mengi lakini katika Kiswahili neno moja huchukua nafasi ya maneno mengi kwa sababu maneno ya Kiswahili huweza kuambikwa mofimu zenye maana kisarufi. Kwa mfano, maneno ‘*membersofthepublic’* yamekalimaniwa kuwa ‘watu’ ambapo kirai chenye maneno matatu kimechukuliwa na neno moja.

Katika diskosi C, kishazi cha neno moja la Kiswahili ‘ukamchukua’ limechukua nafasi ya kishazi maneno ya Kiingereza ‘*youtookthecomplainant’*kuonyesha kuwa ni vigumu kufikia usawa wa maumbo ya virai au vishazi kwa sababu maumbo ya maneno ya Kiingereza si sawa kimuundona maumbo ya maneno ya Kiswahili. Pia, mkalimani anakalimani kwa neno moja

‘akusafirishie’ maneno ya Kiingereza ‘*totransportforher…*’ ‘Ulimpatia’- ‘*shegavehim’*. Viambishi katika lugha ya Kiswahili na maana yao katika lugha ya Kiingereza inaonyeshwa hapa:

U – you, -ka –past tense, m – the complainant, chukua – take

Katika diskosi ya kesi C, Mkalimani anakalimani kwa maneno mengi ujumbe wa kiongozi wa mashtaka. Maneno ‘*OntwentyninthJune’*yakawa ‘Tarehe ishirini na tisa mwezi wa sita mwaka huu’. Mkalimani anatumia maelezo badala ya msamiati ‘Juni’ na anaongeza maneno ‘mwaka huu’ ambayo hayakutokea katika matini asilia. Hata hivyo, maneno hayo yametumiwa kusisitiza kielezi cha wakati wala ujumbe uliokusudiwa haukupotea.

Kirai ‘*twenty shillings’* kinakalimaniwa kuwa ‘shilingi ishirini’. Ambapo katika Kiingereza kirai hiki kimeanza kwa kivumishi idadi kisha nomino, katika lugha ya Kiswahili kirai hiki kimeanza na nomino kisha kivumishi idadi.

Maneno ‘*thesaidperson’*yanakalimaniwakuwanenomoja “wewe’ ‘*calledhim’* kuwa ‘ulimuita’ huku ‘*toworkforyou’*ikawa ‘akufanyie kazi’. Virai hivi vimedhihirisha kuwa usawa wa maumbo katika ukalimani ni jambo linalotokea kwa nadra sana mkalimani anapohawilisha ujumbe kutoka lugha moja hadi nyingine.

Mpangilio wa maneno katika umbo la kirai ‘*hismother’* umekalimaniwa kuwa ‘mama yake’ ambapo kirai cha Kiingereza kimeanza na kivumishi-kimilikishi kisha nomino lakini kirai cha Kiswahili kimeanza na nomino kisha kivumishi-kimilikishi. Kishazi ‘*workingforthesaidperson’* kimekalimaniwa kuwa ‘akikufanyia wewe kazi’, ‘*totrackhim’* ikawa ‘kumtafuta’, ‘*heranaway’* ikawa ‘alitoroka’, ‘*shecaughthim’* ikawa ‘alimshika’, na ‘*tookhim’* ikawa ‘alimpeleka’ ambapo

idadiya maneno na maumbo ya maneno ni tofauti kwasababu ya kuhulutishwa kwa mofimu katika lugha ya Kiswahili.

Katika diskosi za kesi D, kishazi:

Km: '*foundtheaccusedpersonwhoappearedsuspicious'* kuwa

Mk: 'walikupata mshtakiwa ukionekana mshuku'.

Hapa mkalimani alifuata mpangilio wa umbo la matini chanzi lakini bado alitumia maneno machache kwa sababu katika lugha ya Kiswahili kuna viambishi ambavyo vinahulutishwa katika neno moja ili kufumbata maana ya maneno zaidi ya moja katika lugha ya Kiingereza.Mifano ifuatayo inadhihirisha hali hii;

Km: '*Onapproachinghim, hestartedrunningaway'* kuwa

Mk: 'Walipokukaribia ulianza kukimbia',

Km: '*astheyfollowedhim'* kuwa

Mk: 'Walikufuata", na

Km: '*Theycaughthim'* kuwa

Mk: 'Walikushika.'

Katika diskosi za kesi E, kishazi '*Youareaccusedofassault'* kuwa 'Umeshtakiwa kwa kumshambulia.', '*andwasrescuedbymembersofthepublic'* kuwa 'raia waliweza kuja na kumsaidia' kuonyesha kuwa maumbo ya lugha ya Kiswahili ni tofauti na ya lugha ya Kiingereza.

Ni wazi kuwa idadi ya maneno na mpangilio wa maneno katika lugha hizi mbili husika si sawa kwa sababu mfumo wa maumbo ya virai na vishazi katika lugha hizi ni tofauti ingawa zote hutumia othografia sawa.

#### 4.4.4 Maumbo ya Kisintaksia

Kamusi ya TUKI (2000) inaeleza kuwa sintaksia ni tawi la isimu linalojihusisha na miundo na uchanganuzi wa taratibu za uhusiano baina ya maneno katika tungo. Katika sehemu hii maumbo ya sentensi za LC na ya LL yamechunguzwa ili kubainisha usawa au ukosefu wa usawa wao.

Katika diskosi za kesi A, sentensi ya kwanza,

> *KM: You have been accused of cheating the public that you are playing cards and they will win money.*
>
> MK: Mmeshtakiwa kwa kosa la kucheza ‘karate’ kwa umma.
>
> Km: *together, youwerefoundbytheofficers, playingcardstothepublicwithoutalicence*.’
>
> Mk: mlikuwa pamoja mlipatikana mkicheza mchezo wa 'karate' kwa umma na hamna leseni.

Ukalimani huu umefanya mpangilio wa maneno kisarufi kukosa upatanisho wa kisarufi fasaha katika lugha ya Kiswahili. Mpangilio wa maneno katika sentensi ya Kiswahili umevurugwa ili kufuata mpangilio wa maneno katika sentensi ya Kiingereza. Sentensi ya mwisho ya kiongozi wa mashtaka na ukalimani wa mkalimani katika diskosi hii ni tofauti kimaumbo na idadi ya maneno ni tofauti kwa sababu kanuni za utungaji wa sentensi ni tofauti katika lugha hizi mbili. Hata hivyo, ujumbe ambao mkalimani alionelea unamfaa mshtakiwa ndio pekee ambao ameukalimani kuonyesha kuwa ni vigumu kusawazisha maumbo ya kisintaksia katika ukalimani.

Katika diskosi za kesi C, umbo la sentensi,

KM: *Theaccusedpersonwasarrested.*

MK: Wewe ulishikwa, mshtakiwa.

KM:*Iwillenterforyouapleaofnotguiltybecauseyouhavedeniedthecharges. Youwillbegivenanotherdate*.

MK: Umekataa maelezo, kwa hivyo korti itaandika kuwa umekataa mashtaka na utapewa tarehe.

Ukalimani uliofanywa ulifuata mfumo wa neno kwa neno na kukosa kuzingatia upatanisho wa kisarufi katika LL ya Kiswahili. Hata hivyo, maneno yaliyotumiwa katika LL ni machache kuliko yale ya LC kwa sababu lugha ya Kiswahili huwa na uwezo wa kuhulutishwa mofimu nyingi katika neno moja. Kutokana na mifano hii inaonekana kuwa ni vigumu kwa mkalimani kulandanisha maumbo katika ukalimani wa ujumbe kutoka matini chanzi hadi matini lengwa.Hii ni kwa sababu mpangilio wa maneno na upatanisho wa kisarufi hutofautiana katika sentensi za lugha moja na nyingine

Katika diskosi za kesi D, sentensi za kiongozi wa mahakama na ukalimani uliotokea unaonyesha kuwa usawa wa kipengele cha maumbo si rahisi ufikiwe katika ukalimani.

KM: *Theyarrestedhimandtookpossessionoftherecoveredbhang*.

MK:Walikushika na wakachukua hiyo bangi ambayo walikuwa wamekushika nayo.

KM: *Nootherpriorrecords*.

MK: Hakuna makosa hujawahi kufanya makosa huko mbeleni.

KM: *andthecaseisbeforethiscourt*

MK: na kesi ndio hii mbele ya hii korti na kushtakiwa na hii mashtaka.

Katika sentensi za Kiswahili maneno yaliyotumiwa ni mengi kuliko maneno ya sentensi za Kiingereza katika kueleza dhana ile ile. Maelezo ya ziada katika lugha ya Kiswahili yanasababisha kuwepo kwa maneno mengi kwa sababu mkalimani hakupata msamiati mwafaka katika lugha ya Kiswahili kwa baadhi ya maneno kama vile '*prior*'. Hivyo basi, maelezo ya ziada yalihitajika ili mkalimani apitishe ujumbe uliokusudiwa kwa mshtakiwa.

Pia, katika diskosi hii mkalimani alikalimani sentensi,

Jaji:*Isthattrue*?

MK: Hayo maelezo ni ya ukweli?

Ni wazi kuwa idadi ya maneno ni tofauti katika lugha mbili husika kwa sababu mkalimani analazimika kutoa maelezo ya ziada kuhusu neno la Kiingereza '*that*'.

Katika diskosi F, sentensi,

KM: *Theofficersarrestedhimandchargedhimwiththepresentcharges*.

MK:Maafisa walikushika na kukushtaki na mashtaka ambayo yako mbele ya korti.

Mkalimani alifuata mpangilio wa maneno katika sentensi ya Kiingereza lakini ikawa anajirudia katika sentensi ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu maumbo ya sentensi katika lugha hizi mbili husika ni tofauti. Mkalimani anapofuata mpangilio wa maneno katika lugha ya Kiingereza, anatatizika na kulazimika kujirudia ili aeleweke kwa mshtakiwa.

**4.5 Changamoto za Usawa wa Kipengele cha Mtindo**

Kipengele hiki cha mtindo kimechanganuliwa kwa kuzingatia mhimili muhimu wa mtindo katika nadharia ya usawa katika ukalimani.Mhimili huu unaeleza kuwa mtindo uliotumika katika MC unafaa kujitokeza katika ML kwa kuzingatia uaminifu. Mtindo unahusu matumizi ya tamathali za lugha kama vile tasfida, methali, jazanda, tashbiha, istiara na misemo katika matini husika.

Mitindo ambayo imechanganuliwa hapa inahusu tamathali za lugha zilizotumiwa katika diskosi za wahusika wa kesi zilizoteuliwaa na kukalimaniwa au kukosa kukalimaniwa katika LL. Ilibainika kuwa lugha ya mahakama ni rasmi mno na haina ucheshi na kwa hivyo ni nadra sana tamathali za lugha kutumiwa na wahusika wa kesi katika mahakama. Wengi wa wahusika wanawasilisha ujumbe uliokusudiwa pekee na mkalimani naye hukalimani kwa kufuata mtindo wa MC.

Kamusi ya Kiswahili sanifu TUKI (2000) inaeleza kuwa mtindo ni jinsi ya kufanya jambo kwa kufuata taratibu fulani.Maelezo haya ni ya jumla mno kwani hayajikiti kwenye mtindo wa lugha pekee.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa mtindo ni dhana inayorejelea jinsi ya kujieleza katika kazi ya kifasihi. Isitoshe, mtindo unaweza kuelezwa kuhusiana na mwandishi fulani anavyojieleza katika kazi yake. Uchunguzi wa mtindo unahusisha kuangazia uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, mbinu za kibalagha, miundo ya sentensi, sura na upana wa aya zake na hata uakifishaji wake. Kila mwandishi ana mtindo wake. Maelezo ya Wamitila yanajikita kwenye mtindo wa uandishi kwa jumla lakini mtafiti ameshughulikia mtindo katika lugha pekee. Dhana ya mtindo katika utafiti huu inalenga ufundi au ujuzi wa kujieleza kwa kutumia tamathali za lugha kama vile jazanda, tashibihi, tasfida,istiara, methali na misemo.

Kulingana na maoni yaMorris (1995), lugha ya kisheria mara nyingi hutumia msamiati ambao ni wazi bila matumizi ya lugha fiche. Taaluma ya kisheria haina matumizi ya mitindo ya mapambo kama ilivyo katika lugha ya kifasihi. Hata hivyo, wahusika kama vile walalamishi na mashahidi huenda wakatumia tamathali za usemi katika mawasilisho yao. Tamathali za usemi hata hivyo hutumiwa kwa nadra sana katika mazingira ya uendeshaji wa kesi katika mahakama kwani lugha rasmi ya kisheria hutumiwa.

Baadhi ya tamathali za usemi ambazo zilitokea katika diskosi za kesi zilizoteuliwa ni tasfida, misemo, na tashihisi. Mkalimani alikanganywa mno na matumizi ya tamathali hizo za usemi na mara nyingi ukalimani wake haukulandana kiujumbe hata kidogo kutoka LC hadi LL. Hii ni kwa sababu mkalimani hakumaizi visawe vya tamathali hizo katika lugha ya Kiswahili. Mkalimani alisahau ama alikosa kuelewa tamathali ambazo zina usawa kimaana na kimatumizi katika lugha ya Kiswahili. Tamathali za lugha zilizotumiwa katika diskosi za wahusika wa kesi katika mahakama ya Kericho zimeelezwa hapa. Mbinu za lugha zilizotumiwa katika diskosi hizi ni pamoja na tasfida, tashihisi na misemo. Mbinu hizi zimeelezwa kama ifuatavyo;

**Misemo**: Kamusi ya TUKI (2000) inaeleza kuwa msemo ni fungu la maneno linalotumiwa na jamii ya watu kwa namna maalumu ili kutoa maadili. Kulingana na utafiti huu, misemo ni fungu la maneno linalotumiwa na jamii ya watu kwa namna maalumu ili kutoa maadili fulani kwa njia fiche. Maana ya mafungu hayo ya maneno huwa fiche na hayategemei maana ya kawaida ya maneno yaliyotumiwa katika fungu lenyewe. Fungu hilo la maneno huwa na maana fiche inayokubalika na kueleweka kwa wanajamiilugha husika.

Katika diskosi ya kesi A, mkalimani amekalimani '*playingcards'* kuwa 'kucheza karate' ambapo alikosea kwa sababu alikanganywa na msamiati ambao hutumiwa katika msemo huo. Angekalimani msemo huo kuwa 'kucheza karata' ili kuleta dhana ya kucheza mchezo wa kadi ili

kushinda pesa kibahati-nasibu yaani mchezo wa kamari. Mchezo huu mara nyingi hutumiwa na matapeli kuwapunja pesa au mali watu wasiotilia shaka mchezo huo. Mchezo huu ni haramu nchini Kenya na wanaopatikana wakiucheza hutiwa mbaroni na kushtakiwa kwa kosa la unyang'anyi kwa udanganyifu.

Katika kesi E, mkalimani alikalimani msemo '*back-biting'* kuwa 'kukusema' na '*talkingbehindherback'* kuwa 'kukusengenya' badala ya kutumia msemo 'kumramba kisogo' ambao ni msemo wa Kiswahili ulio na maana sawa na ule wa Kiingereza uliotumiwa. Hapa, mkalimani alitumia msamiati wa kawaida badala ya msemo uliotumiwa katika diskosi hii. Hii inamaanisha kuwa katika ukalimani, mkalimani alikosa kutumia msemo unaolandana kimaana na ule wa lugha chanzi. Hii inaonyesha kuwa usawa katika ukalimani kuhusu mtindo wa misemi ni jambo gumu kufikiwa.

Pia, msemo wa Kiingereza, '*Raisealarm'* mkalimani alishindwa kuukalimani kwa sababu angetumia msemo wa Kiswahili 'piga unyende au piga mayowe au piga kamsa' misemo iliyo na maana ya kupiga kelele ili kupata usaidizi kutoka kwa watu.  Mkalimani badala yake alitumia msemo ambao haupo katika lugha ya Kiswahili na unazua maana tofauti 'fanya rabsha' yaani 'fanya vujo au kusababisha ghasia mahali fulani'. Katika hali hii, msemo wa Kiingereza una kisawe chake lakini mkalimani alikosa kukitumia kisawasawa kwani alichanganya maneno ya misemo miwili tofauti. Matokeo ya mchanganyiko huo ni kuwa maana ya misemo hiyo haikulandana. Hali hii inaonyesha kuwa ni vigumu kwa mkalimani kulandanisha kipengele cha misemo katika ukalimani wa matini kutoka LC hadi LL.

**Tasfida**: Tasfida ni suala la kimaadili katika matumizi ya lugha kutegemea utamaduni wa wanajamiilugha husika. Hivyo basi tasfida ni matumizi ya maneno yanayoficha lugha chafu,

lugha matusi, lugha ya kusababisha aibu, lugha ya kuibua hisia kali na lugha ya kutaja mambo ambayo ni mwiko katika jamiilugha husika.

Katika diskosi za kesi B, mkalimani alitumia mbinu ya tasfida na inaelekea kupoteza ujumbe uliokusudiwa inapokalimaniwa katika Kiswahili.  Kwa mfano, mkalimani amekalimani ‘*penis* au *genitals’* kuwa ‘sehemu ya uume’ na *vagina’* kuwa ‘sehemu ya siri’. Hapa kuna ukosefu wa usawa wa mtindo kutoka LC hadi LL kwani katika MC kiongozi wa mashtaka alitumia lugha ya kawaida lakini katika ML mkalimani alitumia mtindo wa tasfida. Hali hii inaonyesha kuwa ukalimani wa msamiati au lugha matusi (ambayo huchukuliwa kuwa mwiko kutajwa mbele ya watu katika utamaduni wa jamii nyingi za Kiafrika) inahitaji mkalimani kutumia tasfida au lugha ya heshima kwa sababu ya mahitaji ya kimaadili ya utamaduni wa lugha pokezi. Ukalimani kwa kutumia tasfida huwa mgumu kwa vile haieleweki ni sehemu ipi haswa inayorejelewa kuwa ya siri. Hii ni kwa sababu sehemu ‘ya siri’ katika jamii moja huenda ikawa si ya siri katika jamii nyingine kutegemea utamaduni wao.

**Tashhisi**: Kamusi ya TUKI (2000)inaeleza kuwa tashihisi ni usemi wa kumpa mnyama, sehemu fulani ya mwili au kitu kisicho na uhai uwezo wa kutenda kama binadamu. Hasa, huu ni usemi wenye kukipa kitu kisicho na uhai sifa za kitu chenye uhai.

Mbinu ya tashihisi imetumiwa mkalimani anapokalimani kuwa ‘sehemu ya uume iligusa sehemu ya siri ya msichana’ husika. Katika kutumia tashihisi mkalimani anaonekana kumwondoa mtendaji ambaye ni mshtakiwa kama binadamu mwenye kutenda kitendo hicho na kuiacha sehemu hiyo ya ‘uume’ kutenda kana kwamba hayo yalifanyika bila hiari ya mhusika, bila mhusika kujua au bila fahamu za mshtakiwa. Hali hii inaonyesha kuwa ni vigumu kulandanisha ujumbe mkalimani anapopania kulandanisha mtindo uliotumiwa katika LC na LL.

### 4.6 Changamoto Kuhusu Usawa wa Kipengele cha Toni Katika Ukalimani

Kipengele hiki kimechanganuliwa kwa kuzingatia nadharia ya usawa. Mhimili mmoja wa nadharia hii ya usawa unaeleza kuwa toni za kihisia katika ukalimani wa diskosi za wahusika inafaa kulandana katika MC na ML ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa. Kulingana na Koller (1979) toni huhusisha uhalisia na mandhari ya matumizi ya lugha na hutegemea hali ya msemaji, uteuzi wa msamiati na kiimbo na kidatu cha uwasilishaji. Utafiti huu umezingatia namna hisia mahususi ziliandamanishwa na ujumbe ulivyowasilishwa katika LC na namna wakalimani walivyouwasilisha ujumbe huo katika LL kitoni.

#### 4.6.1 Dhana ya Toni

Kwanza, inafaa kueleza dhana ya toni ili kufanikisha maelezo ya matokeo ya utafiti kuhusu changamoto za usawa wa toni katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi katika mahakama. Hii ni kwa sababu neno toni huzua mawazo mbalimbali kutegemea muktadha wa matumizi.

Kulingana na kamusi ya Kiswahili sanifu TUKI (2000), toni ni sauti ya kiwango fulani. Kamusi hii ina maelezo kuhusu toni yanayofanana na maana ya kidatu pekee. Kidatu ni kipimo cha sauti ya msemaji na kipimo hicho si lazima kidhihirishe hisia za msemaji. Kinachodhihirisha toni ni hisia nauteuzi wa msamiati anaoutumia msemaji ili kuwasilisha ujumbe wake kwa mlengwa.

Kwa mujibu wa Arege (2013) toni ni hisia za nafsineni zinazoibuka kutokana na uteuzi wake wa msamiati. Kuna toni za kubeza, kuchekesha, kuhoji, kulalamika, majuto, kuonyesha aibu, mamlaka, kudharau na hisia nyingine nyingi.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa toni ni sawa na lahana; dhana inayotumiwa kuelezea mkabala alionao msimulizi wa hadithi kwenye wahusika waliomo katika hadithi yake na matukio

yaliyomo katika hadithi. Utafiti huu unazingatia kuwa toni ni hisia zinazoandamana na ujumbe wa mhusika anapozungumza bila kutegemea kiimbo, kidatu cha sauti yake ila msamiati anaoutumia. Hisia hizo ni kama vile za huzuni, masikitiko, furaha, mapuuza, majuto, kejeli, hasira, dharau au mapenzi kutegemea ujumbe na uhusiano wa wahusika na muktadha wa ujumbe husika.

Maana ya toni ambayo imeshughulikiwa katika utafiti huu ni ile iliyoelezwa na Wamitila (2003) na Arege (2013). Mtafiti ameshughulikia hisia ambazo ziliandamana na diskosi za wahusika katika kesi zilizoteuliwa kwa kuzingatia msamiati ulioteuliwa kurejelea muktadha husika bila kujalisana kidatu na kiimbo cha sauti ya mhusika.

Toni ni kipengele kigumu kukalimani kwa sababu hakina maumbo yanayoonekana wazi. Hivyo basi, mara kwa mara wakalimani hukosa kufikiria kuzingatia toni katika ukalimani wao ila hujitokeza hasa iwapo ukalimani wa msamiati uliotumiwa ni sahihi. Katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi zote, kipengelekikuu kilikuwa ukalimani wa ujumbe uliowahusu wahusika wa kesi. Hakuna sauti ya ukali, huzuni au ghadhabu ambayo ilijitokeza wazi katika ukalimani wa diskosi husika ila katika msamiati wa ujumbe uliokalimaniwa.

### 4.6.2 Toni Iliyokalimaniwa Vilivyo

Katika diskosi za kesi zote toni za shutuma, masuto na lawama zimejitokeza katika ukalimani hasa mkalimani anapokalimani diskosi za kiongozi wa mashtaka na jaji. Hii ni kwa sababu mkalimani amekalimani diskosi za kiongozi wa mashtaka kwa ajili ya mshtakiwa ambaye anachukuliwa kuwa mhalifu wala si kwa ajili ya jaji au mlalamishi. Kwa mfano;

Katika diskosi za kesi A, jaji alitumia toni ya kuamrisha kuonyesha mamlaka yake kuhusu hali na uwezo wake wa kuwahukumu kulingana na matendo yao aliposema kuwa:

Jaji: *Eachoneofyouwillbeconvictedonyourownplea.*

Mk: Mtahukumiwa kwa vile mmeitikia mashtaka.

Viongozi wa mashtaka na washtakiwa walitumia toni ya shutuma kwani aliwashutumu washtakiwa alipotoa ripoti kuhusu kesi husika. Kwa mfano, katika diskosi hii ya kesi A, kiongozi wa mashtaka alipotoa maelezo yake kwa hakimu anaeleza kuwa:

Km*: You have been accused of cheating the public that you are playing cards and they will win money.*

Mk: Mmeshtakiwa kwa kosa la kucheza 'karate' kwa umma.

Toni ya shutuma ilivyojitokeza katika diskosi ya kiongozi wa mashtaka ndivyo imejitokeza katika toni ya masuto ya mkalimani anapomwambia mshtakiwa ujumbe uliowasilishwa na kiongozi wa mashtaka.

Kiongozi wa mashtaka anatumia toni ya unyenyekevu na lawamaanapowasilisha maelezo kuhusu kesi kwa jaji kama inavyoonyesha katika matini ifuatayo naye mkalimani anatumia toni ya masuto na lawama anapowaeleza washtakiwa kuwa ushahidi upo mbele ya mahakama na pale washtakiwa wanapokubali mashtaka kuhusu kesi yao iliyowakabili mbele ya mahakama.

Km: *I wish you to know that the accused have agreed that they were found in the said place and there were cards found in their possession which they used to play and fifty shillings which the officers found with them where they were playing cards. I have them and want to produce them as exibit for this case; the cards and the fifty shilling coins.'*

Mk: 'Kadi ambazo mlishikwa nazo na kiongozi wa mashtaka anataka kuzitoa na pia pesa shilingi hamsini anazitoa kama kielelezo'

Katika kesi A, ukalimani wa ujumbe huo wa kiongozi wa mashtaka, mkalimani alitumia toni ya kusuta na kushutumu washtakiwa kwa sababu anawatajia kuwa wanahukumiwa kwa makosa waliyoyafanya. Hapa toni ya kuhukumu na kulaumu washtakiwa imejitokeza katika LC na LPkatika diskosi ifuatayo.

> *Km: you were asking for money, you were caught with fifty shillings and fifty two cards.*
>
> Mk: Hapo mlikuwa mkitafuta pesa na mkapata shilingi hamsini na mlikuwa na kadi hamsini na mbili.

Katika diskosi za kesi B inabainika kuwa:

Kiongozi wa mashtaka anatumia toni ya lawama na shutuma anaposoma mashtaka ya mhalifu husika na mkalimani alikalimani kwa toni hiyo hiyo ili kuonyesha kughadhabishwa kwao kutokana na kitendo cha unyama alichokitenda huyo mshtakiwa. Hata hivyo, kutokana na msamiati uliotumiwa kueleza ujumbe mzima wa kesi husika, toni katika ukalimani ilibainika kuwa ni ya shutuma na masuto kutoka kwa kiongozi wa mashtaka, mkalimani na jaji.

> Km*: You are accused of raping (the girl who is five years old). Against the laws of Kenya.*
>
> Mk: Unashtakiwa na kosa la kumnajisi (msichana wa umri wa miaka mitano). Kinyume na sheria za Kenya.

Jaji na mkalimani wanatumia toni ya mamlaka wanapomuuliza mshtakiwa swali hili. Mshtakiwa alitumia toni ya kuonyesha aibu alipolijibu swali la hakimu kwa sauti ya chini na kutikisa kichwa. Kukana kwake kulichukuliwa bila ukalimani wowote. Inachukuliwa kuwa mshtakiwa alikuwa na hisia za aibu au woga alipojibu kwa sauti ya chini huku akiangalia chini.

Jaji*: True or false?*

Mk: Ni kweli ama si Kweli?

Mst: La.

Hakimu alitumia toni ya kuonyesha mamlaka anapotoa uamuzi mwishoni mwa kesi hii. Anamtaarifu mshtakiwa kuwa kwa vile amekataa mashtaka itabidi hakimu ampe mshtakiwa tarehe nyingine ahudhurie kikao kingine katika mahakama hiyo ili kesi yake kurejelewa. Mkalimani alikalimani toni hii ya hakimu barabara.

Jaji*: I will enter for you a plea of not guilty because you have denied the charges, you will be given another date.*

Mk: Umekataa maelezo, kwa hivyo korti itaandika kuwa umekataa mashtaka na utapewa tarehe.

Katika diskosi za kesi D, kiongozi wa mashtaka ametumia toni ya malalamishi kwa jaji kuhusu mshtakiwa aliyekamatwa na misokoto ya bangi naye mkalimani vile vile anatumia toni ya shutuma anapokalimani ujumbe huo kwa ajili ya mshtakiwa.

Km*: The AP officers ...found the accused person who looked suspicious and on approaching him, he started running away.They followed him and caught him. On inquiring and doing a search, they discovered twenty four rolls of bhang from his trauser pocket.*

Mk: Maafisa wa utawala …walikupata mshtakiwa ukionekana mshuku. Walipokukaribia ulianza kukimbia. Walikufuata wakakushika. Walikushikshikawaliendelea kupata misokoto ya bangi kutoka mfuko wa long'i.

Mshtakiwa anapojibu swali la jaji, toni ya majuto na masikitiko imejitokeza.

*Jaji: The accused, is all that true?*

Mk: Hayo maelezo ni ya kweli?

Mst: Kweli.

Pia, jaji na mkalimani wanatumia toni ya kuonyesha mamlaka baada ya mshtakiwa kuitikia na kukubali mashtaka yaliyomkabili.

*Jaji: You have been convicted on your own plea.*

Mk: Korti itakutolea hukumu, umekubali mashtaka.

Katika diskosi za kesi E, kiongozi wa mashtaka ametumia toni ya shutuma na malalamishi anapomwarifu jaji kuhusu mashtaka yanayomkabili mshtakiwa naye mkalimani anatumia toni ya shutuma anapokalimani ujumbe husika kwa ajili ya mshtakiwa.

Km: *You are accused of assault…when the accused went and confronted her there where she attacked her by scratching her…*

Mk: Umeshtakiwa kwa kumshambulia…wakati wewe mshtakiwa wakati ulienda na kumsimamia mahali pake. Uliweza kumshambulia kwa kumkwaruza…

Mwishoni mwa diskosi za kesi E, jaji anatumia toni ya kuonyesha mamlaka anapomuuliza mshtakiwa iwapo alikubali mashtaka au la. Mshtakiwa anatumia toni ya ghadhabu katika kujitetea na kutojali anapojibu kuwa mashtaka hayakuwa ya kweli. Toni ya mshtakiwa huenda ilitokana na maelezo kuhusu mashtaka yaliyokuwa ya uongo. Hata hivyo, toni hii haikujitokeza katika ukalimani kwa sababu matini hii haikukalimaniwa.

Jaji: Hayo maelezo ni ya ukweli au si ya ukweli?

Mst: Si kweli.

Katika diskosi za kesi F, toni ya lawama inajitokeza kiongozi wa mashtaka anapomsomea jaji mashtaka yaliyomkabili mshtakiwa kuhusu kesi hii na mkalimani vivyo hivyo anatumia toni ya lawama kwa mshtakiwa anapokalimani ujumbe wa kiongozi wa mashtaka kwa mshtakiwa.

Km: *At that particular time you did not have any entry permit or any authourization to allow you to be in Kenya…*

Mk: Hukuwa na *permit* yoyote au kibali ya kuonyesha kuwa ulikuwa umekubaliwa kuingia Kenya.

Vile vile, jaji katika matini yake alikuwa ameghadhabishwa na matendo ya mshtakiwa. Kwa mfano, alipomuuliza mshtakiwa kuitikia iwapo ni kweli au si kweli, alighadhabishwa na jibu la mshtakiwa ambaye haeleweki iwapo amekubali mashtaka au amekataa. Hata hivyo, mazungumzo ya jaji yalitokea katika lugha ya Kiswahili wala hayakukukalimaniwa. Mshtakiwa naye anatumia toni ya kuonyesha kughadhabika na kuchanganyikiwa. Mwishowe mshtakiwa anapokubali mashtaka anatumia toni ya kukubali shingo upande kwa sababu jaji amesema achague kama ni ukweli au la. Toni ya mshtakiwa kukubali shingo upande ilimfanya jaji kutaka mshtakiwa kusomewa mashtaka yake baadaye katika mahakama hiyo.

Jaji*: Is that true?*

Mk:Hayo maelezo ni ya kweli?

Mst: Maelezo ya mimi kukamatwa jana,

Jaji: Vile umesomewa, maelezo hayo ni ya kweli au si kweli?

Mst: Si kweli kwa sababu mimi nilipotea njia.

Jaji: Kwa hivyo maelezo hayo si ya ukweli?

Mst: Si ya ukweli kwangu ila ni ya ukweli kwenu kwa vile nilipotea njia.

Jaji: Ni kweli au si kweli?

Mst: Ni kweli.

Jaji: Sasa wewe unanichanganya! Kuja saa nane ili usomewe mashtaka yako tena.

**4.6.3 Toni Iliyokosa Kukalimaniwa Vilivyo**

Baadhi ya ukalimani ulikosa kuzingatia usawa wa toni iliyokusudiwa katika MC. Katika diskosi ya kesi A, kiongozi wa mashtaka anasema:

*KM: You have been accused of cheating the public that you are playing cards and they will win money*.

MK: Mmeshtakiwa kwa kosa la kucheza karate kwa umma.

Kiongozi wa mashtaka alitumia toni ya masuto na lawama lakini mkalimani alitumia toni ta kutaarifu. Hali hii pengine imetokana na tofauti ya waarifiwa. Katika kesi hii kiongozi wa mashtaka anamwarifu jaji huku mkalimani akimwarifu mshtakiwa.

Hali hii inajitokeza pia katika diskosi hii kiongozi wa mashtaka na mkalimani wanapowasilisha ujumbe huu:

*KM: You were asking for money, you were caught with fifty shillings and fifty two cards.*

MK: Hapo mlikuwa mkitafuta pesa na mkapata shilingi elfu, shilingi hamsini na mlikuwa na kadi hamsini na mbili.

Katika matini hii toni ilitofautiana hivi kwamba kiongozi wa mashtaka anatumia toni ya lawama na masuto akiwasilisha ujumbe kwa jaji lakini mkalimani anatumia toni ya kutaarifu mshtakiwa. Hali hii inajitokeza kwa sababu mkalimani alikosa kukalimani ujumbe wa kiongozi wa mashtaka ipasavyo. Katika ukalimani huu hata msamiati wa lawama haukutumiwa katika LL.

Katika matini hii toni iliyotumiwa katika MC ilikosa kukalimaniwa kwa sababu mkalimani alikosa kukalimani ujumbe uliotolewa na kiongozi wa mashtaka. Kwa hivyo, usawa wa toni ya masuto na lawama iliyokusudiwa haikumfikia mshtakiwa.

> Km*: I wish you to know that the accused have agreed that they were found in the said place and there were cards found in their possession which they used to play and fifty shillings which the officers found with them where they were playing the cards. I have them and want to produce them as exhibit for this case; the cards are here and the fifty shilling coins.*

Katika diskosi za kesi B, kiongozi wa mashtaka alitumia toni ya lawama akiwasilisha ujumbe wa mashtaka kwa mshtakiwa anapotumia msamiati kuhusu muktadha lakini mkalimani alitumia toni ya kuonyesha aibu anapoficha ujumbe uliokusudiwa kwa kutumia tasfida. Ukosefu wa usawa wa toni unajitokeza.

> *KM: Your penis penetrated the vagina of (name withheld) who is five years old.*
>
> MK: Uliweza kufanya sehemu yako ya uume kupenyeza sehemu ya siri ya msichana huyo ambaye ana miaka mitano.

Katika diskosi za kesi C, kiongozi wa mashtaka ametumia toni ya malalamishi anapotoa ripoti yake kwa jaji lakini mkalimani ametumia toni ya masutona shutuma anapomkalimania

mshtakiwa ujumbe husika. Tofauti hizi zimetokana na kiongozi wa mashtaka kukusudia kumtaarifu jaji huku mkalimani akimtaarifu mshtakiwa.

*Km: According to the complainant of this case who is Victor, who is a minor of eight years. The accused person took the complainant to transport for her sand.*

Mk: Kesi hii ambayo ni ya Victor, ambaye ni mtoto wa miaka minane. Wewe mshtakiwa, ulimchukua akusafirishie mchanga.

Katika kesi D, kiongozi wa mashtaka anatumia toni ya malalamishi akimtaarifu jaji kuhusu mhalifu na uhalifu alioufanya huku mkalimani akitumia toni ya masuto na shutuma anapomtaarifu mshtakiwa ujumbe ufuatao.

*KM: AP officers found the accused person who appeared suspicious and on approaching him he started running away.*

MK: Maafisa wa Utawala walikupata mshtakiwa ukionekana 'mshuku'. Walipokukaribia ulianza kukimbia.

Pia mwishoni mwa diskosi hii, jaji anatumia toni ya mamalaka lakini mkalimani anatumia toni ya kutaarifu bila hisia maalumu katika sehemu ifuatayo:

*Jaji: You have been convicted on your own plea.*

MK: Korti itakutolea hukumu, umekubali mashtaka.

Katika diskosi ya kesi E, inabainika kuwa kuna ukosefu wa usawa wa toni katika ukalimani wa matini hii.

*KM: You have been accused of assault of (name withheld) in Baraka Estate.*

MK: Umeshtakiwa kwa kumshambulia.

Ukosefu wa usawa wa toni unatokea kwamba kiongozi wa mashtaka anatumia toni ya lawama na masuto akimwarifu mshtakiwa makosa yake lakini mkalimani anamtaarifu mshtakiwa makosa yake bila kuihusisha toni yoyote.

Katika diskosi ya kesi F, kiongozi wa mashtaka ametumia toni ya kumtaarifu jaji uhalifu wa mshtakiwa huku mkalimani akitumia toni ya shutuma anapomtaarifu mshtakiwa makosa yake. Tofauti kuhusu usawa wa toni inajitokeza kwa sababu kiongozi wa mashtaka anamlenga jaji huku mkalimani akimlenga mshtakiwa.

Kulingana na matokeo ya uchanganuzi wa kipengele cha toni, inabainika kuwa hisia katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi katika mahakama hutegemea zaidi uteuzi wa msamiati wa kutumiwa katika muktadha wa matumizi. Kiimbo na kidatu cha uwasilishaji wa ujumbe husika si muhimu mno hasa katika diskosi za mahakama ambazo huwasilishwa kwa kidatu cha chini. Hii ni kwa sababu mkalimani na wahusika wote wa kesi mara nyingi hutegemea maadili ya mahakama. Mkalimani pia hutumiwa kama chombo cha kupitisha ujumbe na hana nafasi ya kuonyesha hisia wala mawazo yake binafsi katika matini anayokalimani. Hata hivyo, hisia za kuhukumu na kulaumu washtakiwa zimejitokeza kupitia msamiati matini husika. Ambapo mkalimani alikosa kutumia msamiati mwafaka na kukosa kukalimani matini husika, kulitokea ukosefu wa usawa wa toni katika MC na ML.

**4.7 Majibu kwa Maswali ya Utafiti**

Kutokana na utafiti huu, mtafiti ameweza kujibu maswali ya utafiti yaliyotumiwa kuongoza utafiti huu. Yafuatayo ni maelezo ya matokeo kuhusu maswali hayo ya utafiti na uhusiano wao na malengo ya utafiti huu.

**(i) Wakalimani wameweza kufikia usawa kamili wa ujumbe katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi kutoka LC hadi LL katika mahakama?**

Imebainika kuwa wakalimani walikalimani ujumbe waliouchukulia kuwa muhimu katika kesi husika. Baadhi ya wakati walikosa kufikia usawa wa kipengele chaujumbe katika ukalimani wao wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama. Ingawa wakalimani hao walitumia mbinu mbalimbali kukalimani ujumbe kutoka LC hadi LL, mara kwa mara walishindwa kuufikia usawa huo waujumbe kwa sababu ya ukosefu wa maarifa ya ukalimani katika taaluma ya kisheria na taaluma ya ukalimani na tafsiri kwa jumla. Pia,walikumbwa na ukosefu wa umilisi wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Vile vile, kutolandana kwa ujumbe katika MC na ML kulitokanana ukosefu wa muda wa kusikiliza ujumbe, kufikiria na kuzungumza. Wakati wote, wakalimani walitumia ukalimani fuatizilakini hawakuwa na muda wa kunakili yaliyosemwa na wahusika wa kesi na muda wa kutumia vifaa vya tafsiri kama vile kamusi. Mara kwa mara walidondosha baadhi ya ujumbe au kuchopeka ujumbe ambao haukuwapo katika MC. Mara kwa mara walikalimani visivyo ujumbe wa MC katika matini ya LL.

Imebainika kwamba wakalimani walikumbwa na changamoto za usawa wa kipengele cha ujumbe walipokuwa wakikalimani diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama. Hii ni kwa sababu LC na LL huwa na msamiati maalumu unaotumiwa ukiwa na maana ya kipekee katika taaluma hii ya kisheria.Inabainika kuwa ukalimani ni shughuli yenye dosari nyingi na ni ndoto kwa wanasheria kutarajia ujumbe katika tafsiri na ukalimani wa ML kulandana na ile ya MCwanavyodaiHale na Gibson (1999) na Olsen na wengine (2009).

**(ii) Wakalimani wamekumbwa na changamoto zozote za usawa wa kipengele cha maumbo katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi kutoka LC hadi LL katika mahakama?**

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, imebainika kuwa wakalimani waliohusika katika ukalimani wa diskosi za wahusika walikumbwa na changamoto za usawa wa kipengele cha maumbo. Mara kwa mara, wakalimani walikosa kukalimani maumbo kulingana na mpangilio wa maneno na upatanisho wa kisarufi katika LL na badala yake wakafuata mpangilio wa maneno yalivyotokea katika LC. Hali hii ilitokana na ukosefu wa ujuzi katika ukalimani kwa sababu wakalimani hawakusomea taaluma ya ukalimani inavyohitajika ili kuwa na ufasaha katika shughuli hii.

Katika uchanganuzi huu, imebainika kuwa wakalimani walichanganya mbinu ya ukalimani wa neno kwa neno na ukalimani sisisi katika shughuli yao kwa sababu haja yao kuu ilikuwa kukalimani ujumbe mkuu katika diskosi husika. Ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa, wakalimani walitumia mbinu bunifu ya kutoa maelezo marefu badala ya msamiati wa neno moja katika lugha ya Kiswahili. Mbali na maelezo marefu, wakalimani walitumia msamiati wa Kiingereza uliotumiwa katika MC au mara nyingine waliutohoza msamiati husika ili kuingiliana na maumbo ya lugha ya Kiswahili. Maumbo ya MC yalikosa kulandana kwa sababu katika lugha ya Kiswahili mofimu nyingi zinahurutishwa ili kuunda neno moja lenye maana nyingi kisarufi ambapo mara nyingi maneno ya Kiingereza yana maana moja au mbili pekee kisarufi. Imebainika kuwa tofauti hizi zinatokana na mifumu tofauti ya lugha husika kwa sababu hakuna lugha mbili zinazolandana kimaumbo anavyodai Nida (1976).

**(iii) Wakalimani walikumbwa na changamoto za usawa wa kipengele cha mtindo katika kukalimani diskosi za wahusika wa kesi kutoka LC hadi LL katika mahakama?**

Uchanganuzi huu pia umebainisha kuwa wakalimani walikumbwa na changamoto za usawa wa kipengele cha mitindo ya lugha katika ukalimani wa mitindo iliyotumiwa katika LC hadi LL.

Mara nyingi, badala ya kutumia mtindo uliotumiwa katika LC wakalimani walitumia maelezo marefu au walitumia mtindo ambao hauafiki ujumbe ambao ulikusudiwa katika MC. Hii ndiyo sababu walitumia maelezo marefu au tasfida katika MP. Madai ya Nida (1976) kuwa ni vigumu tamathali za lugha mbili kulandana yamebainishwa. Hapa, ibainike kuwa lugha ya mahakama ni rasmi mno hivi kwamba tamathali za lugha hutumiwa kwa nadra mno.

**(iv) Wakalimani walikumbwa na changamoto za usawa wa kipengele cha toni katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi kutoka LC hadi LL katika mahakama?**

Katika ukalimani wa ujumbe wa matini katika diskosi za wahusika katika kesi mbalimbali, toni ya MC ilibainika kutokana na msamiati uliotumiwa na pia kidatu na kiimbo cha mazungumzo. Mara nyingi toni ya kiongozi wa mashtaka katika LC ilikuwa ya malalamishi na shutuma kwa sababu alikuwa akiwasilisha mashtaka ya walalamishi wa kesi. Toni hii ilijitokeza mara kwa mara katika ukalimani katika LL kwani mkalimani alitumia toni ya shutuma katika uwasilishaji wa ujumbe wake kwa mshtakiwa. Toni ya majuto ilijitokeza katika diskosi za washtakiwa ambapo walikubali makosa waliyoshtakiwa nayo. Toni ya mamlaka ya hakimu ilijitokeza katika ukalimani ambapo mkalimani alikosa kukalimani diskosi ya hakimu baadhi ya wakati na hivyo alikosa kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa na hakimu. Tatizo la ukosefu wa usawa wa kipengele cha toni lilijitokeza pekee ambapo mkalimani alikosa kukalimani diskosiiliyotokea katika LC kwa LL na alipokosea kiujumbe.

Kwa jumla, imebainika kuwa shughuli ya ukalimani huwa na changamoto tele za usawa wa vipengele vya lugha mbili husika mara kwa mara wakalimani wanapojaribu kulandanisha vipengele vyote vya LC na LL. Hali hii ilisababishwa pakubwa na ukosefu wa elimu kwa wakalimani (makarani wa mahakama) kuhusu taaluma ya sheria na ukalimani. Hata hivyo,

wakalimani walitumia mbinu mbalimbali ili kuhakikisha kuwa ujumbe mkuu katika diskosi za wahusika umewasilishwa kwa waliowahitaji.

**4.8Hitimisho**

Sura hii imechanganua hali ya ukalimani katika diskosi za wahusika katika uendeshaji kesi katika mahakama. Vipengele vya usawa wa lugha vilivyozingatiwa katika ukalimani huu ni ujumbe, maumbo, mtindo na toni ya uwasilishaji katika matini asilia na usawa wake na ukosefu wa usawa huo katika matini lengwa. Ilibainika kuwa kulikuwa na changamoto za usawa wa vipengele hivyo vya lugha katika ukalimani wa diskosi hizo kwa sababu ya ukosefu wa mafunzo kuhusu taaluma ya ukalimani kwa wakalimani waliohusika.Wakalimani-makarani walionekana kutochangamkia kazi hii ya ukalimani kwa sababu waliiona kama kazi ya ziada isiyowahusu. Itafaa katika siku za usoni iwapo makarani wakalimani watakaoajiriwa watakuwa wamepokea mafunzo kuhusu taaluma ya ukalimani na tafsiri. Itafaa zaidi iwapo watakuwa na elimu kuhusu taaluma ya kisheria.

## SURA YA TAN0

## MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia muhtasari wa yaliyojiri katika utafiti huu, muhtasari wa matokeo ya uchunguzi kuhusu usawa wa vipengele vya lugha vilivyotafitiwa, mapendekezo kuhusu matokeo ya utafiti namapengo ya utafiti yatakayotafitiwa katika siku za usoni.

### 5.1 Muhtasari

Matokeo ya utafiti huu yametokana na data zilizokusanywa kutoka mahakama kuu ya Kericho kuhusiana na mada ya utafiti huu. Data zilizotumiwa katika uchanganuzi wa mada hii zilikusanywa kwa kutumia shajara maalumu na kalamu iliyotumiwa kuandikia diskosi na maelezo muhimu yaliyotokea katika mahakama wakati wa uendeshaji kesi. Kinasasauti kilikuwa kifaa muhimu zaidi katika kunasa diskosi hizo ili kusikilizwa na kunakiliwa baadaye katika tarakilishi kwa uchanganuzi wa maswali na malengo ya utafiti huu.

Data zilizoteuliwa zilihusu ukalimani wa diskosi kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili. Lugha hizi husika zinatumia othografia sawa katika maandishi lakini maumbo na mitindo katika lugha hizi ni tofauti. Vipengele vya lugha ambavyo vilifafanuliwa ni vya ujumbe, maumbo, mtindo na toni katika ukalimani baina ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili kulingana na malengo na maswali ya utafiti huu. Utafiti huu ulifanywa katika mahakama ya Kericho pekee. Wahusika walikuwa wa umri mbalimbali na walitoka jamii mbalimbali za Afrika Mashariki. Wahusika hawa walihitaji mkalimani kwa sababu walielewa Kiswahili lakini ilikuwa vigumu kwao kuelewa lugha ya Kiingereza.

Uchanganuzi stahilifu ulitumika ambapo maelezo kuhusu matokeo yalitolewa kwa kutumia maelezo wala si majedwali au takwimu. Maelezo yalitokana na uchanganuzi wa diskosi zilizotokana na kesi zilizoteuliwa kwa kutumia sampuli nasibu-horomo na sampuli makusudi ili kufaa mada ya utafiti huu.

Nadharia ya usawa ilifaa sana katika uchanganuzi wa data husika kwa sababu inadai na inadhihirisha kuwa hakuna usawa kamili baina ya lugha mbili kiujumbe, kimuundo, kimtindo na kitoni kwa sababu ya mwonoulimwengu wa mkalimani na utamaduni wa lugha mbili husika.

Lugha ya Kiingereza, lugha ya Kiswahili na lugha za mama zilitumiwa katika mawasiliano ya uendeshaji wa kesi katika mahakama ya Kericho kama inavyopendekezwa katika Katiba ya Kenya (2010). Mawakili, kiongozi wa mashtaka na jaji walitumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Hata hivyo, wakalimani walihitajika katika baadhi ya kesi ili kukalimani diskosi za kiongozi wa mashtaka kwa wahusika ambao hawakuelewa Kiingereza na walihitaji ujumbe husika kukalimaniwa katika lugha ya Kiswahili. Wakalimani hawakuhitajika kukalimani diskosi zilizotolewa katika lugha ya Kiswahili kutoka Kiswahili hadi Kiingereza kwa sababu majaji walikuwa wanaelewa Kiswahili na kutafsiri wenyewe kutoka Kiswahili hadi Kiingereza diskosi za wahusika wa kesi walipoandika rekodi zao kwa lugha ya Kiingereza.

Data za kesi sita zilizoteuliwa na kuchanganuliwa zilibainisha kuwa hakuna ukalimani baina ya lugha mbili ambao unaweza kulandana kwa kila namna katika vipengele vyote vya lugha vya lugha husika.Wakalimani walitumia mbinu zote za ukalimani yaanimbinu ya neno kwa neno, mbinu sisisi, ukalimani wa kisemantiki na pia kipragmatiki katika ukalimani wa diskosi hizo zilizohitaji kukalimaniwa. Kutokana na diskosi za kesi sita zilizoteuliwa kwa uchanganuzi, ilibainika kuwa wakalimani walikumbwa na changamoto za usawa wa vipengele vya lugha mbili husika (Kiingereza na Kiswahili) katika ukalimani wa diskosi za wahusika zilizotokea katika

mahakama. Changamoto hizo za usawa wa ujumbe katika ukalimani wao zilitokana na sababu kadhaa. Kwa mfano, kuwepo kwa vitate katika lugha ya Kiswahili, ukosefu wa msamiati maalumu wa kisheria na maadili ya lugha kufuatia utamaduni wa jamiilugha husika kuliwatatiza wakalimani. Pia, wakalimani walikosa kunyambua maneno ya lugha ya Kiswahili ipasavyo ili kuleta dhana iliyokusudiwa katika MC. Isitoshe, wakalimani walionekana kuchopeka baadhi ya ujumbeambao haukutokea katika MC walipohisi kuwa yalifaa kuwepo katika ML ili ujumbe uweze kueleweka vyema. Zaidi ya hayo, wakalimani walidondosha baadhi ya ujumbe ambao waliuchukulia kuwa haukuwa na umuhimu wowote katika ukalimani wa MC hadi ML. Hali hii iliibua kubadilika kwa ujumbe tofauti na ilivyokusudiwa katika MC.

Wakalimani walitumia tasfida kukalimani msamiati ambao unarejelea sehemu za mwili ambazo ni mwiko kutajwa hadharani katika utamaduni wa jamii nyingi za Kiafrika nchini Kenya. Kwa mhusika ambaye si Mwafrika, huenda akakosa kuuelewa ujumbe uliokusudiwa katika matumizi ya tasfida hizo, jambo ambalo huenda likamnyima mlalamishi haki yake kuhusu kesi husika.

Maumbo ya virai, vishazi pamoja na sentensi yaliwapa wakalimani changamoto kuyakalimani kwani lugha ya Kiingereza na ya Kiswahili huwa na masharti tofauti ya upatanisho wa kisarufi. Pia, maneno ya Kiswahili yanaweza kufumbata mofimu au viambishi ambavyo vina maana kisarufi tofauti na maneno ya Kiingereza ambayo mara nyingi huwa kitenzi kinafumbata nyakati pekee na nomino hufumbata umoja au wingi pekee. Hivyo basi, maumbo ya LC hayakuwa sawa hata katika matini yaliyokalimaniwa neno kwa neno katika LL.

Jambo jingine lililowapa changamoto wakalimani katika shughuli hii ni ukalimani wa tamathali za lugha zilizotumiwa. Wakalimani walishindwa kutumia visawe vya tamathali hizo katika lugha ya Kiswahili na badala yake wakatumia tamathali ambazo zina maana tofauti kabisa na tamathali zilizotumiwa katika MC. Pia, wakalimani walikosa kupata visawe vya baadhi ya tamathali za

lugha ya Kiswahili zinazolandana na zile za lugha ya Kiingereza hivi kwamba waliutumiamtindo wa maelezo ya kawaida.Wakalimani walishindwa kukalimani baadhi ya msamiati na kulazimika kutumia msamiati huo kama ulivyo katika Kiingereza au kuutohoa katika ukalimani wao katika lugha ya Kiswahili. Pia, wakalimani walitumia maelezo marefu ili kufafanua maana ya msamiati husika uliokosa kisawe chake moja kwa moja. Baadhi ya wakati walitumia tamathali ambazo zinakaribia kulandana kimaana na zile ambazo zingefaa kutumiwa.

Kulingana na Stolze (2013) kipengele cha toni huwa nachangamoto tele kwa sababu hakina maumbo maalumu bali hutegemea hali na mwonoulimwengu wa mkalimani. Mara nyingi, wakalimani walikalimani diskosi za wahusika bila kuonyesha hisia zozote. Hata hivyo, wakalimani waliwezakukalimani kwa usawatoni ya diskosi za majaji ambapo angalau waliweza kuonyesha hisia za mamlaka ya majaji. Toni ya onyo kali na mabezo kwa washtakiwa ilijitokeza wakalimani walipokalimani diskosi za majaji. Wakalimani walikalimani kwa usawa toni za viongozi wa mashtaka ingawa kiongozi wa mashtaka alikuwa akimweleza jaji malalamishi ya mlalamishi ilhali mkalimani alikuwa akimweleza mshtakiwa makosa au mashtaka yaliyokuwa yakimkabili katika mahakama. Kiongozi wa mashtaka alitumia toni ya malalamishi na shutuma alipokuwa akimweleza jaji mashtaka ya washtakiwa huku mkalimani naye pia akitumia toni ya shutuma alipokuwa akieleza washtakiwa mashtaka yaliyokuwa yakiwakabili mbele ya mahakama.

Matokeo ya utafiti huu yanabainisha kwamba wakalimani walikalimani ujumbe wa wahusika wakitumia maelezo marefu, wakikopa msamiati wa LC na wakitohoa msamiati wa LC. Hata hivyo, wakalimani hao walikumbwa na changamoto za ukalimani wa baadhi ya vipengele vya lugha. Changamoto kubwa zilitokana na maumbo ya sentensi katika LP, msamiati mwafaka katika LL unaolandana na msamiati wa LC, mitindo iliyotumiwa katika LC kukoseshwa visawe

vyake katika LP na ukosefu wa usawa wa ujumbe husika kwa jumla katika baadhi ya diskosi. Wakalimani walifikia usawa wa toni mwafaka mara kwa mara ingawa kiongozi wa mashtaka alikuwa akimwarifu hakimu ujumbe wake na mkalimani akimwarifu mshtakiwa ujumbe uliokalimaniwa. Wakalimani walidondosha au kuchopeka msamiati na kutoa maelezo marefu na baadhi ya wakati ujumbe husika ulibadilika.

Ilibainika kuwa wakalimani-makarani walikumbwa na changamoto za usawa wa vipengele vya lugha aghalabu katika ukalimani wao hasa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Changamoto hizo zilitokana na mkalimani kukosa msamiati mwafaka katika lugha husika, maadili ya kijamii kutokana na utamaduni wao na msamiati ambao ni mwiko katika lugha-pokezi, vitate katika lugha pokezi na tamathali za lugha ambazo hazipatikani katika lugha pokezi moja kwa moja. Pia, changamoto za ukalimani zilitokana na wakalimani husika kukosa umilisi wa lugha mbili husika hasa katika unyambuaji wa maneno ili kuyapa maana tofauti katika LP. Muundo wa LC (Kiingereza) na LP (Kiswahili) katika kesi husika ni tofauti ingawa othografia sawa hutumika katika maandishi katika lugha hizi mbili.

Kipengele cha toni kilikuwa kigumu zaidi kukalimaniwa kwa sababu hakina maumbo wazi lakini toni hiyo ilijitokeza kwenye uteuzi wa msamiati ulioutumiwa na wakalimani hao husika. Imebainika kuwa wakalimani walikumbwa na changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama kwa sababu hawana umilisi wa lugha zote mbili wala hawajapata mafunzo kuhusu taaluma ya ukalimani na pia kwa sababu hawana ujuzi na mafunzo maalum kuhusu taaluma ya kisheria.

Ilibainika kwamba suala la utafiti ambalo ni ‘changamoto zinazohusu usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama’ ni suala pana na muhimu katika taaluma ya kisheria na ukalimani. Hili ni suala nyeti katika

uendeshaji wa kesi katika mahakama kwa sababu wahusika wengi hawana umilisi wa lugha rasmi ya mahakama na sheria na kikatiba wana ruhusa ya kutumia wakalimani ili kuwasilisha ujumbe wao katika mahakama.

## 5.2 Mahitimisho

Data husika zilichanganuliwa katika kategoria zifuatazo; usawa wa ujumbe, usawa wa maumbo, usawa wa mitindo na usawa wa toni baina ya LC na LL. Kipengele cha ujumbe kiligawanywa katika sehemu ya ujumbe uliokalimaniwa vyema, ujumbe uliokalimaniwa visivyo, ujumbe uliochopekwa katika matini pokezi na ujumbe uliodondoshwa. Kipengele cha ujumbe kilichanganuliwa ili kudhihirisha kuwa ni vigumu kulandanisha ujumbe wa matini yote katika LC na LL. Ilibainika kwamba wakalimani walikosa kulandanisha ujumbe wa MC na ML kwa kuwa walidondosha ujumbe uliokusudiwa katika MC walipokalimani MC katika LC. Baadhi ya wakati ujumbe ambao haukujitokeza katika MC ulichopekwa katika ML. Fauka ya hayo, wakalimani walipotoza ujumbe wa MC walipotumia msamiati ambao una maana tofauti na ule uliotumiwa katika MC. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha maoni yaOlsen (2009) kuwa ni ndoto kwa wanasheria kutarajia ukalimani wa ML kulandana na MC kwa sababu shughuli ya ukalimani ina changamoto nyingi.Hale na Gibson (1999) wanasisitiza kuwa ukalimani ni harakati yenye dosari nyingi katika ulimwengu wenye dosari.

Matokeo ya uchanganuzi wa kipengele cha maumbo ya LC na LL yalidhihirisha kuwa maumbo ya leksimu, virai, vishazi na sentensi yalibainisha kuwa usawa wa maumbo hauwezi kufikiwa kwa urahisi katika LC na LL kwa sababu kila lugha ina kanuni zake za upatanisho wa kisarufi na utamaduni tofauti unaoelekeza maumbo ya kila lugha ya jamii husika anavyoeleza Stolze (2013) na Bucholtz (1995).

Isitoshe, Usawa wa tamathali za misemo, tasfida na tashihisi ulichanganuliwa ili kuonyesha kuwa usawa wa vipengele vya lugha mbili katika ukalimani ni jambo la kukisia kwani hakuna usawa mahususi baina ya mitindo ya lugha mbili zenye utamaduni na mazingira tofauti. Maoni ya Armstrong (2005) yamedhihirika wazi katika utafiti huu inapobainika kuwa misemo na tasfida zilizotumiwa katika MC zilikalimaniwa visivyo katika ML.

Kipengele cha usawa wa toni nacho kilichanganuliwa ili kuonyesha kuwa toni ni muhimu katika ukalimani kwa vile husaidia kupitisha hisia zinazoandamana na ujumbe uliowasilishwa. Kwa mujibu wa Armstrong (2005) ni vigumu kukalimani toni kwa sababu namna ya kuwasilisha hisia ni tofauti baina ya jamii-tumizi lugha tofauti. Katika utafiti huu toni ya MC ilikosa kukalimaniwa vyema katika ML hasa mkalimani alipopotoka kiujumbe na kwa sababu kiongozi wa mashtaka alikuwa akihawilisha ujumbe kwa jaji huku mkalimani akihawilisha ujumbe kwa mshtakiwa. Mara nyingi usawa wa toni ulijitokeza kutokana na uteuzi wa msamiati wa LL ili kuwasilisha ujumbe wa MC.

Imebainika kuwa taaluma ya ukalimani katika uendeshaji kesi katika mahakama ni uwanja unaohitaji kutengewa wakalimani waliohitimu kutoka vyuo vya mafunzo kuhusu tafsiri na ukalimani ili wahusika wa kesi wafaidi inavyopendekezwa katika Katiba Mpya ya Kenya (2010).

Matokeo ya utafiti huu yakitekelezwa, wakalimani ambao bado hawajapokea mafunzo kuhusu ukalimani na tafsiri watalazimika kusomea taaluma hizi. Hii ni kwa sababu wakuu wao wataelewa kuwa ni vigumu kupata usawa mahususi wa vipengele vya lugha katika ukalimani iwapo wakalimani hawajapata mafunzo maalumu kuhusu taaluma ya ukalimani ili kuboresha sifa zao za ukalimani. Wakalimani pia wataelewa kuwa wanafaa kuwa waaminifu kwa MC kila wanapokalimani diskosi za wahusika wa kesi katika mahakama ili kufanikisha haki ya wahusika inavyopendekezwa katika Katiba ya Kenya (2010). Iwapo mapendekezo ya matokeo ya utafiti

huu yatatekelezwa, makarani wa mahakama watafaidi kwa kuondolewa jukumu la ukalimani kwani mapendekezo yanadai kuwa wakalimani wote katika mahakama sharti wapate mafunzo maalumu kuhusu ukalimani katika taaluma ya kisheria. Kwa hivyo, ama makarani hao watadhaminiwa na mahakama kupata mafunzo kuhusu taaluma ya ukalimani na sheria au wakalimani waliohitimu watapata kazi katika mahakama ili kufanikisha ukalimani wa diskosi za wahusika katika mahakama. Mbali na wakalimani, matokeo ya utafiti huu yakitekelezwa, yatawafaa wahusika wa kesi mbalimbali ambao hawaelewi lugha ya Kiingereza na wanahitaji wakalimani ili kukalimani diskosi zao kama zinavyotokea katika mahakama kwa kuchaguliwa kiongozi wa mashtaka anayeelewa lugha yao na kusikilizwa na hakimu ambaye anaelewa lugha wanayoichagua kuwasilisha diskosi zao ili kusitokee changamoto zozote za usawa wa vipengele vya lugha kwa sababu hakuna lugha mbili ambazo zinalandana kabisa katika kila kipengele.

**5.3 Mapendekezo**

Kutokana na matokeo ya utafiti huu inapendekezwa kuwa:

Makarani wa mahakama ambao pia ni wakalimani wasiokuwa na mafunzo kuhusu taaluma ya ukalimani wapokee mafunzo ya muda mfupi kuhusu ukalimani. Pili, wawe walifuzu vyema katika lugha mbili rasmi zinazotumiwa katika ukalimani. Pia, itakuwa bora zaidi iwapo wakalimani katika mahakama watapokea mafunzo kuhusu taaluma ya kisheria hasa istilahi maalumu kuhusu sheria na ukalimani katika vikao vya uendeshaji wa kesi.

Lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha ya kitaifa na rasmi itumiwe katika uendeshaji wa kesi katika mahakama na wahusika wote wakiwemo hakimu, washtakiwa, mashahidi na viongozi wa mahakama ili makarani wa mahakama wasitumiwe kama wakalimani. Ikiwa haitawezekana, basi makarani wanaoajiriwa katika mahakama wapate mafunzo kuhusu taaluma ya kisheria na tafsiri au ukalimani kabla ya kuajiriwa. Hii ni kwa sababu makarani waliopo hawana ujuzi wala

mafunzo ya kutosha kuhusu taaluma ya ukalimani na hivyo hukumbwa na changamoto nyingi za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani.

Wakalimani ambao ni makarani wa mahakama wapewe taarifa ambazo zimetayarishwa mapema na viongozi wa mashtaka ili watafute msamiati unaofaa mapema badala ya kuja kutoa ukalimani wa papo kwa papo na kutatizika wakati wa uendeshaji wa kesi katika mahakama.

Vifaa vya kunasa diskosi za kesi zinazoendeshwa katika mahakama vitumiwe katika mahakama zote nchini. Vifaa hivyo ni pamoja na vinasasauti na kamera za video ili kurekodi yanayoendelea katika mahakama wakati wa kuendesha kesi. Rekodi hizi zinaweza kurejelewa wakati wowote na yeyote anayehitaji kurejelea diskosi hizo inapohitajika. Vifaa hivi ni muhimu kwa sababu mara kwa mara wahusika wengine hubadili wanayoyasema au wakalimani wanaweza kukosea katika ukalimani wao na kumkosesha mhusika haki yake.

Vitabu vya sheria vitafsiriwe katika lugha ya Kiswahili na msamiati unaotumiwa kuanzia kesi kuripotiwa hadi hukumu inapotolewa kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Pia, kamusi ya msamiati wa kisheria na msamiati unaotumiwa katika mahakama utafsiriwe katika Kiswahili ili kurahisisha ufahamu wa diskosi za wahusika wanapotumia msamiati wa kisheria katika mahakama.

Uwanja wa taaluma ya kisheria hasa diskosi zinazotokea katika mahakama ni mpana sana. Mengi yanaweza kutafitiwa katika uwanja huu yakiwemo suala la lugha na msamiati unaotumiwa na hakimu na mawakili katika diskosi zao katika uendeshaji kesi katika mahakama. Pia, utafiti unaweza kufanywa kuhusu changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji kesi katika mahakama ukizingatia lugha za kimaeneo, Kiswahili na Kiingereza. Uchunguzi pia unaweza kufanywa kuhusu namna utamaduni

huathiri mawasiliano katika ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi katika uendeshaji wa kesi katika mahakama kwani suala la utamaduni linafungamanishwa na lugha ya wanajamii husika.

## MAREJELEO


Aiello, T.F. (2013). *Translating Culture: Literary Translation into Swahili.* Swahili Forum 20. East African Translators.

Arege, T. (2013). *TunuyaUshairi*. Nairobi. The Oxford Place.

Armstrong, N. (2005). *Translation, Linguistics, Culture: A French-English Handbook.* Toront. Multilingual Matters Ltd.

As-Safi, A.B. (2007). *Translation Theories, Strategies and Basic Theoretical Issues*. Petra University.

Ayuk, A. Emmanuel (2015). *Discourse/TextualChallengesinLegalInterpretingandTranslation*. www.Pdf.

Baker, M. (1992). *On Other Words. A Coursebook on Translation.* London. Routledge.

Bandia, P. na Milton, J. (2009). *Agents of Translation.* Amsterdam. John Benjamins Publishing Company.

Bassnett, S. (2002). *TranslationStudies*: Third Edition: London and New York. Routridge.

Betlem, S.P. (2013). *Translation Studies: An Introduction to the History and Development of Translation.www.pdf.*

Bucholtz, M. (1995). *Language in Evidence: The Pragmatics of Translation in the Judicial Process*. University of California, Berkeley.

Catford, J.C. (1965). *A Linguistic Theory of Translation: An Essay in Applied Linguistics*. London. Oxford University Press.

Chomsky, N. (1957). *AspectsoftheTheoryofSyntax*. Cambridge, Massachusetts. MIT Press.

Choolun, N. (2009). *Lost in Translation? An Examination of Courtroom Interpreting in Australia*: Vol.2, No. 1. The University of Queensland, Australia.

Cozby, C.P. (2004). *Methods in Behavioral Research.* New York. The McGraw-Hill Companies Inc.

Crystal, D. (1997). *The Cambridge Encyclopedia of Language*: *Second Edition*. Cambridge. Cambridge University Press.

Deborah, S. na wengine (2001). *The Handbook of Discourse Analysis*. Malden, Massachusetts, USA. Blachwell Publishers.

Douglas, R. (1997, 2002). *WesternTranslationTheory*: *FromHerodotustoNietzsche*. Manchester. St. Jerome.

Echo, U. (1976). *ATheoryofSemiotics*. Bloomington. Indiana University Press.

Erickson, A. (2006). *ModelsofInterpreting: Simultaneous, Consecutive and Sight Translation.* Najit. Pdf.

Fawcett, P. *(*2003*). Translation Theories Explained.*Manchester, U.K. St. JoromePublishing.

Ghanooni, A.R. (2012). *AReviewoftheHistoryofTranslationStudies*. Finland. Academy Publishers.

Halliday, M.A.K. (1974). *ExplorationintheFunctionsofLanguage*. London. Edward Arnoid Publishers Ltd.

Hatman, B. na Mason, L. (1979). *TheTranslatorasCommunicator*. London and New York. Routeledge.

House, J. *(*1997*). A Model for Translation Quality Assessment:* A Model Revisited, Tubingen: Gunten Narr.

Iribemwangi,P.I. na Mukhwana, A. (2011). *Isimujamii*. Nairobi, Kenya. Focus Publishers Ltd.

Janigov'a, S. *(*2011*). Speech-acts Focus of Dynamic Equivalence in Legal Translation: Journal of Translation and Interpretation. Vol.5 No. 1.* Savarik University, Slovakia.

Jakobson, R. (1959). *OnLinguisticAspectsofTranslation*. Cambridge, MA. Harvard University Press.

Kinoti, H.W. *(*1998*). A Handbook of Social Research Methods.* Nairobi. TheNationalCouncilofchurchesofKenya.

Kombo, K.D. naDelno, L.A. Tromp, *(*2006*). Proposal and Thesis Writing: An Introduction.* Makuyu, Kenya. DonBoscoPrintingPress.

Kothari, C.R. *(*2004*). Research Methodology: Methods and Techniques. (Second Revised Edition).* NewDelhi. NewAgeInternational *(*P*)* Limited, Publishers.

Larson, M. (1997). *MeaningBasedTranslation*: *GuidetoCross-LanguageEquivalence*. University Press of America.

Maria E.R. na wengine (2009). *AgentsofTranslation*. Amsterdam. John Benjamins Publishing Company.

Marzocchi, C. *(*SSLMIT*). On Norms and Ethics in the Discourses on Interpreting.* UniversityofTrieste.

Mgullu, R.S. (1999).*MtalaawaIsimu*. Nairobi, Kenya. Sema Sasa Publications.

Moore, D.S. *(*1997*). Statistics: Concepts and Controversies.* NewYork. FreemanandCompany.

Morris, R. *(*1995*). Moral Dilemma of Courtroom Interpreting: The Translater, Vol. 1, No. 1.* Bar-IlanUniversity, Israel.

Munday, J. (2001). *IntroducingTranslationStudies*: *TheoriesandApplications*. London and New York. Routeledge.

Mugenda, O.M. naMugenda, A.G. *(*1999*). Research Methods: Quantitative and Qualitatative Approaches.* Nairobi, Kenya. ActsPress.

Mwansoko, H.J.M. na wenzake (2013). *KitangulizichaTafsiri*: *NadharianaMbinu*. TUKI: Dar es Salaam.

MyElimuForum *(*2014*). Misingi ya Tafsiri na Ukalimani (2014). MyElimu Forum 3-10-2014. www*.pdf.

Namakula, C.*S. (*2013*). The Impact of Language Diversity on the Right to Fair trial in International Criminal Proceedings, Uganda.* Johannesburg, 2013.

Newmark, P. *(*1988*). A Textbook on Translation.* Prentice-Hall, Europe. HemelHempstead.

Nida, E. naTaber, C.R. *(*1969*). The Theory and Practice of Translation.* Leiden*:* Brill.

Njagi, J. (2015). *TranslationFullofErrors*, *SaysRuto*. Daily Nation, Wednesday 21-01-2015:8, Kenya.

Obare, V. *(22/09/*2013*: 15-16). Taifa Jumapili: Tafsiri ya Maneno ICC Yazua Hisia Tofauti.*

Odhiambo, K. na wengine (2013). *TheoryandPracticeinLanguageStudies*: Vol.3, No. 6. Finland. Academy Publishers.

Olsen, F. na wengine (2009). *TheInternationalJournalofSpeech*, *LanguageandtheLaw*: *TranslationIssuesinLanguageandtheLaw*. Basingstoke, New York.

Owiti, B. (2014). *Meaning Loss in Interpretation: A Judgement Ruling in Nyando Magistrate's Court, Kenya.* Icit-presentation-pdf.

Peeter Torop (2002). *TranslationasTranslatingasCulture*. University of Tartu. Email: torop@ut.ee.

P'idalov, (1999). *The Language of the Law: Characteristics of the Courtroom Discourses.*www/pdf.

Ranjit, K. (2011). *Research Methodology*. New Delhi. Sage Publications Inc.

Republic of Kenya (2010). *The Constitution of Kenya, 2010*. Nairobi. Kenya National Law Reporting.

Russell, J. (1998). *Conference Interpreting Explained.* Manchester. St. Jerome Publishing.

Satia, E. (2013). *University of Nairobi Journal of Language and Linguistics*: Vol.3, 28-51.

Sierocka, H. (2014). *Studies in Logic, Grammar and Rhetoric: Cultural Dimensions of Legal Discourses*. Vol 38 (51). University of Bialystok.

Snell-Hornby, M. (2006). *The Turns of Translation Studies: New Paradigms or Shifting Viewpoint?* Amsterdam. John Benjamins.

Steiner, G. (1998). *AfterBabel*: *AspectsofLanguageandTranslation*. Third Edition. New York. Oxford University Press.

Stolze, R. (2013). *Translation and Law*: Synaps 28 (2013). TU Darmstadt.

TUKI. (2000) *AStandardEnglish-SwahiliDictionary*. Nairobi, Kenya. Printing Services Ltd.

Van den Broeck, R. (1981). *The Limits of Translatability Exemplified by Metaphor Translation: Poetics today.*Antwerp. Institute for Translations.

Venuti, L. (1995). *The Translator's Invisibility: A History of Translation.* London. Routledge Publishers.

Venuti, L. (1992). *Translation*: *HistoryandCulture*. London: Routledge.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia*. Nairobi. Focus Publications.

Wanjala, S.F. (2011). *MisingiyaUkalimaninaTafsiri*. Mwanza, Tanzania. Serengeti Education Publisher (T) L.T.D.

Wardhuagh, R. (2006). *AnIntroductiontoSociolinguistics*. Oxford. Blackwell.

Yule, G. (2006).*TheStudyofLanguage*.Cambridge.Cambridge University Press.

## VIAMBATISHO

**(a)(i) Barua ya kujitambulisha**

Kwa Bwana/Bibi mkalimani,

**KUMB: BARUA YA KUJITAMBULISHA KWA WAKALIMANI**

Jina langu ni Mwalimu Jane Machani kutoka Shule ya Upili ya Mabanati ya Kipsigis, Kaunti ya Kericho. Mimi ni mwanafunzi wa uzamili katika Chuo Kikuu cha Kabianga. Utafiti huu ni baadhi ya kazi inayohitajika ili kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili. Niko katika harakati za kukusanya data kuhusu 'Changamoto za usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama ya Kericho'.

Lugha mbili ambazo ninahitaji kuchunguza katika utafiti huu ni Kiswahili na Kiingereza katika harakati za ukalimani wa diskosi za wahusika wa kesi mbalimbali.

Ujumbe ambao utapatikana kutokana na majibu yenu utahifadhiwa kwa siri kuu na utatumiwa kwa ajili ya utafiti huu pekee.

Tafadhali andika jibu lako kwenye nafasi iliyoachwa baada ya kila swali. Ni muhimu kwamba uweze kutoa jibu ukizingatia ukweli iwezekanavyo.

Asante kwa ushirikiano wako.

Jane Machani

Nambari ya Simu: 0710242494

**(ii) Hojaji kwa Wakalimani**

Jaza majibu yako katika mapengo yaliyoachwa wazi. Unaweza kutumia lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Usiandike jina lako popote katika hojaji hii.

1. Umeajiriwa na serikali? ____________________________

2. Je, umepata mfunzo ya ukalimani wa diskosi za kisheria? ___________________

3. Je, umepata mfunzo ya kujikumbusha na kujifunza mambo mapya kuhusu ukalimani? ______________________; Mdhamini ni nani? ________________________________ Mara ya mwisho kupokea mafunzo hayo ni mwaka gani?_________________________________

4. Una ujuzi wa miaka mingapi? _____________________________

5. Kiwango chako cha masomo. ______________________________

6. Unaelewa utamaduni na desturi zinazoambatana na lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa ufasaha? ______________

7. Unakalimani diskosi husika ukizingatia unavyoelewa muktadha au unazingatia matumizi ya kila siku ya maneno husika? ______________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

8. Katika ukalimani wako, unazingatia viziada lugha vya wahusika na toni katika mawasilisho yao? ____

Kama jibu lako hapo juu ni ndio, unakalimani hisia na viziada lugha hivyo vipi ili kufikia usawa unaofaa?

_____________________________________________________________________________

9. Unakumbwa na changamoto zipi za usawa wa lugha katika kazi yako ya ukalimani?

10 .Mnahifadhi data za kesi katika mashine gani?

## (b) Barua Kutoka Chuo Kikuu cha Kabianga

UNIVERSITY OF KABIANGA
*ISO 9001:2008 CERTIFIED*
**OFFICE OF THE DIRECTOR, BOARD OF GRADUATE STUDIES**

29TH JULY, 2016

Ref: PGC/KIS/004/13
Ms. Jane Machani
Department of Linguistics Literature & Communication,
University of Kabianga,
P.O Box 2030- 20200,
KERICHO.

Dear Ms. Machani,

**RE: CORRECTED PROPOSAL**

This is to acknowledge receipt of two copies of your corrected Proposal entitled **"Changamoto Zinazohusu Usawa wa Vipengele vya Lugha katika Ukalimani wa Diskosi za Wahusika katika Uendeshaji wa Kesi katika Mahakama ya Kericho, Kenya."**

You are now free to commence your field work on condition that you obtain a research permit from NACOSTI.
Please note that, you are expected to publish at least one paper in a peer reviewed journal before final examination (oral defence) of your Masters thesis.

Thank you.

Yours Sincerely,

29 JUL 2016

PROF. J. K. KIBETT
for **DIRECTOR, BOARD OF GRADUATE STUDIES.**

C.C 1. Dean, SASS
2. HOD, Linguistics Literature & Communication
3. Supervisors

**(c) Barua ya Kibali kwa Utafiti Kutoka NACOSTI**

## NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION

Telephone: +254-20-2213471,
2241349, 3310571, 2219420
Fax: +254-20-318245, 318249
Email: dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke
When replying Please quote

9th Floor, Utalii House
Uhuru Highway
P. O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

KERICHO LAW COURTS
RECEIVED
05 OCT 2016
P.O. BOX 69, KERICHO
TEL: 052-20065

Ref: No.
NACOSTI/P/16/32263/13476

Date:
16th September, 2016

Jane Bosibori Machani
University of Kabianga
P.O. Box 2030-20200
**KERICHO.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on "***Changamoto zinazohusu usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama ya Kericho, Kenya,***" I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Kericho County** for the period ending **14th September, 2017.**

You are advised to report to **the Court Registrar, Kericho Law Courts, the County Commissioner and the County Director of Education, Kericho County** before embarking on the research project.

On completion of the research, you are expected to submit **two hard copies and one soft copy in pdf** of the research report/thesis to our office.

**BONIFACE WANYAMA**
**FOR: DIRECTOR-GENERAL/CEO**

Copy to:

The Court Registrar
Kericho Law Courts.

The County Commissioner
Kericho County.

*National Commission for Science, Technology And Innovation Is ISO 9001:2008 Certified*

**(d) Cheti cha Utafiti Kutoka NACOSTI**



THIS IS TO CERTIFY THAT:
*MS. JANE BOSIBORI MACHANI*
of KABIANGA UNIVERSITY, 1585-20200
KERICHO,has been permitted to conduct
research in *Kericho County*

on the topic: *CHANAGAMOTO ZINAZOHUSU USAWA WA VIPENGELE VYA LUGHA KATIKA UKALIMANI WA DISKOSI ZA WAHUSIKA KATIKA UENDESHAJI WA KESI KATIKA MAHAKAMA YA KERICHO, KENYA*

for the period ending:
*14th September,2017*

Permit No : NACOSTI/P/16/32263/13476
Date Of Issue : 16th September,2016
Fee Recieved :ksh 1000

*Applicant's Signature*

*Director General*
*National Commission for Science, Technology & Innovation*

**(e) Barua ya Mkurugenzi wa Elimu Kaunti ya Kericho**

# MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY

**STATE DEPARTMENT OF EDUCATION**

Email:cdekerichocounty@gmail.com
When Replying Please Quote:

County Education Office
P.O BOX 149
**KERICHO**

**REF:** KER/C/ED/GC/2/VOL.II/12

12th October, 2016.

**TO WHOM IT MAY CONCERN.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION – JANE BOSIBORI MACHANI.**

The above Student has been authorized by National Commission for Science, Technology and innovation to undertake research on ***"Changamoto zinazohusu usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama ya Kericho, Kenya,*** for a period ending 14th September, 2017.

Accord her the necessary assistance.

COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
12 OCT 2016
P.O. Box 149-20200 KERICHO

HELLEN NYANGAU
COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
**KERICHO COUNTY.**

**(f) Barua ya Kamishna wa Polisi Kericho**

THE PRESIDENCY

MINISTRY OF INTERIOR AND CO-ORDINATION OF NATIONAL GOVERNMENT

Telegrams: ..........................
Telephone: Kericho 20132
When replying please quote
kerichocc@yahoo.com

COUNTY COMMISSIONER
KERICHO COUNTY
P.O. BOX 19
KERICHO

REF: MISC.19 VOL.II/ (174)

5th October, 2016

**TO WHOM IT MAY CONCERN**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION –JANE BOSIBORI MACHANI**

Authorization has been granted to Jane Bosibori Machani, by National Commission for Science, Technology and Innovation, as per a letter Ref:No. NACOSTI/P/16/32263/13476 dated 16th September, 2016 to carry out research on ***"Changamoto zinazohusu usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama ya Kericho,Kenya,"*** for a period ending 14th September, 2017.

Kindly accord her the necessary assistance.

ANGELA WANYAMA
FOR: COUNTY COMMISSIONER
**KERICHO COUNTY**

## (g) Barua ya Mkurugenzi wa Mahakama ya Kericho

**ATelegrams: "COURT", Kericho**
**Telephone: Kericho 20065/81**
**When replying please quote**

**Ref: No.** JUD/KCO/GEN.29/11/16

**Chief Magistrate,**
**P.O. Box 69**
**KERICHO**

Date; **29th November, 2016**

HARAMBEE

# JUDICIARY

TO WHOM IT MAY CONCERN

**RE; RESEARCH AUTHORIZATION – JANE BOSIBORI MACHANI**

The above named student has been granted permission to carry out research on "*Changamoto zinazohusu usawa wa vipengele vya lugha katika ukalimani wa diskosi za wahusika katika uendeshaji wa kesi katika mahakama ya Kericho, Kenya,*" within Kericho Law Courts with effect from 16th September, 2016 to 14th September, 2017.

We wish her well in her endevours.

Kindly accord her necessary assistance.

SENIOR PRINCIPAL MAGISTRATE
KERICHO.

for

**HON. G.M.A ONGONDO**
**HEAD OF STATION**

**Data Iliyoteuliwa**

**Kesi A**

Kesi hii inahusu wanaume sita waliokamatwa na polisi wakicheza mchezo wa karata bila kibali wakiwatapeli wananchi katika mataa wa Nyagacho, Kericho. Wanaume hao walikuwa wa umri wa kati ya kumi na tisa hadi ishirini na mitano. Walikamatwa wakiwatapeli watu pesa wakitumia kadi katika mchezo wa karata.Hii ndiyo diskosi iliyotokea.

**Diskosi**

KM: *Youhavebeenaccusedofcheatingthepublicthatyouareplayingcardsandtheywillwinmoney*.

Mk: Mmeshitakiwa kwa kosa la kucheza 'karate' kwa umma.

KM: *without a licence, against the laws of Kenya.*

Mk: bila leseni kinyume na sheria za Kenya.

Km: *You all on 5/8/2015, at 7.00 Pm*

Mk: Mkiwa wote tarehe tano mwezi huu mwaka huu, saa moja jioni,

Km: *at Nyagacho, Kerichotown*

Mk: mkiwa Nyagacho, mji wa Kericho,

Km: *together, you were found by the officers, playing cards to the public without a licence*.

Mk: mlikuwa pamoja mlipatikana mkicheza mchezo wa 'karate' kwa umma na hamna leseni.

Km*: You were asking for money, you were caught with fifty shillings and fifty two cards*

MK: Hapo mlikuwa mkitafuta pesa na mkapata shilingi elfu, shilingi hamsini na mlikuwa na kadi hamsini na mbili.

Km: *Is that true or not true?*

Mk: Kweli ama si kweli?

Wst: Kweli. (Wote walikiri makosa).

Km*: I wish you to know that the accused have agreed that they were found in the said place and there were cards found in their possession which they used to play and fifty shillings which the*

*officers found with them where they were playing the cards. I have them and want to produce them as exhibit for this case; the cards are here and the fifty shilling coins.*

Mk: Na kadi ambazo mlishikwa nazo na kiongozi wa mashtaka anataka kuzitoa na pia pesa shilingi hamsini anazitoa kama kielelezo.

Jaji:  Ni kweli hizo kadi ndizo mlikuwa nazo na pesa?

Wst: Ndio.

Jaji: *Each one of you will be convicted on your own plea.*

Mk: Mtahukumiwa kwa vile mmeitikia mashtaka.

Jaji*: Any records?*

Km: *No records.*

Jaji: *What do you want to say in mitigation?*

Mk: Malilio mbele ya korti kabla ya hukumu.

Wst: (Wote wanaomba msamaha.)

Jaji: *I will call you shortly for your sentence.*

Mk: Mtaitwa baadaye ili kutolewa hukumu.

**Kesi B**

Mvulana wa umri wa miaka kumi na tisa alishtakiwa kwa kumnajisi mtoto wa kike wa umri wa miaka mitano.

**Diskosi**

Km: *You are accused of raping (name of the girl),*

Mk: Unashtakiwa na kosa la kumnajisi (jina la msichana),

Km: *against the laws of Kenya.*

Mk: kinyume na sheria za Kenya.

Km: *That on 4/7 this year,*

Mk: kwamba tarehe 4/7/ mwaka huu,

Km: *In Kericho area,*

MK: ukiwa Kericho *area*, eneo la Kericho,

KM: *In your full senses, against the law,*

Mk: kupenda kwako na, kinyume na sheria,

KM: *Your penis penetrated the vigina of (name of girl) who is five years old.*

Mk: uliweza kufanya sehemu yako ya uume, kupenyeza sehemu ya siri ya msichana huyo, (anataja jina) ambaye ana miaka mitano.

Km: *True or False?*

Mk: Ni kweli ama si kweli?

Mst: La.

KM: *You are accused of a second count of indescently touching the said girl's genital area, on 4/7/2015 at Kiptere.*

MK: Una shtaka la mbadala kuwa uliweza kupapasa sehemu za siri za (jina) 4/7/2016, ukiwa Kiptere.

KM: *In your full senses, against the law, your genitals touched the genital organ of the said girl who is five years old*.

Mk: ikiwa ni kupenda kwako kinyume na sheria uliweza kusababisha sehemu yako ya uume kugusa sehemu ya siri ya (jina la Msichana) ambaye ana miaka tano.

Km: *true or not true?*

Mk: Ni kweli au si kweli?

Mst: La (Anakana kwa ishara akiangalia chini).

Jaji; *So, a plea of not guilty has been entered for you.*

Mk: ……..

Jaji: *And the alternative.*

Mk: ……

Jaji: *You will be given another date of hearing.*

Mk: utapewa tarehe ya kusikilizwa tena

**Kesi C**

Kesi hii inahusu mtoto mvulana wa umri wa miaka minane kufanyizwa kazi na jirani yake na kulipwa badala ya kuenda shuleni. Mamake mtoto alimtayarisha kuenda shule na kuondoka kuenda kazi akidhani mwanawe ameenda shule. Hii ni kesi inayohusu hatia ya ajira kwa watoto.

**Diskosi**

Km: *On twenty eighth June this year,*

MK: Maelezo ni kwamba tarehe ishirini na nane mwezi wa sita mwaka huu

Km: *According to the complainant of this case who is Victor,*

Mk: Kesi hii ambayo ni ya Victor,

Km: *Who is a minor of eight years,*

Mk: ambaye ni mtoto wa miaka minane,

Km: *he was prepared by his mother to go to school*,

Mk: aliweza kutayarishwa na mamake ili aende shule

Km: *then she left for work.*

Mk: na mamake akaenda kazini.

Km: *The said person (name of the accused)*,

Mk: wewe mshtakiwa (jina la mshtakiwa),

Km: *took the complainant to transport for her sand,*

Mk: ukamchukua akusafirishie mchanga

Km: *which he did.*

Mk: ambayo alifanya.

Km: *he was ferrying the sand to the roadside.*

Mk: alikuwa anapeleka mchanga kando ya barabara.

Km: *She gave him food and he left by 1pm.*

Mk: Ulimpatia chakula na akaondoka saa saba mchana.

Km*: And she gave him twenty shillings.*

Mk: Na ukampa shilingi ishirini.

Km*: On twenty ninth June,*

Mk: Tarehe ishirini na tisa mwezi wa sita mwaka huu,

Km: *the complainant was prepared by his mother to go to school,*

Mk: huyo mlalamishi alitayarishwa na mamake aende shule,

Km: *but the said person (name of accused) called him and told him to work for her.*

Mk: wewe ulimuita tena ukamwambia akufanyie kazi.

Km: *He took the sand.*

Mk: Alichukua huo mchanga.

Km: *However, he was not paid because he did not finish and the rain started raining before lunch time.*

Mk: Hakumaliza. Mvua ilianza kunyesha kabla ya saa ya maakuli.

Km: *On thirtieth June this year,*

Mk: Tarehe thelathini mwezi wa sita mwaka huu,

Km: *and first July this year,*

Mk: pia tarehe moja mwezi wa saba mwaka huu,

Km: *and second July,*

Mk: na tarehe mbili mwezi wa saba,

Km: *the complainant worked for her.*

Mk: huyo mtoto aliweza kukufanyia kazi siku hiyo.

Km: *On second July 2016,*

Mk: na tarehe mbili mwezi wa saba mwaka huu,

Km*: when he was working for her,*

Mk: akiwa anakufanyia kazi kama kawaida,

Km*: he saw his mother coming,*

Mk: aliona mama yake akikuja,

Km: *as his mother had received information from the school,*

Mk: na mamake alikuwa amepata habari kutoka shuleni,

Km: *that he had not been attending school,*

Mk: kwamba hakuwa akienda shule,

Km: *and he had been informed by the members of the public*,

Mk: alikuwa ameambiwa na watu,

Km: *that he had been seen working for the accused person,*

Mk: kwamba walikuwa wamemuona akikufanyia wewe kazi,

Km: *and that is when she decided to track him.*

Mk: ndipo alikuja kumtafuta.

Km: *On second July when the complainant saw his mother*,

Mk: Na hii tarehe mbili mwezi wa saba wakati mlalamishi alimuona mamake,

Km*: when he was carrying sand,*

Mk: akiwa amebeba mchanga,

Km: *he ran away,*

Mk: alitoroka,

Km: *and his mother ran after him*.

Mk: lakini mamake alitoka kumukimbiza.

Km*: She caught him,*

Mk: Alimshika,

Km*: and took him to the police station*.

Mk: akampeleka *police station.*

Km: *After investigation,*

Mk: Baada ya uchunguzi,

Km: *the accused person was arrested*,

Mk: wewe ulishikwa, mshtakiwa,

Km: *and charged with the offence that is before this court*.

Mk: na ukashtakiwa na makosa ambayo yako kortini.

Km: *That is all.*

Mk: Ni hayo tu.

Jaji: *So is that true?*

Mk: Ni kweli ilikuwa hivyo?

Mst: Si ukweli, mtoto alikuwa anacheza uwanjani na watoto wangu wakisukumasukuma mchanga kwa barabara.

Jaji: Ati wanafanya nini?

Mst: wakichezacheza na mchanga huko kwa barabara.

Jaji: *I will enter for you a plea of not guilty because you have denied the charges you will be given another date.*

Mk: Umekataa maelezo, kwa hivyo korti itaandika kuwa umekataa mashtaka na utapewa tarehe.

**Kesi D**

Kesi ilihusu kijana wa umri wa miaka ishirini na sita hivi ambaye alikamatwa na misokoto ya bangi katika eneo la Fort Tenan.

**Diskosi**

KM: *The AP officers who were on there normal routine duty at Fort Tenan area.*

Mk: Maofisa wa utawala ambao walikuwa wakifanya kazi yao ya kawaida.

KM: *Shopping centre.*

Mk: *Area* ya Fort Tenan.

*KM: found the accused person who appeared suspicious and...*

Mk: Walikupata mshtakiwa ukionekana 'mshuku'.

*KM: On approaching him he started running away*.

Mk: Walipokukaribia ulianza kukimbia.

*KM: They followed him.*

Mk: walikufuata.

*KM: They caught him*

Mk: wakakushika.

*KM: On inquiring and doing a search they discovered*

Mk: waliku……

*KM: twenty four*

Mk: Walikushikashika waliendelea kupata

*KM: rolls of bhang*

Mk: misokoto ishirini na minne ya bangi

*KM: from his trouser pocket*

Mk: kutoka mfuko wako wa long'i.

*KM: They arrested him and took possession of the recovered bhang*

Mk: Walikushika na wakachukua hiyo bangi ambayo walikuwa wamekushika nayo

*KM: and escorted him to Fort Tenan Police Station where he was charged with the present charges*

Mk: Walikushindikisha mpaka kituo cha polisi cha Fort Tenan na kukushtaki na makosa ambayo yako mbele ya korti hii.

*KM: The recovered cannabis sativa is before court and I wish to produce it as exhibit*

Mk: Hiyo bangi ambayo ilipatikana iko mbele ya korti na kiongozi wa mashtaka angependa kuitoa kama thibitisho.

*Jaji: The accused is all that true?*

Mk: Hayo maelezo ni ya ukweli?

Mst. Kweli

*Jaji: You have been convicted on your own plea.*

Mk: Korti itakutolea hukumu umekubali mashtaka.

*Jaji: Any records?*

*KM: No other prior records.*

Mk: Hakuna rekodi hujawahi kufanya makosa huko mbeleni.

*Jaji: So, what do you say in mitigation?*

Mk: Una malilio?

Mst: Nina malilio.

Mk: Sema.

Mst: Nimekaa gerezani kwa mwezi mmoja.

**Kesi E**

Kesi hii inamhusu mwanamke wa umri wa miaka ishirini na mitano ambaye alishtakiwa kwa kumshambulia na kumjeruhi mwanamke mwingine katika mtaa wa Baraka, Kericho.

**Diskosi**

*Km: You are accused of assault of (name) in Baraka estate.*

Mk: umeshtakiwa kwa kumshambulia

*Km: The complainant namely (name) was at her place of work.*

Mk: Mlalamishi alikuwa mahali pake pa kazi.

*Km: when you the accused (name)*

Mk: wakati wewe mshtakiwa

*Km: went and confronted her there*

Mk: wakati ulienda na kumsimamia mahali pake

*Km: where she attacked her by scratching her*

Mk: uliweza kumshambulia kwa kumkwaruza

*Km: and injured her on her left side of the nose*

Mk: ulimjeruhi upande wake wa kushoto wa pua

*Km: and the upper right arm.*

Mk: na upande wa kulia

*Km: She was alleging that the complainant was backbiting her*

Mk: Alikuwa analalamika kuwa mlalamishi alikuwa akimsengenya

*Km: was talking behind her back that she had been beaten by her husband*

Mk: ulikuwa unadai kwamba mlalamishi alikuwa anakusema kuwa unapigwa na bwanako.

*Km: The complainant raised an alarm and was rescued by members of the public.*

Mk: Mlalamishi aliweza kupiga rabsha na raia waliweza kuja na kumsaidia.

*Km: She boarded a motorcycle and went to the police station where she reported her complaint.*

Mk: aliweza kuenda kituo cha polisi na kuweza kuripoti.

*Km: at Nyagacho Police Station*

Mk: Aliripoti Nyagacho Police Station

*Km: The complainant was treated at Kericho District Hospital and issued with a p3 form.*

Mk: na mlalamishi aliienda Kericho District Hospital na aliweza kujaziwa p3 form

*Km: The statements were recorded*

Mk: na mlalamishi aliweza kuandika statement

*Km: and the case is before this court*

Mk: na kesi ndio hii mbele ya hii korti na kushtakiwa na hii mashtaka.

Jaji: Hayo maelezo ni ya ukweli au si ya ukweli?

Mst. Si kweli.

**Kesi F**

Kesi hii inahusu kijana wa kiume, raia wa Tanzania, mwenye umri wa miaka ishirini na mitano hivi ambaye alipatikana katika mji wa Kipsitet, eneo la Kericho, nchini Kenya bila kibali.

**Diskosi**

*Km: On 4th /8/ 2016, that is yesterday, at around 11.00am*

Mk: Jana saa tano na nusu

*Km: Police officers who were at Kipsitet shopping centre*

Mk: Maaskari ambao walikuwa soko ya Kipsitet

*Km: were informed of the presence of the accused person in the shopping centre*

Mk: ………….

*Km: who was suspected to be of foreign national,*

Mk: kwamba ulishukiwa kuwa wewe si mtu wa Kenya, ni wa nchi ingine

*Km: the officers approached this person and on interrogation they actually established that he is a Tanzanian national.*

Mk; Maaskari walipokuja na kukuuliza maswali walijua kuwa wewe ni mwananchi wa Tanzania.

*Km: At that particular time, you did not have any entry permit or any authorization to allow you to be in Kenya.*

Mk: Hukuwa na *permit* yoyote au kibali ya kuonyesha kuwa ulikuwa umekubaliwa kuingia Kenya.

*Km: the officers arrested him and charged him with the present charges*

Mk: maafisa walikushika na kukushtaki na mashtaka ambayo yako mbele ya korti.

*Jaji: Is that true?*

Mk: Hayo maelezo ni ya ukweli?

Mst: Maelezo ya mimi kukamatwa jana

Jaji: Vile umesomewa, maelezo hayo ni kweli au si kweli?

Mst: Si kweli kwa sababu mimi nilipotea njia

Jaji: Kwa hivyo hayo maelezo si ya ukweli.

Mst: Si ya ukweli kwangu ila ni ya ukweli kwenu kwa vile nilipotea njia.

Jaji: Ni kweli au si kweli?

Mst: Ni kweli.

Jaji: Sasa wewe unanichanganya! Kuja saa nane ili usomewe mashtaka yako tena.